HALIUZWI

NATIONAL HEALTH INSURANCE FUND
NHIF
Dedicated to providing quality health Care

NHIF AFYA NJEMA

ISBN NO. 798-9987-9484 | TANZANIA | TOLEO LA 023 | SEPT. 2025

MAFANIKIO
YA MHE RAIS DKT. SAMIA SULUHU HASSAN
SERIKALI YA AWAMU YA SITA

YALIYOMO

UHAI NA UHIMILIVU WA NHIF WAIMARIKA- WAZIRI MHAGAMA....................................1
UTEKELEZAJI WA BIMA YA AFYA KWA WOTE - KATIBU MKUU (WA)....................................2
UPATIKANAJI WA BIDHAA ZA AFYA WAFIKIA 86% - NAIBU KATIBU MKUU (WA)....................3
HUDUMA ZA MATIBABU ZAIMARIKA NCHINI - MGANGA MKUU WA SERIKALI....................5
MPANGO MKAKATI WA MFUKO 6
NHIF YAIMARIKA - MWENYEKITI WA BODI YA WAKURUGENZI YA NHIF 9
WAJUMBE WA BODI YA WAKURUGENZI YA NHIF 10
MAFANIKIO YA MFUKO KIPINDI CHA MIAKA MINNE - MKURUGENZI MKUU....................11
UONGOZI WA JUU 13
NHIF INA WATUMISHI WENYE WELEDI 14
MAMENEJA KATIKA KURUGENZI NA VITENGO MBALIMBALI MAKAO MAKUU 17
NHIF YACHANGIA UBORESHAJI HUDUMA ZA MATIBABU KWA KUTOA MIKOPO YA VIFAA TIBA 18
WASIMAMIZI WA OFISI NDOGO ZA MFUKO 19
MAFANIKIO YA AWAMU YA SITA 20
MABADILIKO MAKUBWA KWENYE MATUMIZI YA TEHAMA 21
NHIF YAPUNGUZA MUDA WA KULIPA MADAI 25
WANANCHI KUJISAJILI WENYEWE KUPITIA MFUMO 27
UHAI WA MFUKO WAIMARIKA 29
UKAGUZI WA NDANI WAWEZESHA UPATIKANAJI HATI SAFI .... .31
NHIF YAPATA HATI SAFI ZA UNUNUZI 33
NHIF YADHIBITI UDANGANYIFU 35
MAFANIKIO YA NHIF KINONDONI 37
MBEYA YAPANUA WIGO WA VITUO VYA HUDUMA 39
HUDUMA ZA KIBINGWA ZAPATIKANA NDANI YA MKOA WA MANYARA 41

YALIYOMO

UWEPO WA NHIF SONGWE WACHOCHEA UPATIKANAJI WA HUDUMA 42
NHIF TABORA YASOGEZA HUDUMA KWA WANANCHI 43
IRINGA YATEKEKLEZA BIMA YA AFYA KWAWOTE 45
NHIF TANGA YALETA MAPINDUZI YA HUDUMA ZA AFYA 47
KATAVI - SAFARI YA MAFANIKIO NA MIKAKATI YA KUIMARISHA HUDUMA 49
NHIF RUKWA YACHOCHOEA UKUAJI WA BIMA YA AFYA KWA WOTE 50
TEMEKE - ONGEZEKO LA WANACHAMA LAPAA KWA 75% 51
MTWARA- WIGO WA WANACHAMA WAONGEZEKA 52
NHIF ILALA KINARA WA HUDUMA ZA BINGWA NA KIBINGWA BOBEZI 53
NHIF NJOMBE - MAFANIKIO YA MIAKA MNNE 57
NHIF KILIMANJARO - ELIMU DHANA BIMA YA AFYA YAONGEZEKA 59
NHIF MOROGORO YAJIKITA UTOAJI WA ELIMU YA AFYA 61
NHIF MARA NA MAFANIKIO YA AWAMU YA SITA 63
ARUSHA YAIMARIKA UPATIKANAJI HUDUMA ZA KIBINGWA 65
NHIF PWANI - WANANCHI WACHANGAMKIA BIMA YA AFYA 67
NHIF KIGOMA NA MAFANIKIO YA AWAMU YA SITA 69
NHIF GEITA YASOGEZA HUDUMA KWA WANACHAMA 71
NHIF MWANZA YABORESHA HUDUMA ZA MATIBABU 73
NHIF SHINYANGA - WIGO WA WANACHAMA WAONGEZEKA KWA 13.9% 75
NHIF KAGERA - HUDUMA BORA ZAVUTIA WANANCHI KUJIUNGA BIMA YA AFYA 77
NHIF LINDI YALETA CHACHU USAJILI WA WANACHAMA 78
NHIF RUVUMA YAFANIKIWA KUSAJILI VITUO 418 79
NHIF SINGIDA - HUDUMA ZA MATIBABU ZABORESHWA 80
NHIF SIMIYU - WANANCHI WAIKUBALI BIMA YA AFYA 81
NHIF DODOMA YAANZA UTEKELEZAJI WA BIMA YA AFYA KWA WOTE 82
TUGHE TAWI INAVYOSHIRIKIANA NA MENEJIMENTI....................................84

Bima ya afya kwa Wote,
Jiunge Sasa

Mhe. Jenista Mhagama (Mb)
Waziri wa Afya

UHAI NA UHIMILIVU WA NHIF WAIMARIKA

Waziri wa Afya, Mhe. Jenister Mhagama amelihakikishia Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kuwa uhai na uhimilivu wa Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya (NHIF) umeendelea kuimarika hivyo kuufanya Mfuko huo kuendelea kutoa huduma bora zaidi.

Amesema hayo mbele ya Bunge Juni 2, 2025, wakati akiliwasilisha hotuba ya bajeti ya mwaka wa fedha 2025/2026 ambapo aliweka wazi kuwa mapato ya NHIF yameongezeka kutoka Shilingi Bilioni 560.8 kwa kipindi cha Julai, 2023 hadi Machi 2024 na kufikia shilingi bilioni 619.8 kwa kipindi cha Julai 2024 hadi Machi 2025.

"Kutokana na kuimarika huku, Mfuko sasa umeweza kulipa Watoa huduma kwa wakati na katika kipindi cha kuanzia Julai 2024 hadi Machi 2025, jumla ya madai 55,817 yamechakatwa na jumla ya kiasi cha Shilingi Bilioni 438 sawa na asilimia 101 ya lengo kimelipwa," alisema Mhe. Waziri.

Alisema kuwa takwimu zinaonesha kuwa, fedha za NHIF kwa sasa zinachangia wastani wa asilimia 80 ya mapato ya vituo vya kutolea huduma za afya nchini. Mfuko umeendelea kuongeza wigo wa usajili wa vituo vya kutolea huduma za afya ambapo kwa kipindi cha kuanzia Julai 2024 hadi Machi 2025 Mfuko umesajili jumla ya vituo vya kutolea huduma 397 na kufanya jumla ya vituo vilivyosajiliwa na Mfuko kufikia 10,004 ambapo asilimia 72 ni vituo vya Serikali.

Akizungumzia usajili wa wanachama, Mhe. Waziri alisema kuwa katika kipindi cha Julai 2024 hadi Machi 2025, Mfuko umesajili wanachama wapya 462,408 sawa na asilimia 78 ya lengo la kusajili wanachama wapya 593,654. Aidha Mfuko unaendelea kubuni na kutekeleza mikakati mbalimbali ya kuongeza wanachama ikiwemo kutoa elimu mijini na vijijini ili kuhakikisha wanachama wengi wanajiunga na kunufaika na huduma za bima ya afya.

Kwa upande wa utekelezaji wa Sheria ya Bima ya Afya kwa Wote, Mhe. Waziri alisema kuwa sheria hii itawezesha wananchi kupata huduma za afya bila kikwazo cha fedha hivyo akaweka wazi kuwa utekelezaji wake unaanza mara moja.

UTEKELEZAJI WA BIMA YA AFYA KWA WOTE

Dkt. Seif Shekalaghe
Katibu Mkuu - Wizara ya Afya

Katika kuendeleza mapinduzi ya Sekta ya Afya yaliyofanywa na Serikali ya Awamu ya sita, Wizara imeainisha Vipaumbele mbalimbali vitakavyosaidia katika utekelezaji wa Bima ya Afya kwa Wote. Vipaumbele hivyo ni pamoja na;-

i. Kuimarisha huduma za kinga dhidi ya magonjwa ya kuambukiza yakiwemo magonjwa ya milipuko, magonjwa yaliyokuwa hayapewi kipaumbele, magonjwa yasiyoambukiza na huduma za Lishe;

ii. Kuimarisha upatikanaji na ubora wa huduma za afya zinazotolewa katika ngazi zote kuanzia Zahanati hadi Taifa;

iii. Kuimarisha huduma za afya ya uzazi, mama na mtoto ili kupunguza vifo vitokanavyo na uzazi na watoto wachanga;

iv. Kuimarisha upatikanaji na uendelezaji wa wataalam katika Sekta ya Afya kwa fani za kati, ubingwa na ubingwa bobezi;

v. Kuimarisha huduma za matibabu ya ubingwa na ubingwa bobezi pamoja na kuimarisha tiba utalii nchini; Kuendeleza na kusimamia afua za Tiba Asili na Tiba Mbadala;

vi. Kuimarisha upatikanaji wa huduma za tiba dhidi ya magonjwa ya kuambukiza, magonjwa yasiyoambukiza na magonjwa ya mlipuko;

Kutokana na vipaumbele hivi, Wizara kupitia Katibu Mkuu wake Dkt. Seif Shekalaghe ameutaka Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya (NHIF), kuhakikisha unapanua wigo wa elimu kwa wananchi na kuandaa miundombinu kwa lengo la utekelezaji wa bima ya afya kwa wote.

Lengo la bima ya afya ni kuwezesha upatikanaji wa huduma za matibabu kwa wananchi wote bila kuwepo na kikwazo chochote cha kifedha. Hatua itakayosaidia kuboresha afya za wananchi na kupunguza mzigo wa gharama za matibabu kwa familia.

Malengo haya pia yanakwenda sambamba na Dira ya Taifa ya Maendeleo ya 2050 ambayo Nguzo ya ya pili ya Uwezo wa Watu na Maendeleo ya Jamii, inajikita katika kujenga jamii yenye afya.

UPATIKANAJI WA BIDHAA ZA AFYA WAFIKIA 86%;

Wachochea Utekelezaji wa Bima ya Afya kwa Wote

Ismail Rumatila
Naibu Katibu Mkuu -Wizara ya Afya

Katika kipindi cha mwaka 2021 hadi 2025 hali ya upatikanaji wa bidhaa za afya muhimu za kipaumbele 290 ngazi ya vituo vya kutolea huduma za afya imeimarika kutoka asilimia 73 mpaka asilimia 86 sawa na ongezeko la asilimia 13.

1.0 UPATIKANAJI WA BIDHAA MUHIMU ZA AFYA KIPAUMBELE NGAZI YA VITUO VYA KUTOLEA HUDUMA ZA AFYA

Ngazi ya Vituo	2021/ 2022	2022/ 2023	2023/ 2024	Januari - Machi 2025
Zahanati	69%	49%	72%	78%
Vituo vya Afya	68%	52%	68%	76%
Hospitali za Wilaya	72%	61%	75%	81%
Hospitali za Rufaa za Mikoa	83%	93%	95%	97%
Hospitali za Kanda, maalumu na Taifa	73%	81%	92%	99%
Wastani	**73%**	**67%**	**80%**	**86%**

2.0 MAFANIKIO KATIKA KUKABILIANA NA MABADILIKO YA SERA ZA KIMATAIFA

Katika kukabiliana na mabadiliko ya Sera za Kimataifa kwenye uwezeshaji na ugharamiaji bidhaa za miradi misonge, Serikali imetoa jumla ya shilingi bilioni 141.98 kuwezesha ununuzi wa dawa za kufubaza virusi vya UKIMWI, dawa za malaria, vitendanishi kwa ajili ya UKIMWI na Kifua Kikuu na dawa za Uzazi wa Mpango

Katika hili, Serikali imejizatiti katika kuhakikisha mabadiliko ya sera za kimataifa katika uendelezaji wa sekta ya afya na hasa katika kuhudumia magonjwa yanayoambukiza hayana athari kwa wananchi, mpaka sasa Serikali ina akiba ya dawa na vitendanishi zinazotosheleza hadi ifikapo June 2026.

3.0 ONGEZEKO LA VIWANDA VYA KUZALISHA BIDHAA ZA AFYA NCHINI

Wizara ya Afya ina jukumu la kisera la kukuza na kulinda viwanda vinavyozalisha dawa na vifaa tiba nchini. Katika kuhamasisha uwekezaji wa viwanda vya dawa na bidhaa za afya nchini Wizara ya afya kwa kushirikiana na Kituo cha uwekezaji Tanzania (TIC). Kwa juhudi hizi zilizofanyika kumekuwa na ongezeko la idadi ya viwanda vya kuzalisha bidhaa za afya kutoka viwanda 23 mwaka 2020 hadi kufikia viwanda 87 Mei 2025 sawa na ongezeko la asilimia 73.5.

Kuimarika kwa uwekezaji wa viwanda vya dawa na bidhaa za afya nchini ambapo Wizara kwa kushirikiana na wadau mbalimbali imewezesha kuanzishwa kwa viwanda vipya 10 vya dawa na vifaa tiba.

Upatikanaji wa dawa zenye ubora, vifaa tiba vya kisasa na vitendanishi umesaidia kuhakikisha kila mwananchi anapata mahitaji yote muhimu ya msingi ya kimatibabu pale anapoenda kupata huduma katika vituo vya kutolea huduma za afya pamoja na upatikanaji wa ajira, kipato kwa wananchi na fedha za kigeni.

4.0 HUDUMA ZA DHARURA

Idadi ya hospitali yenye majengo ya kutolea huduma za dharura (EMD) zimeongezeka kutoka 7 hadi kufikia 116 Mei 2025 ikiwa ni ongezeko la hospitali 109. Kukamilika kwa ujenzi wa EMD kunapunguza vifo na kuokoa maisha kwa wagonjwa wa dharura na wa ajali. Kwa upande mwingine, idadi ya magari ya kubebea wagonjwa imeongezeka kutoka 540 mwaka 2021 hadi 1,267 Mei 2025.

Kwa sasa uwezo wa kuhudumia wagonjwa wengi zaidi wa dharura na ajali, ambapo uwepo wa huduma za dharura umepunguza idadi ya vifo kutoka 10 hadi 5 kwa wagonjwa wa dharura wanaofikishwa katika vituo vya kutolea huduma za afya.

UPATIKANAJI WA HUDUMA ZA UBINGWA BOBEZI
Serikali imeendelea kuboresha huduma za matibabu ya ubingwa na ubingwa bobezi katika Hospitali ya Taifa, Hospital Maalum, Hospitali za Kanda, na Hospitali za Rufaa za Mikoa ili kuhakikisha huduma hizi zinapatikana ndani ya nchi.

5.0 UTEKELEZAJI WA SHERIA YA BIMA YA AFYA KWA WOTE

Serikali imefanikiwa kuanza utekelezaji wa Sheria ya Bima ya Afya kwa Wote namba 161 kwa kukamilisha maandalizi ya Kanuni za Bima ya Afya kwa Wote. Hatua hii inawezesha Serikali kuanza utekelezaji wa awali wa Bima ya Afya kwa Wote kwa sasa Serikali inaendelea na uelimishaji wa wananchi unaohusisha viongozi wa ngazi zote ikiwemo ngazi za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa kwa lengo la kuwa na uwajibikaji wa pamoja. Hatua nyingine ya utekelezaji wa Sheria ya Bima ya Afya kwa Wote, Sura 161, ni kuanza kukusanywa fedha kutoka katika vyanzo mahususi kwa ajili ya kugharamia bima ya afya kwa wananchi wasio na uwezo kupitia Mfuko maalum ulioanzishwa ambapo hadi kufikia Februari, 2025 kiasi cha Shilingi za Kitanzania Bilioni 122.23 kilikuwa kimekusanywa.

Kukamilika kwa hatua hiyo kutawezesha Serikali kuanza kuwajumuisha wananchi wasio na uwezo kunufaika na huduma za bima ya afya. Vilevile, Serikali imeweza kusimamia Mfuko wa bima ya afya kwa umma na umeanza kuonyesha matokeo kwa wananchi kupata huduma kwa wakati bila kikwazo cha fedha.

Ujumbe mahususi: Utekelezaji wa sheria hii utawawezesha wananchi wote kuwa na uhakika wa kupata huduma za afya wakati wote bila kikwazo cha fedha hususan kwa kaya masikini. Vilevile, Sheria hiyo itawezesha vituo vya kutolea huduma za afya kuboresha huduma za afya zinazotolewa kwa wananchi kuleta usawa katika kupata huduma, kuwa na mfumo sahihi kuwa na uhakika wa matibabu kuanzia ngazi ya msingi mpaka Taifa.

Bima ya Afya kwa Wote, Jiunge Sasa

#BIMA YA AFYA KWA WOTE, JIUNGE

HUDUMA ZA MATIBABU ZAIMARIKA NCHINI

Dkt. Grace Magembe
Mganga Mkuu wa Serikali

Katika kutimiza azma ya Serikali ya kusimamia utoaji wa huduma za afya kwa wananchi ili kuwa na afya bora, Serikali imeendelea kuboresha miundombinu ya kutolea huduma za afya ikiwa ni pamoja na upatikanaji wa huduma za uchunguzi wa magonjwa, huduma za afya ya mama na mtoto,ongezeko la rasilimali watu, ongezeko la ujuzi katika utoaji wa huduma za afya na ushirikiano na sekta binafsi.

Katika kipindi cha Miaka minne ya Serikali ya Awamu ya Sita, kumekuwa na mafanikio makubwa katika sekta ya afya nchini katika ngazi zote, ikijumuisha upatikanaji wa huduma za Ubingwa bobezi, huduma za Kibingwa katika Hospitali za Rufaa za Mikoa na huduma ngazi ya Afya ya Msingi kwa lengo la kuimarisha upatikanaji wa huduma bora za afya kwa wananchi.

Uboreshaji huo umewezesha jumla ya fedha kiasi cha shilingi Trilion 8.9 kutumika katika sekta ya afya katika kipindi cha Serikali ya Awamu ya Sita toka ilipoingia madarakani na hivyo kuvunja rekodi ya ugharamiaji wa sekta ya afya.

Katika Kipindi hiki vituo vya kutolea huduma za afya vimeongezeka kutoka vituo 10,153 mwaka 2021 na kufikia vituo 12,846 Aprili 2025 ikijumuisha kliniki za magonjwa maalum na maabara binafsi. Mgawanyo wake ni kama ifuatavyo:

(i) Zahanati – 8,328
(ii) Vituo vya Afya – 1,254
(iii) Hospitali ngazi ya Wilaya - 361
(iv) Hospitali zenye hadhi ya Mkoa- 76
(v) Hospitali zenye hadhi ya Kanda- 18
(vi) Hospitali Maalumu – 6
(vii) Hospitali ya Taifa – 1
(viii) Kliniki za Magonjwa Maalum 1,013
(ix) Maabara Binafsi 1,676
(x) Vituo vinginevyo vikijumuisha Martenity home 113

Serikali imeendelea na maboresho ya miundombinu ya kutolea huduma za afya ikiwa ni pamoja na ujenzi wa majengo mapya, ukarabati na ukamilishaji wa majengo katika hospitali mpya katika mikoa mipya mitano. Maboresho hayo ni pamoja na;-

(i) Ukarabati wa majengo ya zamani na kuendelea na ujenzi wa jengo jipya la wagonjwa binafsi katika Hospitali ya Taifa Muhimbili;

(ii) Kukamilisha awamu mbalimbali za ujenzi wa hospitali ya Kanda ya Kusini Mtwara na hospitali ya Kanda Chato pamoja na upanuzi wa miundombinu katika Hospitali ya Rufaa ya Kanda ya Kaskazini - KCMC na hapa Serikali imejikita katika kuboresha huduma za tiba mionzi kwa kusimika mitambo na kujenga banka inayotumika katika utoaji wa huduma za mionzi, Hospitali ya Kanda Mbeya na Hospitali ya Benjamin Mkapa-Dodoma pia majengo yake ya kutolea huduma za Saratani yamejengwa na Hospitali ya Kanda ya Bugando Ujenzi wa Wodi ya wagonjwa wa Saratani umefanyika.

(iii) Serikali imefanya ukarabati majengo katika Hospitali maalum ikiwemo Hospitali ya Taifa ya Afya ya Akili Mirembe (Jengo la wodi ya kulaza wagonjwa) na Hospitali ya Magonjwa Ambukizi Kibong'oto (Jengo la utawala).

(iv) Kukamilika kwa ujenzi wa Hospitali mpya za Rufaa za Mikoa katika Mikoa ya Katavi, Njombe, Songwe, Simiyu na Geita pamoja na kuhamisha Hospitali tano (5) kutoka majengo yake ya zamani kwa kujenga Hospitali mpya katika maeneo mapya, Hospitali hizo ni Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Ruvuma, Shinyanga, Singida, Mara na Lindi.

(v) Serikali pia imefanya ukarabati na kujenga majengo mapya ya kutolea huduma za afya katika Hospitali za Rufaa za Mikoa ya Mtwara (Ligula), Mwanza (Sekoutoure), Kigoma (Maweni), Rukwa (Sumbawanga), Tabora (Kitete) na Mwanza (Ukerewe).

(vi) Vilevile Serikali imejenga na kukarabati miundombinu ya kutolea huduma za Afya ngazi ya

msingi ambapo Hospitali mpya za Halmashauri 135 zimejengwa, ukarabati wa Hospitali Kongwe 50 za Halmashauri umefanyika, ujenzi wa Vituo vya Afya 390, ikijumuisha Vituo 234 vilivyojengwa kwa fedha za tozo, ukamilishaji wa maboma ya Zahanati 980, ujenzi wa kituo cha kutibu magonjwa ya milipuko Kisopwa mkoani Pwani, ujenzi wa mitambo 41 ya kuzalisha hewa tiba ya oksijeni kwa ajili ya wagonjwa mahututi na Wagonjwa wa dharura na ujenzi wa nyumba za Watumishi 270 na kukamilika kwa mpango wa kuanza ujenzi wa Hospitali ya maalumu ya kutibu magonjwa ya kuambukiza mkoani Kagera. Vilevile, kukamilika kwa mpango wa kuanza isolation centers kwenye maeneo ya mipakani.

Maboresho makubwa yamewezesha Hospitali za Rufaa za Mikoa ambapo hivi sasa kila hospitali ina majengo yanayotoa huduma za dharura (EMD), mahututi (ICU), mama na mtoto (Maternity ward), upasuaji (Surgical), magonjwa ya ndani (internal Medicine), wagonjwa wa huduma za nje (OPD), huduma za kusafisha figo (Dialysis) pamoja na huduma nyingine za wagonjwa mahututi hasa kwa watoto wadogo (NICU).

Na.	AINA YA MASHINE	2020	Aprili, 2025	JUMLA
1	MRI	7	6	13
2	CT SCAN	13	32	45
3	ANGIO SUITE	4	2	6
4	FLUOROSCOPY	9	4	13
5	DIGITAL X-RAY	147	412	559
6	ULTRASOUND	476	494	970
7	PET SCAN	0	1	1
8	CATHLAB	1	3	4
9	Oxgen plant	0	25	25
10	DENTAL CHAIR	150	545	695
11	DENTAL X - RAY	20	518	538
12	3DCDCT	0	18	18
13	OPG	1	56	57

Aidha, Serikali inaendelea kuimarisha huduma za afya katika ngazi ya Kanda hadi Taifa ambapo, kwa upande wa Hospitali za Kanda, Hospitali ya Benjamin Mkapa inatarajiwa kupandishwa hadhi kuwa Hospitali ya Taifa, Hospitali Maalum za Mirembe kwa ajili ya afya ya akili na Kibong'oto ya magonjwa ya ambukizi zimepandishwa hadhi kuwa Taasisi.

Vilevile, kutokana na kuongezeka kwa magonjwa ya moyo nchini Serikali inaendelea na upanuzi wa Taasisi ya Moyo ya Jakaya Kikwete kwa kushirikiana na Serikali ya Jamhuri ya watu wa China ambapo jumla ya fedha za Kimarekani Dola milioni 24.9 zitatumika kugharamia upanuzi huo.

Ujumbe mahususi: Ujenzi na ukarabati wa miundombinu mipya imewezesha wananchi kupata huduma bora na muhimu karibu na maeneo wanayoishi. Vilevile, imeweza kuwapunguzia wananchi gharama za kutembea muda mrefu kufuata huduma mbali na maeneo yao lakini hata hivyo ujenzi na ukarabati umeweza kuchagiza mazingira wezeshi ya utoaji wa huduma za afya kwa wananchi kuwa rahisi kwa madaktari na watoaji wa huduma na sekta nzima ya afya.

Serikali imeendelea kushirikiana na sekta binafsi katika kuimarisha upatikanaji wa huduma za afya nchini, kama ifuatavyo:-

(i) Zahanati binafisi zimeongezeka kutoka 2,106 mwaka 2020 hadi kufikia 2,272 Aprili, 2025;

(ii) Vituo vya afya binafsi zimeongezeka kutoka 323 mwaka 2020 hadi kufikia 349 Aprili 2025 ; na

(iii) Hospitali binafsi zimeongezeka kutoka 173 mwaka 2020 hadi kufikia 212 Aprili, 2025 zikiwa katika hadhi mbalimbali kuanzia ngazi ya Wilaya, Mkoa hadi Kanda Idadi ya vitanda katika vituo vya umma kwa ajili ya wagonjwa mahututi (ICU) imeongezeka kutoka vitanda 185 vya mwaka 2021 hadi kufikia vitanda 1,362 Aprili 2025. Ongezeko hili limejumuisha vitanda vya wodi za watoto wachanga (NCU). Idadi ya vitanda vya wagonjwa katika vituo vya kutolea huduma za afya nchini imeongezeka kutoka vitanda 104,687 mwaka 2021 hadi vitanda 153,683 Aprili, 2025.

Huduma za Uchunguzi wa Magonjwa
Katika kuimarisha huduma za uchunguzi wa magonjwa kwa kutumia teknolojia za kisasa kwa wananchi, Serikali imenunua vifaa Tiba vya Uchunguzi na matibabu ya wagonjwa vyenye thamani ya shilingi Bilioni 228.1 ambavyo vinapatikana kuanzia ngazi ya Hospitali ya Taifa hadi Hospitali za Rufaa za Mikoa na Halmashauri. Maboresho haya yanalenga kumhakikishia mwananchi upatikanaji wa huduma bora za matibabu wakati wote.

STRATEGIC PLAN MAP
2021/22 - 2025/26



	STATEGIES	OUTCOME
• HIV, AIDS and NCDs reduced and supportive services enhanced;	• Strengthen HIV, AIDS and NCDs preventive measures • Enhance supportive care to staff with HIV, AIDS and NCDs	• Reduced number of new cases for HIV, AIDS and NCDs • Improved livelihood for staff with HIV, AIDS and NCDs
• Implementation of National Anti-Corruption Strategy enhanced and sustained;	• Enhance Good Governance and Anti-Corruption programmes	• Reduced corruption cases • High customer satisfaction • Increased revenues •
• Membership coverage of the Fund expanded;	• Expanding the use of ICT in advocacy and member registration; • Devising mechanism to reach members at all levels and the community at large; • Strengthening stakeholders' relationship in health insurance service provision; • Strengthening member	• Increased number of beneficiaries covered by the Fund.
• Access and quality of services provided to beneficiaries enhanced;	• Enforce service providers' compliance to regulations and protocols; • Enhance usage of technology in service provision; • Timely reimbursement of claims; and • Improve health facilities certification process	• Improved services to beneficiaries
• Revenue collection and Fund's sustainability enhanced;	• Enhance controls to curb fraudulent practice; • Ensure the Fund's solvency and financial sustainability; • Strengthen Risk Management; • Strengthen Business Continuity Management; • Strengthen revenue collection; • Strengthen mechanism for alternative financing; and • Strengthen evidence based decision	• Reduced fraudulent practices in consuming NHIF services • Sustainable Fund • Capacity of NHIF in revenue collection
• Institutional capacity enhanced;	• Strengthen performance management; • Strengthen monitoring and evaluation; and • Enhance conducive working environment	• Staff satisfaction • Good governance • Improved quality of services delivered • Availability of network connectivity • Better services
• Management of Environment and Ecosystem enhanced;	• Go green • Advocating for environmental cleanliness; and • Supporting environmental friendly practices	• Eco-friendly working
• National Multisectoral	• Advocating for healthy diet	• Improved staff health

NHIF YAIMARIKA

Bw. Eliud B. Sanga
Mwenyekiti wa Bodi ya NHIF

1.0 Kifungu cha 30 cha Sheria ya Bima ya Afya Sura 395 imeipa Bodi majukumu kwa lengo la kuhakikisha malengo ya uanzishwaji wa Mfuko yatimia. Majukumu hayo ni:-

i. Kuweka taratibu zinazohitajika kwa ajili ya usajili na uandikishaji wa wanufaika kwa mujibu wa Sheria,
ii. Kubuni mikakati mbalimbali ya udhibiti ili kuzuia matumizi mabaya ya huduma za afya;
iii. Kuwasilisha kwa Wizara ripoti ya mwaka ambayo itajumuisha hali ya Mfuko, jumla ya malipo yaliyotolewa, akiba, gharama wastani kwa wanufaika na takwimu nyingine yoyote muhimu kwa utekelezaji wa mpango huu;
iv. Kuunda ofisi yake, kuajiri Watumishi na kupanga mishahara na maslahi mengine ya kifedha kulingana na mahitaji na mapendekezo ya Mkurugenzi Mkuu;
v. Kusimamia utoaji wa Huduma za Afya na kukagua rekodi za kiafya na kifedha zinazohusiana na Mfuko wa watoa huduma za afya na wanufaika;
vi. Kubainisha masharti na kutoa miongozo kwa ajili ya uthibitisho wa vituo vya afya vilivyosajiliwa kufuatana na Sheria ya Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya;
vii. Kuhakikisha ukusanyaji au urejeshaji wa madeni na wajibu wote, ikiwemo michango ambayo haijalipwa, kwa manufaa ya Mfuko;
viii. Kuingia mikataba na mtu yeyote, kampuni, chama, shirika la ndani au la kigeni kwa ajili ya utekelezaji bora wa Sheria hii;
ix. Kuingia na kukagua vituo vya afya vilivyosajiliwa kwa kuzingatia kulingana na kanuni na masharti yaliyowekwa na Mfuko;
x. Kuandaa na kutekeleza miongozo kuhusu michango na manufaa, uhamishikaji wa manufaa, udhibiti wa gharama, uthibiti wa ubora, na mipangilio ya watoa huduma za afya, mikakati ya malipo na Mifumo ya rufaa;
xi. Kupokea na kusimamia mali, michango, na aina nyingine za misaada;
xii. Kukusanya, kuhifadhi, kuwekeza, kusimamia na kutumia fedha za mpango huu kulingana na masharti ya Sheria hii; na
xiii. Kutekeleza majukumu mengine yoyote yanayohitajika kwa ajili ya kufanikisha malengo ya Mfuko na utekelezaji mzuri wa masharti ya Sheria hii.

2.0 Bodi imekuwa ikiisimamia Menejimenti ya Mfuko katika maeneo mbalimbali ili kuhakikisha huduma zinazotolewa ni bora, uzingatiaji wa miongozo mbalimbali hususan ya kifedha pamoja na uhai na uendelevu wa Mfuko. Usimamizi huo umejikita kwenye;-

i. Usajili wa Wanachma kwa lengo la kupanua wigo huo
ii. Utoaji wa Huduma na udhibiti wa Ubora
iii. Uwekezaji wa ziada ya fedha inayopatikana ili kuimarisha uhai na uendelevu wa Mfuko
iv. Malipo ya Madai kwa Watoa Huduma;
v. Sera za Kudhibiti Vitendo vya udanganyifu.

3.0 Ukuaji Mkubwa wa Rasilimali

Kuongezeka kwa thamani ya rasilimali za Mfuko kwa 22.91% kati ya mwezi Julai, 2024 hadi mwezi Juni, 2025; Hii imewezesha Mfuko kulipa madai ya watoa huduma kwa wakati na hivyo kupunguza malalamiko. Muda wa malipo umepungua kutoka siku 120 mwaka 2023/24 hadi siku 55 mwaka 2024/25. Hayo ni mafanikio makubwa ikilinganishwa na matakwa ya kisheria kulipa madai ndani ya siku 60;

4.0 Mradi wa TEHAMA

Utekelezaji wa mradi wa TEHAMA kwa kutumia wataalam wa ndani ambapo kwa mwaka 2024/25 Mfuko umeokoa kiasi cha Shilingi bilioni 3.5, mradi huu umepunguza matumizi ya karatasi (Claim forms) kwa 75% kutokana na kuchakata madai kupitia Mifumo. Pia mradi umepunguza gharama za Kuchapisha Kadi za wanachama kwa 80%. Hivi sasa wanachama wanatumia kadi za kielektroniki (e-card), mradi huo pia umeboresha huduma kwa wanachama kupitia huduma ya NHIF Jihudumie (NHIF Self-Service) ikiwemo Kuchakata madai kidigiti umeongeza ufanisi na kupunguza vitendo vya udanganyifu. Mafanikio makubwa ya mradi huo wa TEHAMA yaliwezesha kupata tuzo ya mshindi wa pili kati ya miradi bunifu ya TEHAMA kitaifa kwa mwaka 2024/25;

5.0 Kupambana na Vitendo vya udanganyifu

Mfuko umeendelea kupambana na udanganyifu ambapo kwa mwaka 2024/25 Mfuko ulifungia vituo mbalimbali ambavyo vilijihusisha na udanganyifu. Aidha, Mfuko ulipeleka orodha ya majina ya Wataalam wa afya waliojihusisha na udanganyifu kwenye mabaraza yao ya kitaaluma kwa hatua zaidi.
Uhimilivu wa Kifedha Ulioimarika

Kuimarika kwa uhimilivu wa Mfuko (sustainability) kutoka miezi sita mwaka 2024 hadi uhimilivu wa miezi 18 (funding level of 1.6yrs) mwaka 2024/25; Hatua hii inaweka msingi imara wa huduma za matibabu kwa wanachama wake.

WAJUMBE WA BODI YA WAKURUGENZI YA NHIF

Bw. Eliud B. Sanga
Mwenyekiti wa Bodi ya NHIF

Prof. George M. Ruhago
Mjumbe wa Bodi

Bi. Veronica Kishala
Makamu Mwenyekiti wa Bodi

Prof. Kaushik L Ramaiya
Mjumbe wa Bodi

Bw. Shaban A. Kabunga
Mjumbe wa Bodi

Bi. Zubeda Chande
Mjumbe wa Bodi

Bw. Amoury Amoury
Mjumbe wa Bodi

Bw. Dickson Kaambwa
Mjumbe wa Bodi

Dkt. Irene C. Isaka
Mkurugenzi Mkuu wa NHIF

MAFANIKIO YA MFUKO KIPINDI CHA MIAKA MINNE

MWAKA WA FEDHA 2020/21 hadi 2024/25

1.0 Utangulizi

Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya (NHIF) umeendelea kuimarika kupitia mikakati mbalimbali ya usimamizi, rasilimali watu na upanuzi wa wigo wa wanachama, ili kufanikisha azma ya Serikali ya kuhakikisha kila Mtanzania anapata huduma ya afya kupitia Bima ya Afya kwa Wote. Kwa mujibu wa Sheria ya Bima ya Afya Sura 395 Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya una jukumu la kusajili wanachama na waajiri, kusajili vituo vya afya vilivyo idhinishwa na Wizara ya Afya; kulipa madai kwa watoa huduma; kuwekeza, na kusimamia vihatarishi.

2.0 HALI YA MFUKO KWA UJUMLA

Mapato ya Mfuko yameongezeka toka Bilioni 570 mwaka 2020/21 hadi Bilioni 836 mwaka 2024/25. Mapato haya yanajumuisha mapato yatokanayo na michango ya wanachama, mapato ya uwekezaji na mapato toka vyanzo vingine. Michango ya wanachama imeiongezeka toka Bilioni 489.5 hadi Bilioni 772 mwaka 2025. Gharama za utawala zimepungua toka Bilioni 98 mwaka 2021 hadi bilioni 67 mwaka 2025. Kupungua kwa gharama kumetokana na kubana matumizi uendeshaji na kuongezeka kwa matumizi ya TEHAMA ambayo impepunguza matumizi ya karatasi na kuchapisha kadi za wanachama.



Katika kipindi hicho Gharama za huduma kwa wanachama zimeongezeka toka Bilioni 8 hadi billion 15.9, ongezeko hili linatokana na kuongezeka kwa huduma kwa wanachama. Uhimilivu wa Mfuko umeongezeka toka nakisi ya Bilioni 110 mwaka 2021 hadi kuwa na ziada ya Bilioni 223 mwaka 2025. Ziada hii imewezesha Mfuko kulipa madai kwa wakati ambapo muda wa kulipa madai umepungua toka wastan wa siku 120 hadi siku 55. Ziada hii imewezesha kutengeneza vifurushi ili kuwezesha mwananchi mmoja mmoja au vikundi kuweza kupata bima nafuu. Uwiano wa michango na madai(medical loss ratio) imepungua toka 122% mwaka 2021 hadi asilimia 69% mwaka 2025. Uwiano wa hifadhi ya matumizi umeongezeka toka akiba ya miezi 7 mwaka 2023 hadi kuwa na akiba ya Mwaka mmoja na miezi 6 mwaka 2025. Mwenendo wa mapato na matumizi unaonesha matumizi yameendelea kupungua na hivyo kuwezesha ziada kuanza kuzalishwa toka 2023/24 (Mchoro Na.1).

3.0 MALIPO KWA VITUO VYA AFYA

Katika kipindi cha Miaka minne Mfuko umelipa jumla ya shilling Trilioni Tatu kwa watoa huduma. Kati ya malipo hayo asilimia 40% imelipwa kwa vituo vya Sekta Binafsi na asilimia 34 imelipwa kwa Vituo vya Serikali.



Kati ya malipo hayo Jumla ya Shilingi Bilioni 370.5 zimelipwa kwa huduma za matibabu kwa wastaafu.

4.0 IDADI YA MAHUDHURIO

Takwimu zinaonesha kwamba mahudhurio yamekuwa yakiongezeka na Mfuko umelipia jumla ya mahudhurio Milioni 64.3 kama inavyoonekana kwenye jedwali. Katika kipindi husika kiwango cha makato ya malipo kwa vituo yamepungua toka wastani wa 18% hadi kufikia wastan wa asilimia 8%. Vile vile aging ya malipo ya madai imepungua toka wastan wa siku 120 hadi kufika wastan wa siku 55 mwaka 2025.

Idadi ya Mahudhirio 2020/21 hadi 2024/24		
Vituo	Mahudhirio	
Mashirika ya Dini	15,734,414	24%
Vituo vya Serikali	20,351,371	32%
Vituo vya Sekta Binafisi	28,256,359	44%
Jumla	64,342,144	100%

5.0 MIKOPO YA VIFAA TIBA

Mfuko umetoa mikopo yenye thamani ya shilingi Bilioni 17.2 ambapo kiwango cha asilimia 37 ilitolewa kwa vituo vya Serikali.



Mikopo hiyo ilikuwa ni kwa ajili ya vifaa Tiba, ukarabati wa Vituo pamoja na dawa ambapo 66% ya mikopo ilitolewa kwenye vifaa tiba.

5.1 Aina ya Mikopo Iliyotolewa 2020/21 hadi 2024/25

Aina ya Mkopo	Shilingi bilioni	Asilimia ya Jumla
Vifaa Tiba	11.3	66%
Ukarabati Vituo	2.7	16%
Dawa	3.2	19%
Jumla	17.2	

6.0 MAPAMBANO DHIDI YA RUSHWA NA UDANGANYIFU

Mfuko umeendelea kutekeleza Mkakati wa kupambana na rushwa. Katika kipindi husika Mfuko ulifanya jumla ya chunguzi 538 na kuchukua hatua stahiki kwa waliobainika kujihusisha na vitendo vya udanganyifu kulingana na miongozo ya Mfuko ambapo; Mfuko uliokoa (Recovered) jumla ya shilingi bilioni 30.5. kutokana na chunguzi zilizofanyika. Mfuko ulisitisha mikataba kwa jumla ya vituo vya huduma 33 kutokana na vitendo vya udanganyifu. Mfuko ulisitisha matumizi ya vitambulisho 13,984 vya wanufaika waliogundulika kufanya vitendo vya udanganyifu. Mfuko umewachukulia hatua Watumishi 11 waliohusika na udanganyifu.

7.0 MAFANIKIO YA MRADI WA TEHAMA

Utekelezaji wa mradi wa TEHAMA kwa kutumia wataalam wa ndani ambapo kwa mwaka 2024/25 Mfuko umeokoa kiasi cha Shilingi bilioni 3.5, mradi huu umepunguza matumizi ya karatasi (Claim forms) kwa 75% kutokana na kuchakata madai kupitia mifumo. Pia mradi umepunguza gharama za Kadi za wanachama kwa 80%. Hivi sasa wanachama wanatumia kadi za kielektroniki (e-card), mradi huo pia umeboresha huduma kwa wanachama kupitia huduma ya NHIF Jihudumie (NHIF Self-Service) ikiwemo Kuchakata madai kidigiti umeongeza ufanisi na kupunguza vitendo vya udanganyifu.

8.0 UWEKEZAJI KWA WATUMISHI WA MFUKO

Kwa upande wa rasilimali watu, watumishi wote walihudhuria mafunzo ya muda mfupi ya kuongeza ujuzi kulingana na kada zao pamoja na mahitaji ya Mfuko. Zoezi hili limeongeza tija katika utoaji wa huduma.

9.0 MAPAMBANO DHIDI YA UKIMWI NA MAGONJWA SUGU

Mfuko umeendelea kutekeleza Sera ya kupambana UKIMWI pamoja na magonjwa yasiyoambukiza (NCDs) kwa kuwawezesha watumishi kushiriki mazoezi, michezo, mashindano ya kitaifa na mbio za marathon, pamoja na mafunzo ya afya ya akili.

10.0 UTEKELEZAJI WA BIMA YA AFYA KWA WOTE

Kupitishwa kwa Sheria ya Bima ya Afya, Sheria Na 161 ya mwaka 2023 pamoja na kanuni zake za mwaka 2024, kumeweza Mfuko kuanza utekelezaji wa Bima ya Afya kwa wote. Mambo muhimu yaliyofanyika kwa kushirikiana na Wizara ya Afya ni;- Ushirikishwaji wa wadau wakati wa maandalizi ya kitita cha bima ya afya kwa wote. Kwa upande wa NHIF; Mfuko umesimika mifumo ya TEHAMA kwa ajili ya usajili, uchakataji madai na kuunganisha mifumo yake (interoperability) na Mifumo Serikali pamoja na Mifumo ya Taasisi nyingine za kimkakati ili kuanza usajili kwa makundi mbalimbali. Makundi hayo ni;- wakulima, wafugaji, wachimbaji wadogo wa madini, wavuvi, wafanyabiashara wadogo na wafanya biashara wakati.

Hadi sasa, Mfuko umeingia makubaliano na Vyama vya Ushirika (kupitia TCDC) ili kutumia mtandao wa ushirika kusajili wanachama wengi zaidi nchini. Pia, NHIF imeingia makubaliano na Mawakala wa Bima Nchini, baadhi ya mabenki na makampuni ya simu kwa lengo la kuwafikia wafanyabiashara wadogo wadogo katika sekta isiyo rasmi. Kazi zinazoendelea ni Tathmini ya Mfuko kubaini uhimilivu wake kwenye utekelezaji wa Bima ya Afya kwa wote; kuendelea kujenga uwezo kwa Watumishi na watoa huduma, maandalizi ya zoezi la uhamasishaji kwa kushirikiana na Wizara, na wasimamizi wa Bima ya Afya. Tathmini ya Mfuko utakao gharamia kaya zisizo na uwezo pamoja na Mfuko wa magojwa sugu na yasiyo ambukiza.

UONGOZI WA JUU

Dkt. Irene C. Isaka
Mkurugenzi Mkuu wa NHIF

Bw. Celestine Muganga
Mkurugenzi wa Mipango na Uwekezaji

Dkt. Alphonce Chandika
Mkurugenzi wa Huduma za Uanachama

Bi. Grace Temba
Mkurugenzi wa Fedha

Bw. Lembris Laanyuni
Mkurugenzi wa Rasilimali Watu na Utawala

Dkt. David Mwenesano
Mkurugenzi wa Tiba na Ushauri wa Kitaalam

Bi. Leonia Masmin
Meneja Kitengo cha Ununuzi na Ugavi

Dkt. Rose Ntundu
Meneja Kitengo cha Udhibiti wa Vitendo vya Udanganyifu

Bw. Alexander Sanga
Mkurugenzi wa TEHAMA

Bw. Neligwa Maira
Meneja Kitengo cha Ukaguzi wa Ndani

Bw. Matamus A. Fungo
Meneja wa Huduma wa Sheria

Bw. James T. Mlowe
Meneja wa Kitengo cha Uhusiano

Bw. Abubakar Ndwata
Meneja wa Tathmini, Takwimu na Hadhari

NHIF INA WATUMISHI WENYE WELEDI

Bw. Lembris Laanyuni
Mkurugenzi wa Rasilimali Watu na Utawala

- **Wako tayari kutekeleza Bima ya Afya kwa Wote**
- **Wawezeshwa kwa Mafunzo na Vitendea Kazi**

Moja ya Kurugenzi zilizopo Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya, ni kurugenzi ya Utawala na Rasilimaliwatu ambayo jukumu lake kubwa ni kuhakikisha Watumishi wanafanya kazi kwa kuzingatia maadili ya utumishi wa umma, taratibu na miongozo mbalimbali iliyowekwa na Serikali.

Kwa sasa Mfuko una jumla ya Watumishi 727 ambao takwimu za kielimu zinaonesha kuwa Mfuko una nguvu kazi yenye sifa za kitaaluma za juu, ambapo Watumishi 566 sawa na 77.8% wana elimu ya kiwango cha Shahada ya Kwanza au zaidi (Shahada, Shahada ya Uzamili, Stashahada ya Uzamili na Shahada ya Uzamivu - PhD).

1.0 Viwango vya Elimu vya Watumishi



Idadi ya Watumishi wenye Shahada na Shahada ya Uzamili ni 553, sawa na 76.0% ya Watumishi wote, jambo linalodhihirisha uwezo mkubwa wa kitaaluma katika kutekeleza majukumu ya kiutendaji na kitaaluma ndani ya Mfuko.

Katika kipindi hiki cha miaka minne ya Serikali ya Awamu ya Sita, Mfuko umefanikiwa kutoa mafunzo kwa Watumishi wote wa Mfuko katika nyanja mbalimbali. Watumishi walipata mafunzo ya muda mrefu, muda mfupi pamoja na masaa ya kitaaluma (CPD hours)

2.0 Watumishi Walioshiriki Mafunzo ya Muda Mfupi

	CPD HOURS	
	Washiriki	**Idadi**
1	Wahasibu (Accountants & Accounts Officers)	64
2	Wakaguzi wa Ndani (Intemal Auditors)	8
3	Maofisa Ununuzi (Procurement Officers)	13
4	Maofisa Tabibu (Medical Officers)	5
5	Wafamasia (Pharmacists)	13
6	Wanachama wa ISACA	4
7	Mhandisi	1
8	Maofisa wa Kupambana na Vitendo vya Udanganyifu (Anti-Fraud Officers)	14
	Jumla	122

Mfuko katika kuimarisha Utendaji kazi wa watumishi umekuwa ukiwajengea uwezo kwa kuandaa mafunzo ya muda mrefu na mfupi na ambapo katika mwaka wa fedha 2024/2025 watumishi 27 walipatiwa ruhusa ya kuhudhuria masomo ya muda mrefu na watatu (3) mafunzo ya muda mfupi.

3.0 Idadi ya Watumishi walioshiriki mafunzo ya muda mfupi

Group Training	
Mafunzo kwa Maofisa Uanachama kuhusu masoko, usajili kidijiti, kupambana na vitendo vya udanganyifu, sheria ya ununuzi na kanuni zake.	196
Mafunzo kwa Maofisa Udhibiti Bora na Madai kuhusu kupambana na vitendo vya udanganyifu matumizi ya mfumo katika uchakataji wa madai, sheria ya ununuzi na kanuni zake.	238
Mafunzo kwa Wahasibu kuhusu masoko, usajili kidijiti, kupambana na vitendo vya udanganyifu, sheria ya ununuzi na kanuni zake na mafunzo ya IFRS17.	64
Mafunzo ya madereva kuhusu usalama barabarani na ufuatiliaji wa matumizi ya magari (car tracking)	59
Mafunzo kuhusu masoko, usajili kidijiti, kupambana na vitendo vya udanganyifu, sheria ya ununuzi na kanuni zake. Mafunzo hayo yalifanyika kwa Kurugenzi na Vitengo vya DHRA, ARRU, LSM, PRU, PMU & AFU.	64
Mafunzo kwa viongozi ya kujengewa uwezo (Capacity Building for the Management Team)	49
Mafunzo ya Usalam awa Mahala pa kazi (OSHA), kuhusu kudhibiti majanga yaliyofanyika kwa Maofisa Waandamizi.	29
Mafunzo ya Ufuatiliaji na Tathmini (Monitoring and Evaluation)	17
Mafunzo kuhusu Mfumo mpya wa ununuzi (New National e-Procurement System of Tanzania (NEST)	19
Mafunzo kwa Maofisa Udhibiti Ubora na Uchakataji wa Madai kuhusu kitita kipya cha mafao cha mwaka 2023 na maandalizi ya utekelezaji wake.	249
Maofisa wa Kupambana na Kudhibiti Vitendo vya Udanganyifu walipewa mafunzo kuhusu njia za kutambua viashiria na kupambana na vitendo vya udanganyifu.	22
Jumla	1006
Mafunzo ya Kitaaluma na Masaa ya Kitaaluma (CPD Hours)	
Wahasibu (Accountants & Accounts Officers)	64
Wakaguzi wa Ndani (Internal Auditors)	8
Maofisa Ununuzi (Procurement Officers)	13
Maofisa Tabibu (Medical Officers)	5
Wafamasia (Pharmacists)	13
Wanachama wa ISACA	4
Wahandisi	1
Maofisa wa Kupambana na Vitendo vya Udanganyifu (Anti-Fraud Officers)	14
Jumla	**122**

Aidha, watumishi 716 walishiriki katika mafunzo ya pamoja (in-group training), watumishi 41 walihudhuria mafunzo ya muda mfupi, na watumishi 117 walishiriki katika makongamano ya kitaaluma na kupata CPD Hours (Continuous Professional Development).

4.0 Uzingatiaji wa Miongozo Mbalimbali ya Kiutumishi

Mfuko ni miongoni mwa Waajiri Bora nchini, na katika kusimamia masuala ya kiutumishi huzingatia Sheria, Taratibu, na Kanuni mbalimbali za Usimamizi wa Utumishi wa Umma zikiwemo Sheria ya Utumishi wa Umma, na Kanuni zake, Kanuni za Watumishi wa NHIF, 2023 na Miongozo mbalimbali ili kuhakikisha wanachama na wananchi wanapata huduma zenye staha kwa kuhudumiwa na watumishi wanaozingatia taratibu zilizopo.

Aidha, Mfuko huzingatia matakwa ya Sheria Na. 6 ya mwaka 2004 (Employment and Labour Relations Act, 2004) kwa kuhakikisha ushirikishwaji wa wafanyakazi katika maamuzi kupitia vyombo mbalimbali kama Chama cha Wafanyakazi (TUGHE), Baraza la Wafanyakazi, Vikao vya Maafisa Waandamizi na Kamati ya Maslahi ya Watumishi (Welfare Committee Meetings).

Watumishi wa NHIF wakishiriki Mafunzo ya Utawala Bora na Uadilifu

5.0 Usimamiaji wa uadilifu

Katika kutekeleza Mkakati wa Kitaifa wa Kupambana na Rushwa, Mfuko unao miongozo na sera mbalimbali zinawezesha utekelezaji wa suala hili ikiwemo mwongozo wa kupambana na vitendo vya udanganyifu, Sera ya utoaji taarifa kwa siri (Whistleblowers policy), matumizi ya teknolojia katika kubaini vitendo vya udanganyifu na kuundwa kwa Kamati ya Maadili ambayo inakutana mara kwa mara kwa lengo la kushughulikia mashauri ya Watumishi yanayohusiana na vitendo vya rushwa au udanganyifu.

Watumishi wa NHIF walifanikiwa kupanda Mlima Kilimanjaro na kupeperusha bendera ya Bima ya Afya kwa Wote

6.0 Kupambana na Magonjwa yasiyoambukiza

Mfuko umeendelea na kupambana na Magonjwa yasiyoambukizwa kwa kupima watumishi wake kwa hiari na kuwapa mafunzo ya kuepukana na magonjwa hayo kwa kuishi mtindo bora wa maisha. Katika Mwaka wa fedha 2024/2025 jumla ya Watumishi 583 walipima afya zao ambapo watumishi 270 walikutwa na viashiria vya magonjwa yasiyoambukizwa sawa na asilimia 46.

Ili kupambana na hali hii, Mfuko unazo program mbalimbali za kujikinga na magonjwa yasiyoambukizwa ikiwemo kuanzisha program maalum kwa Watumishi kufanya mazoezi baada ya muda wa kazi. Aidha Mfuko umekuwa ukigharamia Watumishi kushiriki katika marathon mbalimbali na kupanda Mlima Kilimanjaro hatua inayosaidia Watumishi kujua hali ya afya zao na kuishi mtindo bora wa maisha.

7.0 Upatikanaji wa Vitendea Kazi kwa Watumishi (ikiwemo Vishikwambi)

Katika kuhakikisha kuwa watumishi wanatimiza majukumu yao kwa ufanisi, Mfuko uliwapatia watumishi vitendea kazi muhimu vinavyozingatia usalama wao mahala pa kazi ili kuepukana na madhara ya kiafya yanayoweza kusababishwa na vitendea kazi visivyokidhi mahitaji.

8.0 NHIF yajenga Ofisi zake Lindi na Pwani

Katika kupunguza gharama za uendeshaji, Mfuko umefanikiwa kujenga Ofisi zake katika Mikoa ya Lindi na Pwani ambazo zitapunguza gharama za kulipa pango ambazo zitasaidia kuimarisha uhai wa Mfuko na kuimarisha hali ya kifedha ya Mfuko.

Haya yote yanalenga kuongeza ufanisi wa utekelezaji wa majukumu ya kila siku ya watumishi hususan katika kipindi hiki ambacho Mfuko unatarajia kuhudumia wananchi wengi zaidi kupitia utekelezaji wa Bima ya Afya kwa Wote.

Watumishi wa NHIF wakishiriki Michezo

MAMENEJA KATIKA KURUGENZI NA VITENGO MBALIMBALI MAKAO MAKUU

Bi. Janeth A. Kibambo
Meneja wa Mipango

Bi. Yusta E. Mandara
Meneja wa Rasilimali Watu

Bi. Anjela A. Mziray
Meneja wa Masoko na Huduma kwa Wateja

Bw. Suleiman S.Madega
Meneja wa Utawala

Bi. Salome S. Manyama
Meneja wa Uanachama na Matekelezo

Bw. David T. Sikaponda
Meneja wa Uwekezaji

Bw. Amour R. Hamad
Meneja wa Utengenezaji wa Mifumo

Dkt. Edith S. Mlay
Kaimu Meneja wa Uchakataji Madai

Bw. Donald F. Malunda
Kaimu Meneja wa Udhibiti na Usaidizi wa Huduma za Mifumo ya TEHAMA

Dkt. Peter D. Nyakubega
Meneja wa Uthibiti Ubora na Uhakiki wa Madai

Bw. Emmanuel Kyomo
Meneja wa Miundombinu

Bw. Celestine Muganga
Mkurugenzi wa Mipango na Uwekezaji

NHIF YACHANGIA UBORESHAJI HUDUMA ZA MATIBABU KWA KUTOA MIKOPO YA VIFAA TIBA

- **Mamia ya Vituo vyanufaika**
- **Huduma za kibingwa zawezeshwa**

Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya (NHIF), umekuwa mstari wa mbele katika kushiriki uboreshaji wa huduma za matibabu nchini. Katika hili Mfuko unao mpango wa mikopo nafuu ya Miundombinu na ukarabati wa majengo pamoja na vifaa tiba na dawa.

Mikopo hii imekuwa ikitolewa kwa Vituo vyote vilivyosajiliwa na Mfuko na marejesho yake yamekuwa yakirejeshwa kwa kukatwa kiasi kidogo kupitia madai wanayowasilisha watoa huduma husika.

Maelezo	Idadi ya Vituo	Kiasi (Bilioni TZS)
Mikopo ya Vifaa Tiba	293	32.6
Dawa na Vitendanishi	52	3.9
Mikopo ya ukarabati wa Majengo	109	12.048

Katika kipindi cha miaka minne ya Serikali ya Awamu ya Sita, Mpango huu wa Mfuko wa kutoa mikopo kwa watoa huduma wake umesaidia na kuwezesha upatakanaji wa vifaa tiba na dawa katika vituo mbalimbali vya kutolea huduma za afya.

Mikopo hii ya vifaa tiba imewezesha watoa huduma kupata vifaa tiba kwa ajili ya maeneo mbalimbali ya huduma, ikiwa ni pamoja na vifaa tiba kwa ajili ya huduma za Radiolojia (X ray Machine, Ultrasound machine), vifaa vya maabara (Haematology, Immunoassay, chemistry analyser), vifaa vya upasuaji (Operating table, Anaesthetic machine), vifaa kwa ajili ya huduma za kinywa na meno, huduma za moyo (ECG machine).

Aidha umewezesha uanzishwaji wa huduma ya uzazi saidizi (IN VITRO FERTILIZATION – IVF) na vifaa tiba vingine mbalimbali ambavyo kwa pamoja vimechangia vituo kuboresha utoaji wa huduma za afya katika maeneo yao.

Mpaka kufikia mnamo Juni, 2025, Mfuko umeweza kutoa jumla ya mikopo yenye thamani ya Shilingi Bilioni 12.9 kwa ajili ya ununuzi wa vifaa tiba.

Mafanikio mengine ni ujenzi na ukarabati wa majengo kwa watoa huduma mbalimbali

kwa ajili ya kuboresha miundo mbinu ya kutolea huduma. Maeneo ya ujenzi na ukarabati yaliyonufaika na mikopo hii ni pamoja na majengo ya OPDs, Maternity wards, Pharmacy, Labarotory, Radiology & theatres.

USAJILI WA VITUO			
1	Serikali	7,385	82%
2.	Binafsi	1,050	12%
3.	Dini	626	7%

Mfuko vilevile kupitia mikopo hii umewezesha ujenzi majengo kwa ajili ya huduma ya kuchuja damu (Dialysis services) na usimikaji wa mifumo ya TEHEMA (HMIS) katika hospitali mbalimbali. Jumla ya mikopo yenye thamani ya Shilingi Bilioni 2.78 imetolewa kwa Vituo 38 kwa ajili ya ujenzi na ukarabati wa miundo mbinu ya kutolea huduma za afya.

WASIMAMIZI WA OFISI NDOGO ZA MFUKO

Bi. Damali I. Nchimbi
Msimamizi wa Ofisi ya
Kigamboni

Bi. Jane G. Mukoba
Msimamizi wa Ofisi ya
Ubungo

Bi. Ridhia W. Makono
Msimamizi wa Ofisi ya
Masasi

Bi. Msua S. Mpinga
Msimamizi wa Ofisi ya
Tunduma

Bw. Haji Z. Mpeta
Msimamizi wa Ofisi ya
Nzega

Bi. Frida C. Senga
Msimamizi wa Ofisi ya
Kahama

Bi. Sarah Adebe
Msimamizi wa Ofisi ya
Tegeta

Bw. Bakary S. Hamdun
Msimamizi wa Ofisi ya
Katoro

Bw. Stephen J. Simwiche
Msimamizi wa Ofisi ya
Mbinga

Bi. Salma R. Marijani
Msimamizi wa Ofisi ya
Ifakara

Bw. Desderius T. Buhiye
Msimamizi wa Ofisi ya
Karagwe

Bw. Meshack B. Songo
Msimamizi wa Ofisi ya
Gongolamboto

Bw. Charles V. Lengeju
Msimamizi wa Ofisi ya
Bukombe

MAFANIKIO YA AWAMU YA SITA

- **Yafanikiwa kuondoa nakisi**
- **Yapata hati safi kila mwaka**

Bi. Grace Temba
Mkurugenzi wa Fedha

Kurugenzi ya Fedha ndani ya Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya, una jukumu la kusimamia na kushauri masuala mbalimbali ya kifedha pamoja kuandaa taarifa za kifedha kwa kufuata miongozo ya kitaifa na kimataifa.

Katika kipindi cha miaka minne (4) cha Utawala wa Awamu ya Sita ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassani Mfuko umekuwa na mafanikio yafuatayo:

1.0 NHIF yapata tuzo

Katika kipindi cha miaka minne ya Awamu ya Sita, Mfuko umeendelea kuandaa taarifa zake za fedha kwa mujibu wa miongozo na kuuwezesha kupata tuzo ya uandaaji wa hesabu zenye ubora kwa miaka minne ya Uongozi wa Mheshimia Rais kutoka Bodi ya Wahasibu na Wakaguzi (NBAA).

2.0 Kutoa ushauri wa kifedha katika uwekezaji wa muda mfupi na mrefu

Kurugenzi ya Fedha imekuwa ikisimamia na kutoa ushauri mbalimbali wa kifedha katika uwekezaji wa muda mfupi na mrefu katika mabenki ya kibishara na Benki Kuu ili kuhakikisha Mfuko unakuwa na ukwasi wakati wote na kuhakikisha madeni ambayo yanapaswa kulipwa yanalipwa kwa wakati. Hatua hii pamoja na hatua nyingine zilizochukuliwa zimeusaidia Mfuko kuondokana na nakisi (Deficit) iliyokuwepo kwa miaka kadhaa na kuanza kupata ziada (Surplus) katika mwaka wa fedha 2023/24 ambapo Mfuko ulipata ziada ya TZS 49.81 billioni .

3.0 Kuandaa na kuwasilisha Hesabu za Mfuko kwa wakati kulingana na Sheria na kuuwezesha Mfuko kupata hati safi ya Ukaguzi kutoka kwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali(CAG)

Mfuko kwa kipindi cha miaka minne umeandaa na kuwasilisha kwa wakati Hesabu kwa mujibu wa sheria kwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG).Hii inaonesha dhamira ya dhati ya Mfuko kuhakikisha unasimamia miongozo sheria na kanuni zinazotolewa na mamlaka mbalimbali za Serikali.

Mfuko tangu kuanzishwa kwake umekuwa ukipata hati safi ya ukaguzi wa Hesabu za Serikali.Hii inaonesha namna ambavyo Mfuko unahakikisha unafanya kazi kwa kuzingatia miongozo sheria na kanuni mbalimbali za kifedha za kimataifa na za kitaifa na hivyo kuendelea kupata hati safi katika ukaguzi.

4.0 Kuzingatia kikamilifu na kuendana na mabadiliko mbalimbali ya miongozo ya kifedha ya kimataifa (International Financial Reporting Standards-IFRS)

Mfuko kwa kipindi cha kuanzia mwaka 2023/2024 ulifanikiwa kuanza kutekeleza muongozo mpya wa kimataifa (IFRS 17) unaohusiana na shughuli za kibima katika uandaaji wa Hesabu zake. Muongozo huu ni muhimu kwa Mfuko katika kusaidia na kutambua kwa wakati vifurushi (Products) vya Mfuko vinavyousababishia Mfuko nakisi na kuchukua hatua kwa wakati.

5.0 Mafunzo ya IFRS 17

Ili kuwezesha ufanisi katika utekelezaji wa Mwongozo huo, Mfuko umetoa mafunzo kwa Wahasibu wote ili kuwajengea uwezo wa kuandaa hesabu kwa kuzingatia mwongozo wa kimataifa wa shughuli za kibima.

6.0 Kufuata sheria na kanuni zilizowekwa na mamlaka mbalimbali za Serikali.

Mfuko kupitia Kurugenzi ya Fedha umekuwa ukihakikisha unazingatia sheria na kanuni mbalimbali zilizowekwa ikiwemo,kulipa malipo yote ya kisheria ikiwemo kodi na tozo mbalimbali za kisheria pamoja na miongozo iliwekwa na Wizara ya Fedha katika usimamizi wa Fedha za Mfuko.

Bw. Alexander Sanga
Mkurugenzi wa TEHAMA

MABADILIKO MAKUBWA KWENYE MATUMIZI YA TEHAMA

- **Wanachama sasa kujihudumia walipo**
- **Yaweka mfumo wa mrejesho wa huduma**

Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya (NHIF), umewekeza kwa kiwango kikubwa katika matumizi ya TEHAMA ambayo yamelenga kurahisisha upatikanaji wa huduma kwa wanachama wake.

Uwekezaji huu umefanyika katika kipindi cha miaka minne ya Mhe. Rais Samia Suluhu Hassan ambapo kwa sasa zaidi ya asilimia 90 za shughuli za Mfuko zinafanywa kwa usaidizi wa Mifumo.

Maboresho haya yameongeza ufanisi, kupunguza gharama na kurahisisha upatikanaji wa huduma kwa wanachama, watoa huduma, waajiri na wananchi wanaotaka kujiunga. Mafanikio haya yametokana na maboresho katika maeneo yafuatayo;-

1.0 Usanifu wa Miundombinu

Usanifu ulilenga kubadili mifumo tegemezi na kuweka mifumo ya kisasa zaidi yenye teknolojia huria kwenye eneo la usimamizi na uhifadhi data.

Hatua hii imesaidia kuboresha usalama na kupunguza gharama za leseni hivyo Mfuko umeweza kuokoa kiasi cha Shilingi Bilioni 3.07 ambazo zingetumika kugharamia malipo ya leseni za program za kibiashara ambazo zilitumika awali.

2.0 Mfumo wa Usajili wa Wanachama (Self Services)

Mfuko umeanzisha Mfumo wa kidijiti unaowawezesha wanachama kujihudumia wenyewe (Self Service) kwa kujisajili pamoja na wategemezi wao, kufanya malipo, kupata kadi ya matibabu ya kielektroniki pamoja na kutoa mrejesho wa huduma, kufuatilia majibu ya changamoto walizowasilisha.



Wanachama sasa wanaweza kujisajili kwa urahisi, kuongeza au kuondoa wategemezi, kupata kadi ya kielektroniki (eCard) na kulipia michango bila ya kulazimika kutembelea ofisi za Mfuko. Mfumo huu umeboreshwa kwa kuwekewa kikokotoo cha malipo (calculator) kinachozingatia umri, idadi ya wanufaika na kifurushi kilichochaguliwa, hivyo kurahisisha mchakato wa kujua kiwango sahihi cha mchango. Aidha, uhakiki wa nyaraka hufanyika moja kwa moja kupitia mamlaka husika kama RITA na NIDA bila kuhitaji kuambatisha nakala za nyaraka. Hatua hii imepunguza mzigo kwa watumishi wa Mfuko na kurahisisha upatikanaji wa huduma kwa wanachama, popote walipo na kwa wakati wowote.

3.0 Usajili wa wanachama kupitia Waajiri

i Mfuko umeboresha mifumo yake ili kuruhusu waajiri kuunda akaunti, kusajili wanachama, kusaini mikataba kidigitali na kuendesha huduma mbalimbali mtandaoni.

ii. Usajili wa wanachama kupitia Mawakala
Mawakala wamewezeshwa kupitia Mfumo kuunda akaunti, kusajili wanachama, kusaini mikataba kidigitali na kuendesha huduma mbalimbali mtandaoni. Aidha, wafanyakazi wa Mfuko pia wamesajiliwa kama mawakala wa usajili, jambo lililoongeza kasi ya usajili na kuwafikia wananchi kiurahisi zaidi.

4.0 Usajili wa Vifurushi

Mfumo wa usajili wa vifurushi umeanzishwa ili kuruhusu wanachama kuchagua na kujisajili kwenye vifurushi vya matibabu kulingana na mahitaji yao. Mfumo huu unatoa urahisi kwa wanachama binafsi na vikundi kujiunga na vifurushi kwa njia ya kidigitali bila kupitia taratibu ngumu za karatasi. Hatua hii imeongeza uwazi, kupunguza muda wa kushughulikia usajili na kutoa chaguo pana kwa wanachama katika kupata huduma za afya.

5.0 Usimamizi wa Vituo (Facilities)

Moduli hii imetekelezwa ili kutoa jukwaa la kidigitali kwa vituo vya afya kuunda akaunti na kusimamia mchakato mzima wa uthibitisho, ikiwemo maombi, usimamizi wa ukaguzi, vikao vya kamati ya uthibitisho na maazimio yake. Pia moduli hii inawezesha vituo kuteua na kusajili watia saini, kusaini mikataba kidigitali na kufanya mabadiliko ya taarifa za kituo kwa urahisi zaidi na uharaka.

6.0 Usimamizi wa Mikataba Kidigiti

Kupitia moduli hii, mikataba sasa inasainiwa kidigitali na wadau wote wakiwemo waajiri, vituo, mawakala na watumishi wa ndani. Utekelezaji wake umeleta manufaa makubwa, kwani mikataba inasainiwa kwa wakati bila ucheleweshaji huku gharama za uchapishaji, usambazaji na utunzaji wa mikataba ya karatasi zikiepukwa.

7.0 Kuboresha Mzunguko wa Matibabu (Treatment cycle)

Maboresho makubwa katika mfumo Service portal yamefanyika ili kushughulikia mzunguko mzima wa matibabu ya mwanachama (treatment cycle) kuanzia uhakiki wa mwanachama, usimamizi wa huduma katika eneo la tiba, kuidhinisha huduma, kulazwa na usimamizi wa matibabu. Pia mfumo unaruhusu ujumuishaji na mifumo ya watoa huduma. Maboresho haya yanatarajiwa kuondoa matumizi ya Fomu 2A&B kwa kuwa watendaji wote wataingia kwenye mfumo na kufanya miamala kidigitali, jambo litakalopunguza gharama za uchapishaji na usimamizi wa fomu za karatasi.

8.0 Usimamizi wa Michango (Contribution Management)

Upande wa usimamizi wa michango imeboreshwa zaidi na sasa inawawezesha wanachama na waajiri kupata namba za kudumu za malipo. Aidha, imeunganishwa na mifumo ya ERMS unaosimamiwa na Mamlaka ya Serikali mtandao (eGA) ili kuwezesha urejeshaji wa michango inayolipwa kwa mwaka mzima na kuboresha uchakataji wa taarifa kwa kuzingatia viwango vya kimataifa vya taarifa za kifedha.

9.0 Usimamizi wa Mahusiano na Wateja (CRM)

Kwa sasa wanachama wanaweza kutoa mrejesho, kuuliza maswali na kutoa tathmini kuhusu huduma za Mfuko. Mfumo unarahisisha uwasilishaji na ufuatiliaji wa mrejesho huku watumishi wakiwa na uwezo wa kushughulikia moja kwa moja malalamiko na kuyapatia suluhisho. Pia, kuna dashboard inayoonyesha mrejesho uliopokelewa, ulioshughulikiwa na ulio wazi, hatua ambayo imeongeza uwazi kwa menejimenti. Zaidi ya hapo, moduli hii imeunganishwa na mfumo wa serikali wa eMrejesho, kuruhusu maoni na malalamiko yaliyowasilishwa kupitia eMrejesho kushughulikiwa moja kwa moja ndani ya mfumo wa Mfuko bila kuhama mifumo.

10.0 Usimamizi wa Watumiaji (User Management)

Moduli hii imetengenezwa kwa ajili ya kusimamia watumiaji wote wa ndani na wa nje wa mfumo. Inajumuisha kugawa majukumu kwa watumiaji, kusitisha akaunti inapohitajika na kudhibiti usalama wa akaunti kwa ufanisi.

11.0 Usimamizi wa Kazi (Task management)

Kupitia moduli hii, wasimamizi wanaweza kuunda kazi na kuzigawa kwa wasaidizi wao, ambapo wasaidizi hufanya kazi walizopewa na kuripoti matokeo. Mfumo pia unamwezesha Mkurugenzi Mkuu kugawa na kufuatilia majukumu yote

yaliyotolewa kwa wakurugenzi na mameneja kwa uwazi na urahisi.

12.0 Uunganishaji na mifumo ya taasisi mbalimbali

Ikiwa sehemu ya utekelezaji wa maelekezo ya Serikali ya mifumo kusomana, uunganishaji wa mifumo na wadau pamoja na taasisi mbalimbali za serikali pia umetekelezwa ambapo taasisi 17 kati ya 26 waliotambulika tayari wameunganishwa kupitia GovESB. Mfuko umewezesha mifumo yake kusomana na mifumo ya taasisi mbalimbali za kiserikali, baadhi ya taasisi ni kama zifuatazo:

Mamlaka ya vitambulishi vya taifa (NIDA) - kupitia kusomana kwa mfumo wa huu na mfumo wa mamlaka ya vitambulisho vya taifa, mwanachama wa Mfuko wa taifa wa bima ya afya anaweza kujisajili na kusajili wategemezi kwa kuingiza namba za utambulisho wa NIDA na kukamilisha usajili bila kufika ofisi za NHIF wala kuambatanisha viambatanisho vyovyote. Pia mwanachama anaweza kutumia namba yake ya NIDA kupata huduma katika vituo vya afya baada ya kujisajiri Wakala wa usajili wa vizazi na Vifo Tanzania Bara (RITA) na Mamlaka ya usajili wa vizazi na Vifo Zanzibar (ZCSRA) - Kupitia kusomana kwa mfumo huu na mfumo wa wakala wa usajili wa vizazi na vifo, Mfuko umerahisisha wanachama kuongeza au kuondoa wategemezi kama watoto bila kufika katika oflsi za NHIF wala kuambatanisha viambatanisho vyovyote.

Mfuko pia umehakikisha mfumo huu unasomana na taasisi nyingine mbalimbali ikiwamo taasisi za elimu ya msingi na sekondari (NECTA), taasisi ya vyuo vya elimu ya kati (NACTVET), taasisi ya elimu ya juu (TCU) ili kurahisisha usajiri wa wanafunzi katika ngazi zote za elimu.

Pia Mfuko umehakikisha mfumo unasomana na taasisi nyingine kama PSSSF na NSSF, taasisi ya usajili wa biashara (BRELA), Utumishi, Wizara ya fedha (GEPG), wizara ya afya upande wa usajiri wa vituo vya afya, baraza la madaktari nk.
Kupitia kuunganisha mfumo huu na taasisi mbalimbali, Mfuko umetekeleza na unaendelea kutekeleza azma ya serikali ya awamu ya sita kuhakikisha mifumo inasomana na kuweza kurahisisha utoaji wa huduma kwa wananchi na kupunguza gharama za uendeshaji kwa Mfuko na serikali kwa ujumla.

13.0 Usalama wa Mfumo

Katika maendeleo ya maboresho ya mifumo ya Mfuko, jitihada maalum za usalama wa kimtandao zilifanyika ili kuhakikisha mifumo inazinduliwa kwa hatari ndogo iwezekanavyo. Ukaguzi wa usalama ulifanyika Pia, hatua za ziada kama uthibitisho wa hatua mbili (MFA) katika mifumo, usimbaji data, urekebishaji wa maktaba zilizo na udhaifu, na utekelezaji wa mbinu bora za kudhibiti taarifa zimeanzishwa. Aidha, eGA imetoa barua ya uthibitisho wa usalama kwa Mfuko. Hii imedhihirisha mafanikio makubwa kwa Mfuko kuwa na uweza wa kuunda mifumo inayokidhi viwango vya kiusalama vinavyokubalika.

14.0 Tuzo ya Tehama

Mfuko ulipata heshima ya kushiriki kwenye TEHAMA Awards 2025, jukwaa la kitaifa linalotambua ubora na ubunifu katika sekta ya TEHAMA. Tarehe 21 Februari 2025, mradi wa kubuni upya mifumo uliwasilishwa kwenye kipengele cha *Best Use of ICT in Healthcare* kupitia mifumo mitatu: *Self-Service, Automated Claims Processing,* na *Online Claims Submission.* Ushiriki huu ulionyesha jinsi mifumo hiyo ilivyopunguza muda wa kushughulikia madai na kuboresha upatikanaji wa huduma kwa wanachama na watoa huduma. Matokeo yake, Mfuko ulitajwa kama mshindi wa pili kitaifa, nyuma ya mfumo wa m-mama, na hivyo kuthibitisha mchango mkubwa wa mifumo hii katika mageuzi ya afya kidigitali nchini.

NATIONAL HEALTH INSURANCE FUND
NHIF
Dedicated to providing quality health Care
ISO 9001:2015 CERTIFIED
Jiunge na NHIF wewe na familia yako kwa Uhakika wa Matibabu

Dkt. David Mwenesano
Mkurugenzi wa Tiba na Ushauri wa Kitaalam

NHIF YAPUNGUZA MUDA WA KULIPA MADAI

- **Wanachama kutambuliwa kidijitali**

Ili kuhakikisha wanachama wa Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya wanapata huduma bora, inayo Kurugenzi inayoratibu masuala yote ya huduma za matibabu ambayo husimamia upatikanaji na ubora wa huduma za matibabu kwa wanufaika.

Katika kipindi hiki cha Miaka minne ya Mhe. Rais Samia Suluhu Hassan, imekuwa na mafanikio mbalimbali ambayo ni pamoja na;-

1.0 Usajili wa Vituo

Mfuko umeweza kuongeza idadi ya vituo kutoka vituo 8,482 mwezi Juni 2021 hadi vituo 10,088 mwezi Juni 2025

USAJILI WA VITUO			
1	Serikali	7,385	82%
2.	Binafsi	1,050	12%
3.	Dini	626	7%

2.0 Uhakiki wa Madai (Claims Verification)

Mfuko umeweza kuboresha utaratibu wa kuhakiki madai kwa kuimarisha matumizi ya Tehama kwenye eneo la utoaji huduma kwa kuweka mfumo wa utambuzi wa wanuifaka kwa njia ya vidole (Finger printing) katika maeneo ya kutolea huduma, Kuimarisha uwasilishaji wa madai kutoka vituoni kwa njia ya mtandao (Online claims submission), na kuimarisha mfumo wa uchakataji wa madai kwa kutumia akili unde (Automation of claims processing).

Kutokana na matumizi haya ya Mifumo, Mfuko umeweza kupunguza madai yanayokataliwa (Rejection rate) kutoka asilimia 6.6 Mwezi Julai 2021 hadi asilimia 2.8 Mwezi Juni 2025.

3.0 Kupunguza muda wa ulipaji madai (Claims Aging rate)

Mfuko umeweza kupunguza muda wa ulipaji madai kutoka wastani wa siku 62 mwezi Juni 2021 hadi wastani wa siku 45.9 mwezi Juni 2025. Mafanikio haya yamesaidia kuondoa malalamiko kwa Watoa huduma hivyo kuongeza ufanisi katika upatikanaji wa huduma bora kwa wanachama.

4.0 Kuongezeka kwa huduma kwa njia ya vifurushi

Mfuko umeongeza wigo wa vifurushi kutoka vifurushi vitatu (3) Julai 2021 kufikia vifurushi

vitano (5) mwezi Juni 2025 ili kuwawezesha wananchi wengi zaidi kujiunga na Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya. Vifurushi hivyo ni pamoja na Tarangire, Ngorongoro, Mikumi, Serengeti na Tanzanite Afya. Huduma za vifurushi zimezingatia mahitaji halisi ya wananchi ambazo ni kama ifuatavyo katika jedwali lifuatalo;-

5.0 Mahusiano na Watoa Huduma

Mfuko umeendelea kufanya vikao na wadau mbalimbali ikiwa ni pamoja na waajiri, watunga sera na watoa huduma ili kuwa na uelewa wa pamoja kuhusu sera na huduma zinazotolewa na Mfuko.

Baadhi ya wadau ambao Mfuko umekutana nao mara kadhaa ni Wizara ya Afya,TAMISEMI, Chama cha watoa huduma binafsi APHTA,Taasisi chini ya Wizara ya Afya (MNH,ORCI,JKCI,MOI).

Taasisi za kidini zinazosimamia huduma za Afya kama CSSC,BAKWATA

MALIPO KWA VITUO		
1	Serikali	87%
2.	Dini	91%
3.	Binafsi	92%

6.0 Kulipa madai ya watoa huduma kwa wakati.

Mfuko una wajibu wa kuhakikisha madai ya watoa huduma yanalipwa kwa wakati kwa mujibu wa sheria.Hii inaonesha namna ambavyo Mfuko unathamini mchango wa watoa huduma za afya katika kuhakikisha wanachama wa Mfuko wanapata huduma na kuhakikisha unachangia mapato ya watoa huduma ili kuhakikisha uendelevu wa huduma kwa wanachama.

Bima ya Afya kwa Wote, **Jiunge Sasa**

WANANCHI KUJISAJILI WENYEWE KUPITIA MFUMO

- Yafungua Ofisi mpya 13
- Yaanzisha vifurushi nafuu kwa wananchi

Dkt. Alphonce Chandika
Mkurugenzi wa Huduma za Uanachama

Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya (NHIF), umeweka utaratibu unaomwezesha kila Mtanzania kujiunga na kunufaika na huduma za matibabu bila kikwazo cha fedha.

Utaratibu huu umewekwa kupitia vifurushi vyenye gharama nafuu ambavyo mwananchi anaweza kuchagua na kujiunga kulingana na mahitaji yake.

Mfuko unayo Kurugenzi ya Huduma za Wanawachama ambayo jukumu lake kubwa ni kusajili wanachama na kukusanya michango inayowezesha kugharamia huduma za matibabu.

Katika kipindi cha miaka Awamu ya Sita, Mfuko umefanikiwminne, Mfuko umefanikiwa kuongeza wanufaika 4,647,436 ambapo awali kulikuwa na wanufaika 691,774 mwaka 2001/2002 hadi kufikia wanufaika 5,339,210 mwezi Juni 2025 sawa na asilimia 8 ya Watanzania wote.

Katika kipindi cha Julai, 2021 hadi Juni 2025 ambacho ni kipindi cha ndani ya miaka minne ya Serikali ya Awamu ya Sita, Mfuko umefanikiwa kuwa na ongezeko la wanufaika wapya 517,977 sawa na asilimia 11. Mafanikio ya ongezeko hili linatokana na;-

1.0 Uzinduzi wa Vifurushi Vipya

Katika kuweka mazingira rahisi katika utekelezaji wa Bima ya Afya kwa Wote ili kuwawezesha wananchi wengi kuwa katika mfumo wa bima ya afya, Mfuko ulizindua Vifurushi vipya vitano vinavyojulikana kama Tarangire Afya, Ngorongoro Afya, Mikumi Afya, Serengeti Afya na Tanzanite Afya. Aidha, kwa upande wa Kundi la Watoto, wamewezeshwa kuwa na kifurushi kinachomwezesha mtoto mmoja mmoja kujiunga lakini pia Watoto kupitia shule wanazosoma.

Vifurushi hivi vimezingatia pato la mwananchi wa kawaida na vinampa fursa ya kuchagua kifurushi anachohitaji kulingana na mahitaji yake yakiwemo ya wategemezi au huduma za matibabu.

Ili kurahisisha usajili wa wanachama, Mfuko umekuja na Mfumo unaomwezesha mwananchi kujihudumia kokote aliko kupitia mfumo wa selfservice na kupata kadi ya mtandao (e-card) ambayo ataitumia kutambulika katika vituo vya matibabu ili kupata huduma. Mafanikio haya yamefikiwa ndani ya mud awa miaka minne ambapo awali wananchi walilazimika kufuata huduma za usajili Ofisi za Mfuko lakini kusubiria kadi kwa mud awa siku 21.

Aidha, Mfuko umeunganisha mifumo yake na NIDA na RITA na hivyo, mwanachama anaweza kutumia namba yake ya kitambulisho cha taifa katika

kutambulika kwenye vituo vya huduma.

Kwa upande wa Waajiri, wamewezeshwa kujihudumia wenyewe kupitia mfumo wa NHIF Employer Porter kwa kuandikisha wafanyakazi na kupata namba ya malipo ya michango bila kufika ofisi za NHIF.
Kuongeza kasi ya usajili wa wanachama kwa kushirikiana na wadau wa usajili na mpaka sasa Mfuko umeingia makubaliano na Wakala wa bima nchini na Vodacom Mpesa kwa ajili ya kuanza kusajili wanachama.

2.0 Huduma za ziada (Supplimentary Services)

Ili kuhakikisha huduma bora za matibabu zinapatikana kwa wanachama wake, Mfuko umeanzisha mpango wa huduma za ziada kwa waajiri wanaohitaji huduma hizo. Kupitia mpango huo Mwanachama anapewa fursa ya kuongeza huduma za ziada atakazozipenda kulingana na mahitaji yake kwa makubaliano maalum kati ya Mwajiri na NHIF.
Mpango huu umekuwa na manufaa makubwa kwa Taasisi mbalimbali kujiunga na huduma hizi ambazo zimeleta tija ya kihuduma za matibabu pale wanapozihitaji.

3.0 Elimu kwa Umma
3.1 Mikutano ya Wadau
Mfuko umekuwa ukikutana na wadau wake kupitia mikutano mbalimbali ikiwemo ya Kitaaluma, mikutano hii imewezesha Mfuko kukuza uelewa wa masuala ya bima ya afya kwa kuwasilisha mada katika mikutano na kutoa ufafanuzi wa maboresho ya huduma yaliyofanyika ndani ya Mfuko. Mikutano hiyo inajumuisha wanachama, watoa huduma, waajiri, vyama vya wafanyakazi, waandishi wa habari, Waheshimiwa Wabunge na viongozi wa madhehebu ya dini. Mikutano ya Kitaaluma ni pamoja na ALAT, Jumuiya ya Maridhiano, MELsaT, MAT, PPRA, ASSA na TRAMPA.

3.2 Elimu kupitia Maonesho
Mfuko umekuwa ukishiriki maonesho ya Kitaifa na ya mialiko kutoka kwa wadau mbalimbali. Maonesho hayo ni pamoja na Sabasaba, Nane Nane, Wiki ya Sheria, Maonesho ya Madini na Wiki ya Vijana. Maonesho haya yamekuwa chachu kwa wananchi kupata elimu, kujiunga, kupata mrejesho na utatuzi wa changamoto mbalimbali.

3.3 Usogezaji wa Huduma kwa wananchi

Katika kuhakikisha urahisi wa upatikanaji wa huduma kwa wananchi wengi zaidi, Mfuko umeendelea kufungua ofisi zake karibu zaidi na maeneo yenye wananchi wengi zaidi. Ofisi zilizofunguliwa ni pamoja na Kigamboni, Gongolamboto na Ubungo, Tegeta, Mbinga, Kahama, Masasi, Ifakara, Katoro, Bukombe, Karagwe, Tunduma na Nzega ambazo zimefanya idadi ya ofisi za Mfuko kuwa 41.

3.4 Kuimarisha mifumo ya kupokea mrejesho wa wadau

Mfuko umeendelea kuimarisha mfumo wa wadau kutoa mrejesho kupitia kituo cha huduma kwa wateja kinachotoa huduma saa 24, e-mrejesho na mfumo wa ndani TAI na mitandao ya kijamii ya Mfuko. Mifumo hii imewezesha wananchi kutatua changamoto zao kwa uharaka zaidi lakini kuwasilisha maoni na mrejesho wa huduma. Ofisi zilizofunguliwa ni pamoja na Kigamboni, Gongolamboto na Ubungo, Tegeta, Mbinga, Kahama, Masasi, Ifakara, Katoro, Bukombe, Karagwe, Tunduma na Nzega ambazo zimefanya idadi ya ofisi za Mfuko kuwa 41.

Kuongeza kasi ya usajili wa wanachama kwa kushirikiana na wadau wa usajili na mpaka sasa Mfuko umeingia makubaliano na Wakala wa bima nchini na Vodacom Mpesa kwa ajili ya kuanza kusajili wanachama.

Mfuko umeendelea kuimarisha mfumo wa wadau kutoa mrejesho kupitia kituo cha huduma kwa wateja kinachotoa huduma saa 24, e-mrejesho na mfumo wa ndani TAI na mitandao ya kijamii ya Mfuko. Mifumo hii imewezesha wananchi kutatua changamoto zao kwa uharaka zaidi lakini kuwasilisha maoni na mrejesho wa huduma.

Mfuko umeendelea na utoaji wa elimu ya bima ya afya kwa wananchi kupitia mbinu mbalimbali ikiwemo ya mikutano na wadau wake ambao ni pamoja na wanachama, watoa huduma, waajiri, vyama vya wafanyakazi, waandishi wa habari, Waheshimiwa Wabunge na viongozi wa madhehebu ya dini pamoja na vyombo vya Habari ikiwemo mitandao ya kijamii.

Bw. Abubakar Ndwata
Meneja wa Tathmini, Takwimu na Hadhari

UHAI WA MFUKO WAIMARIKA

1.0 Uboreshaji wa Uhai na Uendelevu wa Mfuko

Kipindi cha Awamu ya Sita kimeshuhudia juhudi za kina za kuimarisha msingi wa kifedha na utawala wa NHIF ili kuhakikisha kuwa Mfuko unaendelea kuwahudumia wananchi kwa ufanisi kwa miaka ijayo.

1.1 Uboreshaji Mkubwa wa Uhai wa Kifedha (Funding Ratio):
Mfuko umeweza kufanya mageuzi makubwa ya kifedha yanayoonekana wazi katika kuimarika kwa uhai wake. Mwaka 2022/23, uhai wa mfuko ulikuwa ni mwaka mmoja tu. Hata hivyo, kufuatia mikakati madhubuti ya kifedha, hadi kufikia mwaka 2024/25, uhai wa Mfuko umeongezeka na kufikia mwaka mmoja na miezi tisa. Hii inaonyesha kuongezeka kwa uwezo wa kudumu kwa muda mrefu (sustainability).

1.2 Kugeuka kwa Mtiririko wa kifedha:
Mfuko umefanikiwa kugeuza hali yake ya kifedha kutoka kwenye kupata nakisi kwa miaka mitatu mfululizo hadi kuanza kupata faida kwa miaka miwili mfululizo (2023/24 na 2024/25). Hali hii imetokana na sababu nyingi zikiwemo: usimamizi bora wa rasilimali na uongozi mzuri, kuboresha ukusanyaji wa mapato, kudhibiti matumizi yasiyo ya lazima (kwenye ulipaji wa madai pamoja na shughuli za kiutawala) pamoja na kutekeleza mapendekezo yaliyotolewa na mtaalam elekezi wa Tathmini ya Mfuko (Actuarial Valuation) ya kipindi kinachoishia Juni 2021.

Kuboreka kwa uhai wa Mfuko, kumesaidia kuweka NHIF kwenye msingi thabiti wa kifedha, zikiongeza uwezo wake wa kukabiliana na misukumo na kuhakikisha huduma za afya za watu zinadumishwa. Pia imepelekea kuongezeka kwa fedha za uwekezaji kupitia bakaa inayopatikana ambazo huwekezwa katika vyanzo mbalimbali, kupata riba na kuongeza mtaji wa taasisi.

2.0 Utengenezaji wa Vifurushi (Products Development)

Mfuko umeboresha utengenezaji wa vifurushi ambapo umezingatia uwezo wa wananchi kuchangia, upatikanaji wa huduma za msingi, uendelevu na uhai wa Mfuko pamoja na mahitaji ya jamii kutokana na mrejesho unaotolewa kupitia njia mbalimbali.
Ili kukidhi mahitaji mbalimbali ya wananchi, NHIF imeboresha na kupanua vifurushi vyake kwa wanachama binafsi kwa kiasi kikubwa zaidi, ikiwa ni mkakati wa kuwafikia wale walio kwenye sekta isiyo rasmi na wenye uwezo mdogo wa kifedha.

2.1 Kuboreshwa kwa Vifurushi:
Mfuko umebadilisha kabisa muundo wake wa vifurushi kwa wanachama binafsi ambapo badala ya vifurushi vitatu (3) vilivyokuwepo awali, NHIF imeanzisha vifurushi vipya vitano (5). Kuwapo kwa vifurushi zaidi kunamwezesha mwananchi kuchagua kifurushi kinacholingana zaidi na uwezo wake wa kifedha na mahitaji yake ya kiafya.

2.2 Kupunguzwa kwa Kiwango cha chini cha Mchango:
Kwa kutambua uwezo wa kifedha wa wananchi, NHIF imepunguza kiwango cha chini cha mchango kwa wanachama binafsi. Kiwango cha chini cha mchango kimepunguzwa kutoka shilingi 192,000/= kwa mwaka iliyokuwa ikilipwa awali, hadi shilingi 168,000/= kwa mwaka. Hii imelenga kuwafanya wananchi wengi zaidi waweze kumudu huduma za bima ya afya.

2.3 Kuongezeka kwa Idadi na Uwiano wa Huduma:
Uanzishwaji wa vifurushi vipya na zaidi kumepelekea kuongezeka kwa idadi ya huduma zinazopatikana kwa wanachama. Huduma za ziada na bora zaidi zimeongezwa katika orodha ya huduma, na kuwapa wateja uhuru wa kupata matibabu katika nyanja zaidi za afya.

3.0 Udhibiti wa Vihatarishi na Majanga

Chini ya uongozi wa Awamu ya Sita, NHIF imeendelea, kwa makini, kutekeleza utaratibu wa ndani wa kudhibiti vihatarishi na kukabiliana na majanga yanayoweza kuuharibu kiutendaji Mfuko. Mikakati hii imelenga hasa kulinda rasilimali za Mfuko, kuhakikisha mwendelezo wa huduma, na kumkinga mwanachama. Kwa kutambua umuhimu wake, Mfuko ulianzisha kitengo maalum kinachoshughulikia udhitibi wa vihatarishi na majanga ambao hufanya kazi ya kuchambua na kupima vihatarishi mbalimbali vya kifedha na kiutendaji pamoja na kufuatilia utekelezaji katika udhibiti wa majanga kwenye ofisi zote za Mfuko zilizopo nchi nzima.

3.1 Udhibiti Bora wa Mfiduo wa Hatari (Risk Exposure):

Kupitia uchambuzi wa kina pamoja na kuchukua hatua stahiki juu ya hatari zinazoweza kutokea, NHIF imeweza kuhakikisha kuwa kiwango cha mfiduo wa hatari (Risk Exposure) hakifikii viwango hatarishi ambapo hadi mwezi Juni 2024 kiwango hicho kilikuwa kwenye asilimia 48.
Kiwango hiki kipo chini ya kiwango cha juu kinachokubalika (acceptable limit) ikiashiria kuwa Mfuko umeweza kuepuka hatari nyingi zikiwemo za kifedha na una uwezo wa kustahimili misukumo ya kiutekelezaji na kiuchumi. Udhibiti huu wa hatari umeuokoa Mfuko na hasara mbalimbali zikiwemo za kifedha pamoja na kuhakikisha kuwa huduma zinaendelea kutolewa kwa wanachama wake.

3.2 Kupitia usimamizi na udhibiti wa majanga, Mfuko umepata mafanikio mengi yakiwemo;

a) Kudhibiti ukuaji wa madai ambapo madai ya Mfuko yamepungua kutoka shilingi bilioni 743 mwaka 2022/23 hadi shilingi bilioni 539 mwaka 2024/25;

b) Kuhakikisha kuwa hakuna maamuzi makubwa ya kimkakati yanafanyika bila kufanyika tathmini ya udhibiti wa vihatarishi (risk assessment);

c) Kuongeza mapato ya uwekezaji ambapo kwa mwaka 2024/25, mapato ya uwekezaji yaliongezeka kwa asilimia 16 ikilinganishwa na miaka ya nyuma ambapo mapato ya uwekezaji yalikuwa yanapungua;

d) Kuhakikisha mifumo inayotumika na Mfuko inaweza kurudi kwa wakati pale inapotokea hitilafu na kuhakikisha huduma zinaendelea kutolewa kwa wateja wa Mfuko;

e) Kuendelea kuchukua hatua kali dhiti ya vitendo vya udanganyifu vinavyofanywa na baadhi ya watoa huduma, wanachama na waajiri;

f) Kuhakikisha hakuna kesi zidi ya Mfuko zinazoweza kupelekea upotevu wa fedha au kuchafua picha ya Mfuko kwenye jamii; na

g) Kuhakikisha kuwa Mfuko unakuwa na sifa ya uzingativu wa juu wa kanuni za udhibiti (high regulatory compliance).

Mikakati hii ya ndani imeweza kuulinda Mfuko na hasara kubwa za kifedha na kisheria. Imepunguza kwa kiasi kikubwa udanganyifu na uvujaji wa fedha, na kuhakikisha kwamba michango ya wanachama inatumika kwa mujibu wa malengo ya Mfuko. Pia, imejenga imani na uhakika kwa wanachama kwamba fedha zao zinatumiwa kwa uadilifu na kwamba Mfuko utaendelea kuwahudumia hata wakati wa shida.

Bw. Neligwa Maira
Meneja Kitengo cha Ukaguzi wa Ndani

UKAGUZI WA NDANI WAWEZESHA UPATIKANAJI HATI SAFI

- **Yasimamia Miongozo na Taratibu katika Kazi**

Kitengo cha Ukaguzi wa Ndani (IAU) ndani ya Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya kimeanzishwa kwa mujibu wa Kanuni ya 28 ya Kanuni za Fedha za Umma za mwaka 2001. Kitengo kimeendelea kutekeleza majukumu yake ya msingi ya kutoa uhakikisho na ushauri kwa Menejimenti na Bodi, kuhusu ufanisi wa mifumo ya udhibiti wa ndani, usimamizi wa vihatarishi na taratibu za utawala bora.

Kitengo cha Ukaguzi wa Ndani kinaundwa na wataalamu mbalimbali kama wahasibu, maafisa manunuzi na ugavi, madaktari, wafamasia, na maafisa TEHAMA. Wataalamu hawa huwezesha Kitengo kufanya kazi zake kwa ufanisi na kuwezesha kuisaidia menejimenti kwenye uboreshaji wa ufanisi kwenye utendaji wa Kurugenzi na Vitengo mbalimbali.

Katika kipindi hiki cha miaka minne ya Uongozi wa Serikali ya Awamu ya Sita, kitengo kimeweza kusaidia Mfuko katika uzingatiaji wa sheria, miongozo na taratibu na kuwezesha Mfuko kupata hati safi kila mwaka kwa kutekeleza yafuatayo;-

1.0 Utekelezaji wa hoja za ukaguzi

Kwa kushirikiana na Menejimenti, Kitengo kimefanikiwa kufuatilia kwa karibu mapendekezo yaliyotolewa na Mkaguzi wa ndani na Mkaguzi wa nje na kuwezesha menejimenti kutekeleza mapendekezo ya ukaguzi na kupata hati safi.

2.0 Kuimarisha uwajibikaji:

Kupitia mrejesho wa mara kwa mara kwa Menejimenti na Bodi, Kurugenzi na vitengo husika vilichukua hatua za haraka kutekeleza mapendekezo, jambo lililoimarisha nidhamu ya kiutendaji.

3.0 Mafunzo ya kujenga uwezo:

Kitengo kilitoa mafunzo ya shughuli za ukaguzi na usimamizi wa utekelezaji wa mapendekezo, hivyo kuongeza uelewa na ufanisi katika kufuatilia na kutoa ushauri.

4.0 Ukaguzi wa Uzingatiaji wa Sheria, Miongozo na Taratibu

Ukaguzi uliofanyika ulionesha kupungua kwa kasoro zinazohusiana na uvunjifu wa Sheria, Kanuni, Miongozo na Taratibu za Mfuko kwenye usimamizi wa manunuzi, fedha, wanachama, madai na utawala.

Kitengo kilitoa ushauri wa mara kwa mara kwa menejimenti kuhusu maboresho ya mifumo mbalimbali, utekelezaji wa shughuli mbalimbali za Mfuko na uzingatiaji wa sheria

na miongozo, hivyo kupunguza hatari ya ukiukwaji wa kisheria.

5.0 Ukaguzi kutumia Mifumo

Kitengo cha ukaguzi kinatumia mfumo wa "ACL" kwenye uchakataji wa taarifa mbalimbali wakati wa maandalizi ya ukaguzi. Mfumo huu huwezesha kitengo kuchakata taarifa nyingi kwa muda mfupi na hivyo kuweza kubaini mapungufu mbalimbali na kuishauri menejimenti ipasavyo.

6.0 Ukaguzi unaozingatia maeneo hatarishi

Ukaguzi wa kufuata taratibu (compliance audits) ulisaidia kubaini mapungufu mapema na kuchukua hatua za haraka za marekebisho.

Kutokana na haya, Kitengo cha Ukaguzi kimefanikiwa kuimarisha nidhamu ya utekelezaji wa mapendekezo ya ukaguzi na kuongeza kiwango cha uzingatiaji wa sheria, miongozo na taratibu. Mafanikio haya yamechangia kwa kiasi kikubwa katika kuimarisha uwajibikaji, uwazi na ufanisi wa Mfuko.

Bi. Leonia Masmin
Meneja Kitengo cha Ununuzi na Ugavi

NHIF YAPATA HATI SAFI ZA UNUNUZI

Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya (NHIF) ni Taasisi ya Umma ambayo pamoja na majukumu yake mengine, inajukumu la kufanya manunuzi mbali mbali kupitia kitengo chake cha Ununuzi kwa kuzingatia Sheria ya Ununuzi wa Umma na kanuni zake. Katika kipindi cha utekelezaji wa sheria hiyo, Mfuko umeweza kupata mafanikio makubwa kutokana na mikakati mbalimbali, hususan katika eneo la kujenga uwezo wa watumishi na kuhakikisha uzingatiaji wa taratibu za ununuzi. Mafanikio hay oni pamoja na;-

1.0 Mafunzo kwa Watumishi

Katika kujenga uwezo wa watumishi na kuongeza tija kwenye utekelezaji wa Sheria ya Ununuzi wa Umma, Mfuko kupitia Kitengo cha Ununuzi uliendesha na kushiriki katika mafunzo mbalimbali yaliyolenga kuongeza uelewa na weledi wa watumishi. Baadhi ya mafunzo hayo ni pamoja na:

2.0 Mafunzo ya Sheria ya Ununuzi na Kanuni zake

Mfuko uliwezesha Watumishi wake wote kupata mafunzo mbalimbali kwa makundi yakiwemo ya Sheria ya Ununuzi na Kanuni zake yaliyofanyika Mkoani Dodoma Oktoba, 2024.

3.0 Mafunzo ya Sheria ya Ununuzi na Kanuni zake zilizoboreshwa

Mafunzo haya yalifanyika Juni 2021 mkoani Arusha yakiwa na lengo la kuongeza uelewa wa watumishi juu ya sheria na taratibu za manunuzi ili kuongeza ufanisi na kuondoa changamoto zinazoweza kujitokeza katika mchakato wa manunuzi.

Mafunzo ya Mfumo Mpya wa NeST uliobadilisha TANePS;

Mfumo wa NEST ulianzishwa ili kuboresha usimamizi wa mchakato wa manunuzi kwa njia ya kidigitali. Watumishi wa Kitengo walipatiwa mafunzo haya tarehe 21–25 Agosti 2023 mkoani Iringa, ambapo walipata ujuzi wa kutosha kuhusu matumizi ya mfumo huo mpya na namna unavyosaidia katika uwazi na uwajibikaji wa manunuzi. Pia kumekuwa na uendelevu wa kupatiwa mafunzo ya NeST kwa watumishi kila moduli mpya inapo anzishwa na Mfuko umekuwa ukiwezesha ushiriki.

4.0 Mafunzo ya Sheria Mpya ya Manunuzi ya 2023 na Kanuni zake za 2024;

Mafunzo haya yalifanyika tarehe 19–23 Agosti 2024 mkoani Morogoro. Watumishi waliweza kufahamu kwa undani mabadiliko yaliyopo kwenye sheria mpya na kanuni zake, jambo

ambalo limeongeza uwezo wa Mfuko kutekeleza majukumu yake kwa kuzingatia miongozo mipya ya kisheria na kanuni.

5.0 Ushiriki wa warsha na makongamano yalitolewa na Bodi ya Ununuzi na Ugavi (PSPTB) na Mamlaka (PPRA).

Watumishi waliweza kushiriki katika warsha 5 na makongamano 5 kwa kipindi cha mwaka 2021 hadi sasa yaliyofanyika sehemu mbalimbali na yaliyo tolewa na Mamlaka na Bodi ya Ununuzi na Ugavi. Ushiriki wa warsha na makongamano hayo yaliweza kuongeza tija katika ufanisi wa utendaji kazi,

Mafunzo haya yote kwa pamoja yamekuwa chachu ya kuongeza weledi, uwajibikaji na ufanisi wa Kitengo cha Ununuzi na Ugavi katika utekelezaji wa majukumu yake.

6.0 Hati Safi Katika Ununuzi (2021–2025)

Katika kipindi cha mwaka 2021 hadi 2025, Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya umekaguliwa mara kadhaa na taasisi husika zikiwemo Mamlaka za Udhibiti na Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali. Katika kaguzi zote,

Mfuko umeendelea kupata hati safi kwenye eneo la manunuzi.

Mafanikio haya yametokana na utekelezaji wa Sheria ya Ununuzi wa Umma na kanuni zake, uwajibikaji na weledi wa watumishi wa Kitengo cha Ununuzi, uwepo wa mifumo bora ya usimamizi wa manunuzi na uwekezaji katika mafunzo ya mara kwa mara

Kutokana na utekelezaji wa Sheria ya Ununuzi wa Umma, Mfuko umepata mafanikio makubwa katika kipindi cha mwaka 2021 hadi 2025. Mafanikio haya yamejidhihirisha kupitia uongezaji wa ujuzi na maarifa kwa watumishi kupitia mafunzo mbalimbali na kupata hati safi za ukaguzi kipindi chote cha miaka minne mfululizo.

NHIF itaendelea kujenga uwezo wa watumishi na kuimarisha mifumo ya usimamizi ili kuhakikisha utekelezaji wa Sheria ya Ununuzi wa Umma unazidi kuleta tija na manufaa kwa taasisi na kwa umma kwa ujumla.

NHIF YADHIBITI UDANGANYIFU

- **Yaokoa zaidi ya billioni 30**
- **Mifumo sasa kubaini udanganyifu**

Dkt. Rose Ntundu
Meneja Kitengo cha Udhibiti wa Vitendo vya Udanganyifui

Na Mwandishi Wetu

Katika jitihada za kudhibiti na kupambana na vitendo vya udanganyifu, Mfuko umekuwa ukifanya chunguzi mbalimbali kwa watoa huduma, waajiri, wanachama na watumishi wa ndani. Aina mbali mbali za vitendo vya udanganyifu ambavyo Mfuko unakabiliana navyo ni pamoja na;

1.0 Watoa huduma waliosajiliwa na Mfuko

Vitendo vya udanganyifu ambavyo vimekuwa vikifanywa na kundi hili ni pamoja na; Kuwasilisha madai kwa huduma ambazo hazikutolewa kwa wanachama wa Mfuko;Kuwasilisha madai ya huduma za gharama ya juu ikilinganishwa na huduma iliyotolewa; Kudai ada ya kumuona daktari bingwa ili hali mgonjwa alionwa na daktari wa kawaida; Kushirikiana na maduka ya dawa binafsi yaliyosajiliwa na Mfuko kwa kuwasilisha madai ya udanganyifu na kutunza kumbukumbu za uongo kwenye vituo vya huduma ili kuhalalisha madai ya uongo yaliyowasilishwa NHIF.

2.0 Waajiri Binafsi

Kwa upande wa Kundi hili, vitendo vya udanganyifu vimekuwa vikifanywa na waajiri wa sekta binafsi ambavyo ni pamoja na;kuwasilisha taarifa za michango zenye udanganyifu ili kupunguza kiasi cha mchango unaostahili kuwasilishwa katika Mfuko; kuwasilisha orodha ya wafanyakazi hewa kwa lengo la kuwawezesha wasio waajiriwa kupata huduma za Mfuko.

3.0 Wanufaika/Wanachama wa Mfuko

Vitendo vya udanganyifu vinavyofanywa na kundi hili ni pamoja na; Kuwapatia wagonjwa ambao siyo wanufaika wa Mfuko vitambulisho vya uanachama na kuvitumia wakati wa kupata huduma za matibabu; Kutumia kadi ya uanachama kwa njia ya udanganyifu ili kujipatia kipato kwa kuchukua dawa na kuziuza kwa wamiliki wa maduka, kuuza nafasi kwa wategemezi wasiostahili na Kuwasilisha nyaraka za kughushi, kutoka katika mamlaka mbalimbali, wakati wa kuwasilisha maombi ya kujaza nafasi za wategemezi.

4.0 Watumishi wa Mfuko

Vitendo vya udanganyifu ambavyo vimekuwa vikifanywa na baadhi ya watumishi wasio waaminifu ni pamoja na kutengeneza kadi za NHIF kwa wanufaika wasiostahili; Kupokea michango kwa njia ya fedha taslimu na kutowasilisha katika Mfuko na kupelekea kutengeneza kadi bila ya michango na Kushirikiana na watoa huduma katika kujipatia kipato kwa njia isiyo halali.

Katika kipindi cha miaka minne ya Uongozi wa Serikali ya Awamu ya Sita, Mfuko umekuwa na mafanikio katika maeneo mbalimbali yakiwemo ya;-

5.0 Uchunguzi Uliofanywa na Mfuko

Katika kipindi cha kuanzia mwezi Julai 2021 hadi Juni 2025, Mfuko umefanya uchunguzi kwa jumla ya matukio 538 ya viashiria vya udanganyifu na hivyo hatua stahiki kulingana na miongozo ya Mfuko zilichukuliwa.

Hatua zilizochukuliwa ni pamoja na kurejesha fedha zilizogundulika kuwa ni za udanganyifu. Kupitia

chunguzi hizo 538 Mfuko uliokoa jumla ya Tsh. billioni 30.5, kusitisha jumla ya mikataba 33 kwa watoa huduma, kutoa taarifa katika mabaraza ya taaluma ambapo jumla ya Watumishi wa Sekta ya Afya 221 waliobainika kujihusisha na vitendo vya udanganyifu .

Hatua nyingine ni pamoja na kusitisha matumizi ya vitambulisho vya wanufaika na kurejesha fedha ambapo jumla ya vitambulisho 13,984 vya wanufaika waliogundulika kufanya vitendo vya udanganyifu vilisitishwa.

6.0 Kuchukua Hatua za kinidhamu kwa watumishi wa Mfuko

Mfuko hauna uvumilivu na vitendo vya udanganyifu (fraud zero tolerance) na hivyo huchukua hatua stahiki za kinidhamu kwa watumishi wake wanaobainika kujihusisha na vitendo vya udanganyifu. Katika kipindi cha kuanzia Julai 2021 hadi Juni 2025, Mfuko ulichukua hatua za kinidhamu kwa jumla ya watumishi 17 waliobainika kujihusisha na vitendo vya udanganyifu.

7.0 Kusitisha mikataba na Vituo

Katika kipindi cha kuanzia Julai 2021 hadi Juni 2025, Mfuko umesitisha mikataba kwa jumla ya vituo vya huduma 33 kutokana na vitendo vya udanganyifu.

8.0 Kufungua mashtaka dhidi ya waliobainika na vitendo vya udanganyifu

Jumla ya mashtaka 5 kwa wanachama 67 waliobainika kufanya vitendo vya udanganyifu yamefunguliwa na Mfuko na yapo katika hatua mbalimbali kwa mujibu wa Sheria na taratibu za nchi.

9.0 Kuwasilisha taarifa za uchunguzi TAKUKURU kwa ajili ya hatua zaidi

Jumla ya taarifa za vituo vya kutolea huduma 43 na taarifa ya wanachama 148 ziliwasilishwa TAKUKURU kwa ajili ya hatua zaidi.

10.0 Mafunzo ya Kupambana na Vitendo vya Udanganyifu kwa Watumishi wa Mfuko

Ili kuweze kuboresha ufanisi katika kupambana na vitendo vya udanganyifu, katika kipindi cha kuanzia Julai 2021 hadi Juni 2025, Mfuko ulitoa mafunzo ya kupambana na vitendo vya udanganyifu kwa watumishi wake wote.Aidha kupitia vyombo vya Habari, Mfuko umekuwa na program mblimbali za kuelimisha na kuonya kuhusu vitendo hivyo.

11.0 Mikakati ya kudhibiti udanganyifu

Katika kuendelea kupambana na vitendo vya udanganyifu kwa watoa huduma, waajiri, wanachama na watumishi wa Mfuko kwa ujumla, Mfuko umeendelea kufanya yafuatayo;-

(i) Kuendelea kuimarisha mifumo ya ndani ya TEHAMA ya uchakataji madai ili kuweza kuzuia, na kugundua vitendo vya udanganyifu mapema;

(ii) Kuendelea kushirikiana na vyombo vingine vya dola kama Polisi na TAKUKURU katika chunguzi za kina pale inabidi kushirikiana;

(iii) Kuendelea kuchukua hatua kali kwa vituo vya huduma vinavyobainika kufanya vitendo vya udanganyifu ikiwa ni pamoja na kusimamishiwa kutoa huduma kwa wanachama wa Mfuko;

(iv) Kutoa elimu endelevu kwa watumishi wa ndani na wadau wengine juu ya madhara ya vitendo vya udanganyifu.
Mafanikio yaliyopatikana katika kipindi hiki ni pamoja na;-

Kuanzisha namba ya bure 0800111163 (Fraud stopper Toll free number) ya kupokea taarifa za vitendo vya udanganyifu dhidi ya Mfuko kwa siri. Namba hii imesaidia Mfuko kupokea taarifa za udanganyifu zaidi ya 58 ambazo zimepelekea kugundulika kwa udanganyifu na kupelekea Mfuko kuokoa zaidi ya billioni 2.67

Kuandaa na kuboresha miongozo mbalimbali ya kitengo cha kupambana na vitendo vya udanganyifu ambayo ni *Antifraud Manual, Antifraud Policy, Whistle Blower Policy* na *Standard Operating Procedures;*

Kuimarisha Kitengo cha kupambnana na vitendo vya udanganyifu ambapo watumishi saba (7) wa Kitengo kupata Professional Certification na kuwawezesha watumishi hao kutambulika kimataifa kama *Certified Fraud Examiner*

Kuimarisha na kujenga ushirikiano na vyombo vya dola vya kiuchunguzi kama TAKUKURU na JESHI LA POLISI. Katika kipindi husika zaidi ya chunguzi 36 zimefanywa na Mfuko kwa kushirikiana na vyombo hivyo

Dkt. Raphael Mallaba
Meneja wa Mkoa

KINONDONI

MAFANIKIO YA NHIF KINONDONI

- Uridhishwaji wa Huduma waongezeka kwa 92%
- Maboresho huduma yavutia wananchi kujiunga NHIF

Kinondoni ni moja ya Ofisi kubwa za Kimkakati za Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya (NHIF), inayohudumia wananchi wengi wa Mkoa wa Dar es Salaam katika eneo la bima ya afya.

Ofisi ya Kinondoni inahudumia Waajiri 668 ikiwa na jumla ya vituo vya kutolea huduma 259 vinavyojumuisha vituo vya Serikali, Binafsi na Vituo vinavyomilikiwa na madhehebu ya dini. Wigo huu wa vituo unatoa fursa kwa wanachama kuchagua au kupata huduma za matibabu kwa urahisi zaidi.

Katika kipindi cha Miaka Minne ya Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Ofisi ya Kinondoni imepata mafanikio mbalimbali ya kihuduma ambayo yamewezesha kuboresha huduma kwa wanachama na Sekta ya afya kwa ujumla.

1.0 MAFANIKIO YA SERIKALI YA AWAMU YA SITA

1.1 Wigo wa Wanachama waongezeka kwa 40%

Katika kuhakikisha Mfuko unawafikia wanachama wengi zaidi kuelekea utekelezaji wa Bima ya Afya kwa Wote, Ofisi ya Kinondoni imefanikiwa kuwa na ongezeko la wanachama 35,163 ambapo idadi ya wanachama ilikuwa 51,723 hadi kufikia idadi ya wanachama 86,886 Juni 2025. Hatua hii imesaidia kuendelea kuimarika kwa uhai wa Mfuko na kuwezesha upatikanaji wa huduma bora zaidi.

1.2 Kusogeza huduma kwa wananchi

Kutokana na mwamko mkubwa wa wananchi kujiunga na bima ya afya, Ofisi ya Kinondoni imefanikiwa kusogeza zaidi huduma kwa wananchi ambapo imefungua ofisi ndogo katika Kituo cha Mabasi cha Magufuli na Ofisi nyingine katika eneo la Tegeta. Ofisi hizi zimefunguliwa kwa lengo la kuleta ufanisi katika kuwafikia wananchi ili waweze kupata elimu na kusajiliwa kwa urahisi zaidi.

1.3 Maboresho ya Mifumo

Katika kipindi cha miaka minne ya Serikali ya Awamu ya Sita, NHIF imefanikiwa kwa kiwango kikubwa kufanya maboresho ya mifumo ambayo yamerahisisha usajili wa wanachama, uwasilishaji na uchakati wa madai ambapo kwa sasa mwananchi anaweza kujisajili popote alipo lakini pia madai kulipwa kwa wakati.

Matumizi ya mifumo yamesaidia kuondoa malalamiko ya kihuduma kwa wanachama ikiwemo ucheleweshaji wa vitambulisho, upatikanaji wa vibali kwa huduma zinazohitaji vibali pamoja na msongamano mkubwa wa wananchi katika Ofisi ya Kinondoni.

Awali Ofisi ya Kinondoni ilikuwa inahudumia wanachama zaidi ya 300 kwa siku ambao walilazimika kufika ofisini lakini kwa sasa wanachama hao wanapata huduma zote za usajili na michango wakiwa majumbani au makazini kwao, hatua hii imesaidia kuondoa usumbufu kwa wananchi wa kuja ofisini.

1.4 Kampeni za Uhamasishaji Jamii

Katika kipindi cha miaka minne Mfuko umeendelea kufanya kampeni mbalimbali za uhamasishaji katika taasisi za serikali, binafsi, mitaa, kata, vyuo, mashule, makanisa, misikiti na matamasha ya kijamii kama ikiwemo Tamasha la Twenzetu kwa Yesu na Tamasha la Siku ya Wanawake ambayo wananchi wengi walipata elimu juu ya umuhimu wa bima lakini pia ilileta msukumo wa wananchi kujiunga.

Aidha, Ofisi ya NHIF Kinondoni imeendelea na utoaji wa elimu kupitia vyombo mbalimbali vya Habari, Makongamano na kwenye maeneo yanayokusanya wananchi wengi. Hii inafanyika ili kuhakikisha wananchi wanapata elimu na wanahamasisha kujiunga na NHIF ili kuwa na uhakika wa kupata huduma za matibabu wakati wowote.

1.5 Dawati la Huduma za Ziada (Corporate Desk)

Ofisi ya NHIF Kinondoni imefanikiwa kuwa na dawati maalumu la huduma za ziada ili kuwezesha upatikanaji wa huduma kwa haraka kwa Kundi hili nah ii imepunguza malalamiko na imeweza kuimarisha mahusiano ya Mfuko na waajiri na kuongeza idadi ya waajiri wanaojiunga na huduma za ziada. Hatua hii imeongeza wigo kutoka waajiri 9 hadi kufikia waajiri hadi 35.

1.6 Wito kwa wananchi

Meneja wa Ofisi ya Kinondoni, Dkt. Raphael Mallaba amewaomba wananchi kutumia ofisi hiyo na Ofisi ndogo za Ubungu na Tegeta kwa ajili ya kupata huduma na kutatua changamoto wanazokumbana nazo wakati wanapokuwa vituoni.

Aidha amesema kuwa Ofisi yake imejipanga kuhakikisha wanafika maeno yote ya Kinondoni kwa ajili ya kuwahudumia wananchi hususan katika kipindi hiki cha kutekeleza Bima ya Afya kwa Wote.

Dkt. Eliud Kilimba
Meneja wa Mkoa

MBEYA

MBEYA YAPANUA WIGO WA VITUO VYA HUDUMA

- Huduma za matibabu zaimarika
- Yajipanga kuwafikia wananchi wote

Mkoa wa Mbeya ni kati ya mikoa 31 inayounda Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania ukiwa Nyanda za juu Kusini, Mkoa umepakana na mikoa ya Njombe,Tabora Singida, Rukwa Pamoja na nchi jirani ya Jamhuri ya Malawi kwa upande wa mashariki.

Mkoa wa Mbeya unaundwa na Wilaya tano (5) ambazo ni ni pamoja na Mbeya, Kyela, Rungwe, Mbarali, Chunya.

Kwa mujibu wa takwimu za Sesa ya watu na makazi ya mwaka 2022 Mkoa wa Mbeya una jumla ya wakazi 2,343,754 ambao wanashiriki katika shughuli mbalimbali za kiuchumi ikiwemo kilimo, ufugaji, uchimbaji na uchenjuaji wa madini, Uvuvi na shughuli za viwanda na biashara.

Ili wananchi wa Mkoa wa Mbeya wawe na uhakika wa huduma za matibabu, Mfuko unayo ofisi mkoani humo ambayo inalo jukumu la kuhakikisha inawafikia wananchi mmoja mmoja, vikundi au ushirika waliomo ili waweze kujiunga na bima ya afya.

Katika kipindi cha miaka minne ya Serikali ya Awamu ya Sita, Ofisi ya NHIF Mbeya ina jumla ya wanachama wachangiaji 35,599 wanaojumuisha waajiri wa umma, waajiri binafsi na waajiri wa mashirika ya dini. Aidha Ofisi imejiwekea lengo la kusajili waanachama 65,878 kutoka makundi mbalimbali ya watanzania .

1.0 Usajili wa Vituo vya kutolea huduma

Mafanikio katika eneo hili, jumla ya Vituo vya kutolea huduma 380 vimesajiliwa vikijumuisha vituo vya Serikali, Binafsi na vya mashirik ya dini ambavyo vimerahisisha upatikanaji wa huduma kwa wanachama wa Mfuko mkoani Mbeya.

2.0 Ulipaji wa madai

Ulipaji wa madai kwa watoa huduma umekuwa na mafanikio makubwa kutokana na kuanza kulipa madai ndani ya siku 45 ikilinganishwa na awali ambapo madai yalilipwa ndani ya mud awa siku 60. Mafanikio haya yanatokana na maboresho ya mifumo ya uwasilishaji na uchakataji wa madai ambao umepunguza malalamiko kutoka kwa watoa huduma.

3.0 Mahusiano na wadau

Mfuko umefanikiwa kujenga na kuendelea kuimarisha mahusiano na wadau wake ikiwemo Ofisi ya Mkuu wa Mkoa, Ofisi ya Katibu tawala wa Mkoa pamoja na wasaidizi wake wote katika halmashauri zote za mkoa wa Mbeya.

Mafanikio haya yamekuwa na tija katika kutimiza azma njema ya serikali kuhakikisha wananchi wote wanajiunga na bima ya afya ili wawe na uhakika wa matibabu bila changamoto ya fedha.

4.0 Yashiriki Maonesho ya Nane Nane

Ofisi ya Mbeya imekuwa ikishiriki maonesho ya Kitaifa na ya mialiko kutoka kwa wadau mbalimbali. Maonesho hayo ni pamoja na Nane Nane. Maonesho haya yamekuwa chachu kwa wananchi kupata elimu, kujiunga, kupata mrejesho na utatuzi wa changamoto mbalimbali.

5,0 Utekelezaji wa Bima ya Afya

Ili kuhakikisha wananchi wengi zaidi wanafikiwa kupitia utekelezaji wa Bima ya Afya kwa Wote, Ofisi imejiwekea malengo ya kuongeza kampeni za elimu na uhamasishaji ili kuwezesha usajili wa wanachama wapya wengi zaidi.

Aidha Mfuko utashirikiana na wadau wengine wakiwemo mabalozi na viongozi wa Serikali za Mitaa ili kuongeza ushawishi kwa wananchi.

Taarifa za uanachama
Anuani za ofisi za NHIF nchi nzima
Taarifa za wategemezi wako
Vituo vya matibabu vilivyo karibu nawe
Orodha ya dawa na vipimo vilivyopo kwenye Kitita cha Mafao
Home
News
FAQs
Products
Facilities
Services
Contacts
Prices
Tools
Member
NHIF Tanzania
JIPAKULIE
Huna haja ya kupata tabu, pata taarifa mbalimbali za uanachama wako kupitia
NHIF APP
ANDROID APP ON Google play
Available on the iPhone App Store

MANYARA

- Huduma za kibingwa zapatikana ndani ya mkoa
- Yahamasisha wananchi kujiunga na NHIF

Bw. Emmanuel Mwikwabe
Meneja wa Mkoa

Upatikanaji wa huduma za matibabu hususan za kibingwa, ilikuwa ni ndoto kwa baadhi ya wananchi wa baadhi ya mikoa hapa nchini ambapo walilazimika kusafiri umbali mrefu ili kupata huduma hizo hivyo walitumia gharama kubwa na wakati mwingine kupoteza maisha kwa kushindwa kufikia huduma hizo.

Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya ukiwa ni mdau mkubwa katika Sekta ya afya, inazo Ofisi zake katika Mikoa yote nchini kwa lengo la kusogez huduma kwa wananchi.

Mkoa wa Manyara unayo Ofisi ya NHIF ambayo ina jukumu kubwa la kuwafikia wananchi kwa lengo la kuwaelimisha, kuwahamasisha na kuwasajili ili wawe ndani ya mfumo wa bima ya afya ambao unawezesha kupata huduma za matibabu wakati wote.

Ofisi hii imefanikiwa katika maeneo mbalimbali ndani ya uongozi wa Serikali ya awamu ya Sita chini ya Uongozi wa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan. Mafanikio hayo ni pamoja na Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya (NHIF) kusajili vituo vyenye huduma za kibingwa.

Awali, wanachama walilazimika kusafiri umbali wa zaidi ya kilomita 200 kufuata huduma katika Mkoa wa Arusha. Wengine walilazimika hata kuhamia na kupanga makazi ya kudumu Arusha ili wawe karibu na huduma hizo. Hali hii ilisababisha usumbufu mkubwa, gharama za kifedha na changamoto za kijamii kwa wanachama na familia zao.

Kwa sasa, kutokana na jitihada za Mfuko na ushirikiano wa wadau wa afya, NHIF imesajili vituo viwili vinavyotoa huduma za kusafisha samu ndani ya Mkoa wa Manyara, ambavyo ni Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Manyara na Hospitali ya Haydom na hadi kufikia kufikia mwezi Agosti 2025, jumla ya wagonjwa 30 ambao ni wanachama wa Mfuko wamepatiwa huduma ya kusafisha damu na kuokoa maisha yao.

Kutokana na upatikanaji wa huduma hizi, wananchi wanaombwa kujiunga na bima ya afya ili kujihakikishia huduma za matibabu bila kikwazo cha fedha.

"Bima ya Afya kwa Wote, Jiunge sasa"

Bw. Simon Mmbaga
Meneja wa Mkoa

SONGWE

UWEPO WA NHIF SONGWE WACHOCHEA UPATIKANAJI HUDUMA

- **Wigo wa Vituo vya Huduma Waongozeka**

Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya (NHIF), unayo Ofisi yake katika Mkoa wa Songwe ambayo ilifunguliwa kwa lengo la kusogeza zaidi huduma kwa wananchi ili waweze kujiunga na bima ya afya.

Mkoa huo unazo shughuli mbalimbali za kiuchumi ikiwemo kilimo, ufugaji na biashara hivyo uwepo wa NHIF unasaidia kurahisisha upatikanaji wa huduma kwa wananchi.

Katika kipindi cha miaka minne ya uongozi wa Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, NHIF Songwe imekuwa na mafanikio mbalimbali ikiwemo ongezeko la vituo vya kutolea huduma ambapo kwa sasa jumla ya vituo 266 ambavyo vinahudumia wanachama katika mkoa huo.

Uwepo wa vituo hivyo umeongeza na kuimarisha upatikanaji wa huduma za msingi kwa wananchi wa maeneo ya vijijini na mijini. Aidha uwepo wa Hospitali ya Rufaa ya Mkoa inatoa huduma mbalimbali ambazo awali hazikupatikana hususan huduma za kitaalamu zaidi (kibingwa) pamoja na vifaa vya kisasa vya uchunguzi kama Dital X-ray na CT scan, vinavyowezesha utambuzi sahihi na matibabu bora.

Ofisi ya Songwe imeendelea kushirikiana na wadau na kuimarisha Mahusiano na wadau wa ndani na nje kupitia vikao vya mara kwa mara, vikao ambavyo vimeweka msingi wa mipango endelevu ya kuendeleza upatikanaji wa huduma za afya.

Kwa upande wa ongezeko la wanachama, Ofisi imeendelea kuwafikia wananchi na kuwasajili kupitia vifurushi vya bima ya afya ambavyo vimempa fursa kila mwananchi kuchagua na kujiunga.

Mafanikio mengine ni maandalizi ya utekelezaji wa Bima ya Afya kwa Wote ambapo Ofisi iko tayari kuwafikia na kuwasajili wananchi ili wawe na uhakika wa kupata huduma za matibabu wakati wote. Maandalizi hayo ni pamoja na kufungua Ofisi ndogo katika mji wa Tunduma ambapo itarahisisha huduma kwa wananchi bila kulazimika kusafiri umbali mrefu.

Kutokana na haya Ofisi ya NHIF Songwe iinaendelea na mikakati ya kushirikiana na wadau mkoani hapo ili kufikia malengo ya Bima ya Afya kwa Wote na kutoa huduma bora kwa wanachama wake.

Bw. Salum Adam
Meneja wa Mkoa

TABORA

- Tabora yasogeza huduma kwa wananchi
- Yaweka mikakati utekelezaji Bima ya Afya kwa Wote

Katika kuhakikisha wananchi wanafikiwa na huduma za Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya (NHIF), Mfuko ulisogeza huduma katika Mkoa wa Tabora kwa kufungua ofisi inayohudumia Halmashauri nane ambazo ni Halmashauri ya Manispaa ya Tabora, Uyui, Nzega, Sikonge, Igunga, Kaliua na Urambo. Mkoa huu unazo shughuli za kiuchumi ambazo ni ufugaji, kilimo cha kibiashara cha Tumbaku na Pamba.

Ili kuhakikisha wananchi wanafikiwa, Ofisi ya Mkoa wa Tabora inatekeleza majuku yake yakiwemo ya kuandikisha wanachama, kukusanya michango,

kusajili vituo vya kutolea huduma, kulipa madai kwa watoa huduma,
kufanya kaguzi kwa waajiri na watoa huduma pamoja na kutoa elimu kwa Umma.
Katika kipindi cha miaka minne ya Serikali ya Awamu ya Sita, Ofisi ya NHIF Tabora imefanikiwa katika maeneo mbalimbali ambayo ni pamoja na;-

1.0 Elimu kwa Umma

Katika kipindi cha miaka minne, Ofisi ya Tabora imewekeza katika utoaji wa elimu kwa wananchi juu ya dhana ya bima ya afya ili kuwezesha wananchi kufahamu faida za kuwa ndani ya mfumo wa bima ya afya.

Ofisi ya Mkoa imeendelelea kutumia njia mbalimbali za kutoa elimu kwa Umma ikiwemo matumizi ya vyombo mbalimbali vya habari kama vile Redio za Kijamii, mikusanyiko mikubwa inayofanyika kimkoa kama vile siku ya chanjo kitaifa, sikukuu za nane nane na siku ya ushirika Duniani

Ofisi imeendelea kutekeleza mkakati wa usajili wa wanachama kwa kuwafikia wananchi katika maeneo yao lakini pia maeneo ya masoko makuu, Vituo vya usafiri, nyumba za Ibada, vyuoni, shuleni, magulio na maeneo yenye mikusanyiko ya watu wengi. Kupitia mkakati huu, Ofisi imefanikiwa kufikia makundi 85 katika mwaka wa fedha 2024/25.

2.0 Yashiriki Maonesho Siku ya Ushirika

Mfuko umekuwa ukishiriki maonesho ya Kitaifa na ya mialiko kutoka kwa wadau mbalimbali. Maonesho hayo ni pamoja na Siku ya Ushirika Duniani ambapo hutumika kuhamasisha wakulima kupitia Vyama vya Ushirika kujiunga na kutoa elimu juu ya bima ya afya kwa wote.

3.0 Uandikishaji wanachama wapya

Katika eneo la Usajili, Ofisi ya Mkoa wa Tabora imekuwa na ongezeko la wanachama wapya 8,875 ambapo kwa sasa mwamko umeendelea kuwa mkubwa kutokana na uwekezaji uliofanywa kwenye eneo la elimu.

4.0 Uandikishaji wanachama kupitia Mfumo wa Usajili (Self Service Portal)

Kutokana na maboresho makubwa yaliyofanyika katika eneo la Mifumo, Ofisi ya Tabora imefanikiwa kuanza kutumia Mfumo huo kusajili wanachama wake, Mfumo huu unasaidia wananchi kujihudumia kokote walipo na kuondoa usumbufu wa kufika ofisini kwa ajili ya usajili.

Hatua hii imerahisisha na imeondoa malalamiko ya ucheleweshaji wa vitambulisho kutokana na mfumo huo kumpatia kadi ya kielektroniki inayomwezesha mwanachama kupata huduma anapokuwa kituoni.

5.0 Ulipaji wa Madai

Ofisi ya Tabora imefanikiwa kupunguza muda wa ulipaji wa madai kutoka siku 60 hadi siku 45 hali hii imesaidia uboreshaji wa huduma na kuondoa malalamiko ya watoa huduma.

6.0 Usajili wa Vituo

Mkoa wa Tabora umekuwa na mafanikio makubwa katika eneo hili ambapo umefanikiwa kusajili vituo jumla ya 400 vinavyotumika kuhudumia wanachama wa Mfuko. Kuwepo kwa vituo hivi kunaongeza ushawishi kwa wananchi kujiunga na bima ya afya hususan kipindi hiki cha utekelezaji wa bima ya afya kwa wote.

7.0 Kusogeza huduma

Ofisi ya Mkoa wa Tabora, imefanikiwa kufungua Ofisi katika Mji wa Nzega ili kuongeza ufanisi katika kuwafikia wananchi na kuwasajili na bima ya afya.

8.0 Mahusiano na wadau

Ofisi ya Mkoa imefanikiwa kuimarisha mahusiano na wadau wake hali inayowezesha kuwepo kwa ushirikiano mkubwa kati ya Mfuko na Uongozi wa Serikali ya Mkoa. Ushirikiano huu umeongeza tija katika utendaji kazi hususan katika kuwafikia wananchi na kuwahamasisha kujiunga na bima ya afya.

IRINGA

- Yatekeleza Bima ya Afya kwa Wote
- Yahudumia wanachama zaidi ya Elfu 67

Bi. Agness Chaki
Meneja wa Mkoa

Mkoa wa Iringa ni miongoni mwa mikoa inayotegemea sana kilimo na ufugaji kama uti wa mgongo wa uchumi wake. Mazao yanayolimwa kwa wingi ni pamoja na chai, parachichi, miti ya mbao, mpunga, mahindi, alizeti, vitunguu na nyanya. Aidha, sekta ya ufugaji inastawi kwa mifugo kama ng'ombe, ngamia na mbuzi, ikifuatiwa na shughuli za uvunaji wa miti kwa mbao, biashara na utalii husussan Hifadhi ya Taifa ya Ruaha.

Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya unayo Ofisi yake katika Mkoa wa Iringa ambayo inawahudumia wananchi kwa kuwapa elimu, kuwahamasisha, kuwasajili na kuwahudumia wanachama wake.

Katika kipindi cha Miaka minne, Mkoa wa Iringa umefanikiwa katika maeneo mbalimbali ambayo yameboresha upatikanaji wa huduma kwa wanachama na wananchi kwa ujumla.

1.0 Yahudumia zaidi ya wanachama elfu 67
Ofisi ya NHIF Iringa imefanikiwa katika eneo la kuongeza wigo wa wanachama kutokana na uwepo wa vifurushi mbalimbali vinavyowawezesha wananchi kuchagua na kujiunga na kunufaika na huduma za matibabu. Uhamasishaji wa wananchi umesaidia kuamsha ari ya wananchi kujiunga na bima ya afya. Hadi sasa, Mkoa una jumla ya wanachama 67,189 ambao wamejumuishwa katika makundi ya Watumishi wa Umma, Sekta rasmi, wanafunzi na sekta isiyo rasmi.

Mkoa wa Iringa umeandika historia katika kipindi cha miaka minne iliyopita kupitia utekelezaji wa Mpango wa Bima ya Afya kwa Wote. Kupitia jitihada za Serikali kwa kushirikiana na wadau mbalimbali, wananchi wa Iringa sasa wanafurahia huduma bora za matibabu zinazopatikana kwa urahisi na kwa gharama nafuu.

2.0 Ongezeko la Vituo vya Huduma vya Bima ya Afya
Mkoa wa Iringa unajivunia kuwa na jumla ya vituo 285 vya kutolea huduma vinavyohudumia wanachama wake na vituo hivi vimejumuisha Vituo vya Serikali, Binafsi na Mashirika ya Dini.

Uwepo wa vituo hivi unawapa wigo mpana wanachama wa kupata huduma kutoka kwenye vituo mbalimbali lakini unachangia kuvutia wananchi wengine kujiunga na bima ya afya.

3.0 Malipo kwa Watoa Huduma
Katika kipindi cha miaka minne, jumla ya Tsh 26.4 Bilioni zimelipwa kwa watoa huduma kwa wakati ambapo fedha hizi zimeendelea kuimarisha na kuboresha upatikanaji wa huduma za matibabu. Aidha Watoa huduma mkoani Iringa kwa sasa wanalipwa madai yao kati ya siku 30 hadi 45 ikilinganishwa na awali siku 60.

4.0 Mikopo ya Vifaa Tiba na Ukarabati
Mfuko umekuwa mstari wa mbele kuhakikisha unashiriki katika uboreshaji wa huduma za matibabu kupitia mpango wa Mikopo nafuu ya ukarabati wa miundombinu, vifaa tiba, dawa na TEHAMA. Kutokana na hili Hospitali ya Mji Mafinga imeboresha huduma za mama na mtoto pamoja na kujenga wodi za kulaza wagonjwa binafsi na Hospitali ya Ilula imeboresha huduma za uchunguzi kwa ununuzi wa Ultra Sound Machine, hatua iliyopunguza changamoto kwa akina mama wajawazito.

5.0 Bima ya Afya kwa Wote
Mkoa umejikita katika kutoa elimu kwa wananchi kupitia redio za kijamii na mikutano ya hadhara. Hatua hii imeongeza usajili, hususan kwa kundi la wanafunzi wa vyuo vikuu na vya kati. Takribani wanafunzi 13,000 wanasajiliwa kila mwaka, jambo linaloongeza wigo wa wanachama.

6.0 Mahusiano na Wadau
Ofisi ya Mkoa wa Iringa imeendelea na uimarishaji wa mahusino na Serikali ya Mkoa, Halmashauri, watoa huduma na waajiri. Mahusiano haya yanarahisha utendaji kazi na kuondoa malalamiko.

Matibabu ni gharama kubwa mno. Tusipochangia, huduma zitarudi nyuma. Tulipofika hapa, ili tuweze kutoa huduma endelevu; Suala la bima ya afya haliepukiki. Tujipange kila mmoja kuwa na bima yake ili tutibiwe ipasavyo'.

10 Januari, 2024

Bw. Evans Nyangasi
Meneja wa Mkoa

TANGA

- Yaleta mapinduzi ya huduma za afya
- Bima ya Afya kwa Wote yaleta matumaini mapya kwa wananchi

Mkoa wa Tanga ina wilaya 8 za utawala ikiwa na Halmashauri ya jiji (1), Halmashauri ya mji (2) na Halmashauri ya wilaya (8) Ikiwa na jumla ya idadi ya watu 2,615,597. Shughuli za kiuchumi ni pamoja na kilimo cha mazao, ufugaji, uvuvi, madini, viwanda (wakubwa, wa kati na wadogo), na ujasiriamali wa kiuchumi ambapo takribani asilimia 80% ya wananchi wanajihusisha na kilimo na Takriban 5% ya watu wanaoishi kwenye fukwe za Bahari ya Hindi wanajishughulisha zaidi na uvuvi.

Hata hivyo, hakuna maendeleo endelevu bila afya bora na kwa kuzingatia hili, Serikali kupitia uongozi wa Awamu ya Sita imewekeza nguvu kubwa katika sekta ya afya kwa lengo la kusogeza huduma bora karibu na wananchi na kufanikisha ajenda ya Bima ya Afya kwa Wote.

Katika kipindi cha miaka minne (2021–2025), Mkoa wa Tanga umeandika historia kupitia mageuzi makubwa kwenye sekta ya afya. Hatua hizi zimewezesha wananchi wengi kupata huduma bora bila kulazimika kusafiri umbali mrefu, jambo ambalo hapo awali lilikuwa changamoto kubwa kwa familia zenye kipato cha chini.

Mafanikio haya ni matokeo ya utekelezaji wa sera thabiti, uwekezaji katika miundombinu, vifaa tiba na kuongezeka kwa uelewa wa wananchi kuhusu umuhimu wa bima ya afya.

1.0 Mafanikio Makubwa Yaliyopatikana Ongezeko la Wanachama wa Bima ya Afya

Kiwango cha usajili wa wanachama wa Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya (NHIF) mkoani Tanga kimeongezeka kutoka wanachama 8,842 mwaka 2021 hadi kufikia wanachama 10,745 kufikia Juni, 2025. Hii ni ishara tosha ya kuongezeka kwa uelewa wa wananchi kuhusu faida za bima ya afya na jitihada za serikali katika kusogeza huduma karibu.

2.0 Huduma za Kibingwa Sasa Ndani ya Mkoa

Miaka ya nyuma, wananchi wengi wa Tanga walilazimika kusafiri mikoa ya jirani kama Kilimanjaro na Dar es Salaam kufuata huduma za kibingwa kwa sababu huduma hizo hazikuwepo. Leo hii, hali imebadilika kabisa.

Huduma za CT-Scan na MRI sasa zinapatikana ndani ya Mkoa, hatua iliyopunguza gharama kwa wananchi na kuokoa muda wao. Maboresho haya yameongeza imani ya wananchi kwa mfumo wa bima ya afya.

3.0 Huduma za Figo na Kusafisha Damu (Dialysis)

Huduma ya Dialysis sasa inapatikana katika vituo viwili vikubwa mkoani Tanga, ambapo zaidi ya wagonjwa 19 wanaweza kuhudumiwa kwa wakati mmoja kwa kila session. Hii ni hatua kubwa katika kupunguza mateso ya wagonjwa wa figo ambao zamani walihangaika kutafuta huduma hii katika mikoa ya mbali.

4.0 Mikopo kwa Ajili ya Vifaa Tiba na Maboresho ya Hospitali

Ili kuboresha huduma, Mfuko wa Bima ya Afya umetoa mikopo yenye thamani ya zaidi ya TZS 393 milioni kwa

vituo vinne vya kutolea huduma mkoani Tanga.

Miongoni mwa vituo vilivyonufaika ni Hospitali ya Mkoa wa Tanga, ambayo ilipokea mkopo wa TZS 213 milioni kwa ajili ya kuboresha jengo la upasuaji na kununua vifaa muhimu kama: Vitanda vya upasuaji, Monitor za wagonjwa, Mitungi ya gesi ya oksijeni, Mashine ya anesthesia

Hatua hizi zimeboresha huduma kwa wagonjwa wanaohitaji upasuaji na huduma za dharura.

5.0 Kuongezeka kwa Idadi ya Vituo vya Huduma

Ofisi ya Mkoa wa Tanga imefanikiwa kuongeza vituo vya kutolea huduma, kutoka vituo 245 mwaka 2021 hadi vituo 474 kufikia Juni, 2025, sawa na ongezeko la 48%.

Hii inamaanisha huduma ziko karibu zaidi na wananchi, na kupunguza malalamiko kuhusu ukosefu wa huduma. Wananchi sasa hawalazimiki tena kusafiri umbali mrefu kufuata matibabu.

6.0 Malipo kwa Watoa Huduma – Kasi Imeongezeka, Makato Yamepungua

Katika kipindi cha 2021 hadi Juni 2025, jumla ya TZS 57,050,400,216.49 zimelipwa kwa vituo vyote 474 vilivyosajiliwa na Mfuko ndani ya siku 52, ikilinganishwa na siku 75 mwaka 2021.

Makato pia yamepungua kutoka 8% mwaka 2021 hadi 3% mwaka 2025, jambo linaloongeza uaminifu wa watoa huduma kwa Mfuko.

Uhamasishaji wa Bima ya Afya – Ajenda ya Kitaifa

Ofisi ya NHIF Mkoa wa Tanga inaendelea kutoa elimu kwa wananchi kuhusu umuhimu wa kuwa na bima ya afya kupitia:

(i) Vyombo vya habari (Radio za kijamii na matangazo)
(ii) Mikutano ya kijamii na ya kidini
(iii) Ushirikiano na viongozi wa Serikali, chama tawala, vyama vya siasa, viongozi wa dini na wadau wa afya.

Lengo kuu ni kuhakikisha kila mwananchi anakuwa na bima ya afya ili kutimiza ndoto ya Serikali ya wananchi wote kutibiwa kupitia mfumo wa bima ya afya.

7.0 Ushiriki wa michezo katika kupambana na NCDs

Katika kupambana na magonjwa yasiyoambukiza, Mfuko kupitia Ofisi ya Tanga ulifanikiwa kushiriki katika michezo mbalimbali ikiwemo ya SHIMIWI ambayo pia ilitumika kuhamasisha Bima ya Afya kwa Wote.

8.0 Wito kwa wananchi

Kwa niaba ya watumishi wa Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya Mkoa wa Tanga, tunatoa shukrani za dhati kwa Uongozi wa Mkoa wa Tanga kwa ushirikiano na mazingira mazuri yaliyowezesha mafanikio haya. Ushirikiano huu umekuwa chachu ya maendeleo na msingi imara wa kuifanya bima ya afya kuwa ajenda ya kitaifa kwa manufaa ya Watanzania wote.

Bw. Ally Mwakababu
Meneja wa Mkoa

KATAVI

SAFARI YA MAFANIKIO NA MIKAKATI YA KUIMARISHA HUDUMA

Ofisi ya Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya (NHIF) mkoani Katavi imekuwa chachu ya maendeleo makubwa katika upatikanaji wa huduma za afya bora kwa wananchi. Kupitia jitihada za pamoja kati ya Serikali, wadau wa afya na NHIF, mkoa huu sasa unajivunia mafanikio makubwa ambayo yamebadilisha sura ya huduma za afya na kuongeza imani kwa wananchi kujiunga na bima ya afya.

Serikali ya Awamu ya Sita katika kipindi cha miaka minne, imefanya mapinduzi makubwa ya kihuduma hususan za afya mkoani Katavi. Mafanikio yaliyopo ni pamoja na uwepo wa Hospitali ya Rufaa ya Mkoa (KRRH Hospital) ambayo imekuwa nguzo kuu ya utoaji wa huduma za afya za kibingwa mkoani Katavi. Wananchi sasa wanapata huduma karibu bila kulazimika kusafiri umbali mrefu.

Uwepo wa Hospitali hii umeongeza Imani kubwa kwa wanachama wa Mfuko kwa kuwa wanapata huduma wanazozihitaji bila kikwazo cha fedha au umbali.

Aidha uwepo wa Zahanati na Vituo vya Afya Katika Halmashauri Zote imepanua wigo wa huduma za afya na kupunguza changamoto za upatikanaji wa huduma kwa wakazi wa maeneo ya vijijini.

1.0 Huduma za kibingwa

Uwekezaji mkubwa uliofanyika katika eneo la vifaa tiba limewezesha upatikanaji wa huduma za kibingwa kwa wanachama wa NHIF mkoani hapo na kuwaondolea usumbufu wa kufuata huduma hizo umbali mrefu. Mfano Huduma ya CT Scan na huduma ya kusafisha damu ilianza kutolewa mkoani Katavi, ikipunguza gharama na muda wa usafiri kwa wagonjwa waliokuwa wakilazimika kwenda Mbeya, Mwanza au Dodoma kupata huduma hii.

Mafanikio mengine ni Mfuko kufanikiwa kusajili Vituo vipya vya kutolea huduma kutoka vituo 100 hadi kufikia vituo 135 katika kipindi cha miaka minne. Kwa upande wa wanachama kumekuwa na ongezeko kutoka wanachama 5,000 hadi wanachama 8,250 haya ni mafanikio makubwa kutokana na mazingira halisi ya mkoa huo.

2.0 Mikakati ya Kuendelea Kuimarisha Huduma

Ofisi ya Mkoa wa Katavi inayo mikakati mbalimbali katika utekelezaji wa bima ya afya kwa wote. Mikakati hiyo ni pamoja na kuongeza wigo wa elimu kupitia radio za kijamii, mikutano ya wadau, na kampeni za moja kwa moja kwa wananchi.

Mkakati mwingine ni kuongeza Wigo wa Wanachama kwa kuendelea kushirikiana na taasisi za dini, vyama vya ushirika, na vikundi vya kijamii ili kuongeza ushiriki. Pamoja na kuboresha Huduma kwa kushirikiana na watoa huduma kuhakikisha madai yanalipwa kwa wakati na kupunguza changamoto za kiufundi.

Bw. Jeremiah Chaki
Kaimu Meneja wa Mkoa

RUKWA

NHIF RUKWA YACHOCHEA UKUAJI BIMA YA AFYA

- **Upatikanaji huduma waongezeka**

Mkoa wa Rukwa una jumla ya wakazi 1,540,519 kwa mujibu wa sensa ya mwaka 2022. Shughuli kuu za kiuchumi zinazofanyika mkoani ni pamoja na kilimo ambachi ni uti wa mgongo wa uchumi wa mkoa. Mazao ya chakula na biashara yanayolimwa ni pamoja na mahindi, maharagwe, mpunga, na alizeti.

Shughuli nyingine ni Ufugaji: Ufugaji wa wanyama mbalimbali umeendelea kuwa sehemu ya kipato na lishe kwa kaya nyingi na Uvuvi kupitia Ziwa Tanganyika, una Ziwa Rukwa na mabwawa madogo ambayo hutumika kwa uvuvi wa asili kwa ajili ya biashara na chakula.

Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya (NHIF) unayo Ofisi yake katika Mkoa wa Rukwa ambayo inahudumia wananchi wa Mkoa huo. Katika kipindi cha miaka minne ya Uongozi wa Serikali ya Awamu ya Nne, Ofisi ya Rukwa imerekodi mafanikio mbalimbali yakiwemo;-

1.0 Ongezeko la Wanachama

Hadi kufikia Juni 2025, Mkoa wa Rukwa umeongeza idadi ya wanachama hadi kufikia jumla ya wanachama 19,055 ambapo wanachama 13,318 ni kutoka taasisi za umma zinazohudumiwa moja kwa moja na ofisi ya mkoa na wanachama 5,737 ni kutoka sekta binafsi na sekta isiyo rasmi wanaonufaika na huduma za bima katika vituo mbalimbali vya kutolea huduma za afya.

2.0 Vituo vya Kutolea Huduma

Mkoa wa Rukwa umefanikiwa kusajili jumla ya vituo 247 vinavyotumika kutoa huduma kwa wanachama wa Mfuko ambapo 225 ni vituo vya Serikali, 17 ni vituo vya asasi za kidini na 5 ni vituo vya binafsi.

3.0 Malipo kwa Watoa Huduma

Kwa kipindi cha miaka minne, Mkoa wa Rukwa kwa kushirikiana na Mkoa jirani wa Katavi, umefanya malipo ya jumla ya Tsh. 15,157,542,528.40 kwa Watoa huduma zinazotokana na huduma za matibabu waliyopata wanufaika.

Mafanikio katika hili, Ofisi imeweza kulipa madai hayo kwa wakati ikilinganishwa na awali ambapo malipo yalichelewa kulipwa na kusababisha malalamiko kwa Watoa huduma. Kwa sasa malipo yanalipwa chini ya muda wa siku 45 nje ya siku 60 zilizoko kwenye mkataba wa huduma.

4.0 Mahusiano na Wadau

Mkoa wa Rukwa unajivunia mahusiano bora na wadau mbalimbali wakiwemo Watoa huduma wa Serikali na binafsi, Waajiri, Taasisi za kidini, Viongozi wa chama na serikali, Wananchi na wanachama wa NHIF.

5.0 Wito kwa Wananchi

Ofisi ya NHIF Mkoa wa Rukwa inatoa wito kwa wananchi wake kujipatia bima ya afya kabla ya kuugua, kwa kuwa huduma hii ina wigo mpana wa matibabu na gharama nafuu. Bima ya Afya ni njia ya uhakika ya kupata huduma bora katika vituo vyote vilivyosajiliwa nchini, sambamba na kutimiza azma ya serikali ya kuhakikisha kila mwananchi anakuwa na bima ya afya.

Dkt. Salum Mohamed
Kaimu Meneja wa Mkoa

TEMEKE

- **Ongezeko la wanachama lapaa kwa 75%**

Mkoa wa Temeke ni kitovu kikuu cha viwanda katika jiji ya Dar es Salaam hasa maeneo ya kurasini, pia wananchi katika manispaa hiyo wanajihusisha na shughuli za biashara ndogo ndogo, ujasiriamali, shughuli za viwanda, bandari na usafirishaji (logistics), pamoja na uvuvi.

NHIF Temeke imekuwa na jitihada mbalimbali katika kuhakikisha wananchi wanakuwa na uelewa mkubwa wa dhana ya Bima ya Afya, wajiunge na huduma na kuwa na uhakika wa kupata huduma za matibabu wakati wowote.

Katika kipindi cha miaka minne ya Uongozi wa Serikali ya Awamu ya Sita chini ya Mhe. Samia Suluhu Hassan mafanikio yamepatikana katika maeneo mbalimbali kama ifuatavyo;-

1.0 Usajili wa Wanachama

Wanachama wameongezeka kutoka 28,451 mwaka 2020/2021 hadi 37,908 mwaka 2024/2025. Ongezeko hili limetokana na kuongezeka kwa uelewa kwa wananchi kuhusu dhana ya bima ya afya.

2.0 Maboresho ya Mifumo

Mafanikio ya maboresho ya mifumo yamesaidia kwa kiasi kikubwa kuondoa usumbufu kwa wananchi wa kufuata huduma katika Ofisi za NHIF, Wanachama kwa sasa wanapata huduma haraka kwa kujisajili wao wenyewe kupitia mtandao unaowezesha kupata kadi za matibabu kwa uharaka zaidi. Awali usajili wa wanachama ulikuwa na changamoto nyingi kutokana na ucheleweshaji uliosababishwa na uhakiki wa nyaraka za kujiunga. Kwa sasa Mfumo unawezesha uhakiki wa nyaraka kutoka kwenye mamlaka husika.

3.0 Usajili wa Wanafunzi

Katika kipindi hiki cha miaka minne, kupitia maelekezo ya Serikali, Wanafunzi kwa sasa wanasajiliwa na Bima ya Afya wakati wa kujiunga na masomo hatua inayowahakikishia kupata huduma za matibabu wakati wowote wanapokuwa masomoni.

4.0 Utambuzi wa wanachama vituoni

Mfumo wa utambuzi wa wanachama umesaidia kuondoa malalamiko ya ucheleweshaji wa kupata huduma wanapokuwa kwenye vituo vya kutolea huduma.

5.0 Mahusiano na Wadau

Ofisi ya Mkoa imefanya jitihada za kuhakikisha inaboresha mahusiano yake na wadau, kwa kipindi husika mahusiano yameboreka kwa kiasi kikubwa. Ofisi inashikirikiana kwa kiwango kikubwa na Uongozi wa Serikali, Watoa huduma, wanachama na wananchi kwa ujumla.

Kwa kipindi cha miaka minne iliyopita, Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya umetekeleza mageuzi na maboresho makubwa ambayo yamechangia kwa kiasi kikubwa kuimarisha mfumo wa afya nchini. Mafanikio haya yamejikita katika kuongeza upatikanaji wa huduma bora za afya, kuimarisha usajili wa wanachama, kuanzisha mifumo ya kidigitali inayorahisisha huduma, pamoja na

Dkt. Edwin Chitage
Kaimu Meneja wa Mkoa

MTWARA

Wigo wa wanachama waongezeka

- Fursa kilimo cha korosho yatumika
- Huduma za kibingwa zapatikana

Mkoa wa Mtwara unategemea kwa kiasi kikubwa kilimo kama chanzo kikuu cha uchumi, ambapo zaidi ya asilimia 80 ya wakazi wake ni wakulima. Zao kuu la biashara ni korosho, ambalo linachukuliwa kama uti wa mgongo wa uchumi wa mkoa. Zao hili linafuatiwa na zao la ufuta, choroko na mbaazi.

Kutokana na hali hii ya kiuchumi, Ofisi ya NHIF Mkoa wa Mtwara imeweka mkakati wa kuimarisha usajili wa wanachama kwa kulenga maeneo yenye wakulima wa korosho, ikitambua umuhimu wa kuwahakikishia wananchi huduma bora za afya kupitia bima.

Katika kipindi hiki cha miaka minne ya Uongozi wa Serikali ya Awamu ya Sita, Ofisi ya Mkoa wa Mtwara, imekuwa na mafanikio mbalimbali hasa kukuza uelewa wa wananchi kuhusu dhana ya bima ya afya ambayo imechochea kwa kiwango kikubwa kuwepo kwa ongezeko la wanachama.

1.0 Wigo wa Wanachama

Katika kipindi cha miaka minne (4) kuanzia mwaka wa fedha Ofisi ya NHIF Mkoa wa Mtwara imefanikiwa kusajili jumla ya wanachama 30,755 kupitia makundi mbalimbali ya Watumishi wa Umma, Watumishi wasio wa Umma, Wanafunzi, Vifurushi Afya, Ushirika Afya na Toto Afya.

Idadi hii imeongezeka kutoka wanachama 6,851 mwaka 2020/2021, jambo linaloonyesha mwamko mkubwa wa wananchi katika kujiunga na huduma za bima ya afya.

2.0 Mahusiano Katika Ngazi ya Mkoa

Ili kuimarisha mshikamano na mahusiano bora, Ofisi ya NHIF Mkoa wa Mtwara imeendelea kushirikiana na wadau mbalimbali katika shughuli na mikutano ya mkoa. Baadhi ya shughuli hizo ni Sherehe za Mwenge wa Uhuru, Maadhimisho ya Siku ya Wakulima (Nane Nane), Sikukuu ya Wafanyakazi (Mei Mosi), Maadhimisho ya kumbukumbu ya Rais wa Tatu, Ndugu Benjamin Mkapa, Ufunguzi wa Hospitali ya Rufaa ya Kanda ya Kusini (SZRH), Mikutano ya kamati za ushauri za wilaya na mkoa (RCC).

3.0 Wito kwa Wakazi wa Mkoa wa Mtwara

Ofisi ya NHIF Mkoa wa Mtwara inaendelea kutoa hamasa na elimu ya bima ya afya kwa wananchi kupitia kampeni mbalimbali, ikiwemo kuhamasisha makundi yasiyo rasmi kujiunga na huduma za NHIF. Kupitia juhudi hizi, wananchi wameendelea kujiunga kupitia vifurushi vilivyopo, mpango wa wanafunzi na makundi mengine.

Dhamira kubwa ya Ofisi ya NHIF Mkoa wa Mtwara kuhakikisha kila mwananchi anapata huduma bora za afya kupitia mfumo wa bima ya afya unaomwezesha kunufaika na huduma za matibabu bila kikwazo chochote cha fedha.

Dkt. Aifena Mramba
Meneja wa Mkoa

ILALA

ILALA KINARA WA HUDUMA ZA KIBINGWA NA KIBINGWA BOBEZI

Yalipa Watoa Huduma zaidi ya Bilioni 686.5

NHIF ILALA

Ofisi ya NHIF Mkoa wa Ilala ni Ofisi iliyopo katika jiji la kibiashara la Dar Es Salaam. Ofisi hii inasimamia eneo la Ilala lenye idadi ya watu 1,649,912 kulingana na Sensa ya Watu na Makazi ya mwaka 2022 Census, ambapo kasi ya ukuaji ni 5.6%.

Kiutawala, Ofisi hii inasimamia Tarafa 3 - Ilala, Ukonga na Kariakoo, Kata 36, Mitaa -159. Kisiasa inasimamia Majimbo manne ya uchaguzi yaani Ilala, Segerea, Ukonga na Kivule.

Kiutekelezaji wa shughuli za Mfuko, Vituo vya huduma za afya vilivyo chini ya usimamizi wa Ofisi hii ni 170 kama vilivyochanganuliwa chini kwenye jedwali kulingana na umiiki.

SERIKALI	BINAFSI	MADHEHEBU YA DINI
58	96	16
34.1%	56.5%	9.4%

Aidha, kati ya vituo hivi Hospitali za Taifa na Maalum ni tano (5).

Eneo linalosimamiwa na Ofisi ya Ilala lina jumla ya Waajiri 1,326 (ambapo waajiri 449 wamesajiliwa) na Vyuo 31, ambapo vyuo vikuu ni 8 (vyote vimesajiliwa) na vyuo vya kati ni 23 (5 vimesajiliwa). Aidha eneo lina jumla ya shule 848, ambapo za msingi ni 524 na sekondari ni 324

1.0 Shughuli za Kiuchumi za Mkoa wa Ilala
Mkoa huu umezungukwa na shughuli mbalimbali za kiuchumi zinazochangia pato la mkoa na nchi kwa ujumla. Eneo la Ilala ni eneo muhimu la jiji la Dar es Salaam kiuchumi, shughuli hizo ni kama:

1.1 Biashara
Ofisi ya NHIF mkoa wa Ilala ipo katika kitovu kikuu cha biashara nchini Tanzania ambako kuna Masoko makubwa kama Soko la Kimataifa la Kariakoo, Buguruni, na Ilala Boma ambayo hutoa huduma za biashara ya rejareja na jumla. Biashara za bidhaa za kilimo, viwandani, na bidhaa za kutoka nje ya nchi na usafirishaji wa bidhaa kwenda mikoa mingine na nchi jirani. Fursa hii ya biashara imesaidia Mfuko kusajili wanachama wa vifurushi kulingana na uwezo na hali ya maisha ya wafanyabiashara hawa.

1.2 Sekta ya Usafirishaji na Usafiri.
Ofisi ya NHIF mkoa wa Ilala imezingirwa na vituo muhimu vya usafirishaji kama Stesheni ya reli ya TRL(Reli ya Kati na SGR), Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Julius Nyerere (JNIA), Bandari kavu pamoja na Mabasi yaendayo mikoani na huduma za daladala hizi zote zinachangia ajira katika sekta rasmi na isiyo rasmi na uchumi wa eneo hili. Ofisi imeweza kusajili watumishi wa taasisi za umma kama TRC, TAA, TCAA, TASAC, LATRA, AIR Tanzania pamoja na makampuni binafsi makubwa kama Swissport, YAPI MERKEZI, CELEBI AVIATION, Simba Logistics and Simba Supplies, Prime Regional, SUHARA Transport, Makampuni ya AZAM na wanafunzi kutoka chuo cha ndege.

1.3 Sekta ya Viwanda
Ofisi ya NHIF mkoa wa Ilala ipo kwenye eneo lenye viwanda vya aina mbalimbali vya kuchakata mazao ya kilimo na kutengeneza bidhaa kama plastiki, vinywaji, nguo, mifuko, madawa na saruji. Maeneo kama eneo la viwanda Vingunguti, Kipawa na Buguruni yana viwanda vingi vya kati na vidogo. Mfano, SSB, Zenufa, Phillips Pharmaceticals, Pristine Manufacturing, KAMAKA

1.4 Kilimo na Ufugaji
Ingawa Ilala ni sehemu ya mji, Ofisi ya NHIF Ilala bado ipo katika eneo la shughuli za kilimo pembezoni mwa mkoa kama Ukonga, Chanika, na Pugu. Kama vile Kilimo cha mboga mboga, matunda, na mazao ya chakula; Ufugaji wa kuku, mbuzi, ng'ombe na samaki. Ofisi imeweza kusajili kampuni za Farmbase, PestGuard pia imeweza kusajili vifurushi kupitia utaratibu uliopo.

1.5 Huduma za Kifedha
Ofisi ya NHIF mkoa wa Ilala imezungukwa na Benki nyingi na Taasisi za kifedha. Ofisi ya Ilala imeweza kusajili Benki Kuu ya Tanzania, Exim, Absa, Baroda, NMB, CRDB, NBC, vyama vya ushirika, Rafiki Forex Bureau n.k.

1.6 Utalii wa Miji, Urithi na Hoteli.
Ofisi ya NHIF mkoa wa Ilala ipo katika maeneo ya kihistoria kama Mnara wa Saa wa Ilala, makanisa ya zamani, na makaburi ya mashujaa ni vivutio vya ndani. Aidha, kuna hoteli na migahawa mingi maarufu ambayo tumeweza kusajili na kuwapatia bima, kama Hyatt Regency, Johari Rotana, Four Seasons, Holiday Inn, Serena.

1.7 Ajira katika Sekta ya Umma na Binafsi
Ofisi ya NHIF mkoa wa Ilala ipo katika makao makuu ya ofisi nyingi za serikali, mashirika ya umma, taasisi za elimu, afya, na mashirika binafsi na hii huchangia ajira na matumizi ya bidhaa/huduma ndani ya mkoa kama vile TRA, NSSF, TPDC

1.8 Sekta ya Elimu
Ofisi ya NHIF mkoa wa Ilala imezungukwa na vyuo vikuu na vya kati ambapo Ofisi ya Mfuko imetumia nafasi hiyo kusajili wanafunzi wengi kila mwaka. Ofisi imesajili vyuo kama CBE, MUHAS, IFM, DIT, KIU, DMI, TPSC

2.0 Usajili wa wanachama
Ofisi ya NHIF Ilala kutokana na kuzungukwa na idadi kubwa ya wananchi, imefanikiwa kuwa na ongezeko kubwa la wanachama ambapo mpaka sasa inahudumia jumla ya wanachama 300,919 kwa mchanganuo ufuatao;-

Taasisi za Umma	Taasisi Binafsi	Sekta isiyo rasmi
190,638	75,025	35,256

3.0 Hali ya Mahusiano ya Mfuko na Wadau wa Mkoa
Ofisi ya Mkoa wa Ilala umekuwa na uhusiano mzuri na wadau wake kiserikali, kijamii, na wananchi kwa ujumla.

3.1 Mahusiano na Vituo vya Kutolea Huduma za Afya
Ofisi ya Ilala ina uhusiano wa moja kwa moja na hospitali, vituo vya afya, na zahanati za serikali na binafsi ndani ya Mkoa wa Ilala; Ofisi inajihusisha na ukaguzi wa mara kwa mara wa ubora wa huduma na ufuatiliaji wa mwenendo wa matumizi ya huduma za Mfuko. Vilevile, kuhakikisha uwazi katika michakato ya malipo, uandikishaji na utoaji wa huduma.

3.2 Mahusiano na Serikali za Mitaa
Ofisi ya Ilala hushirikiana na halmashauri ya Manispaa ya Ilala, ofisi za kata, na mitaa katika kutoa elimu kuhusu umuhimu wa bima ya afya. Maafisa wa ofisi hizi pamoja na viongozi wa kata husaidia kufanikisha kampeni za usajili, maeneo yote, hasa pembezoni mwa jiji kama Chanika, Ukonga, na Pugu.

3.3 Mahusiano na Waajiri/Watumishi
Ofisi ya Ilala hushirikiana na waajiri katika sekta ya umma na binafsi ili kuhakikisha watumishi wanasajiliwa na wanapata huduma ipasavyo kupitia semina na mafunzo ya mara kwa mara kwa wadau. Hasa katika kipindi cha ukaguzi, usajili, makongamano, mabaraza ya wafanyakazi na warsha mbalimbali.

3.4 Mahusiano na Taasisi za Elimu na Dini
Ofisi ya Ilala hufanya kampeni za kuhamasisha wanachama wapya haswa katika taasisi za elimu (shule na vyuo). Mbinu zinazotumika ni kufanya vikao na uongozi, mikutano na wazazi na wanafunzi, na kuweka makambi katika taasisi hizi hasa kipindi cha usajili wa wanafunzi wapya.

3.5 Kijamii kwa ujumla
Ofisi ya Ilala imekuwa ikihudhuria matamasha, maadhimisho na maonesho yanayojitokeza katika maeneo mbalimbali ya mkoa ili kuhakikisha jamii yote imefikiwa. Pamoja na hayo, kuendelea kutoa elimu kuhusu upatikanaji wa haraka wa huduma za Bima ya Afya kama vile uwepo wa vituo vya msaada wa wateja kama Call Center na One Stop Center na uwepo wa huduma za kimtandao (Self Service) ili Kuongeza matumizi ya teknolojia ya kidijitali katika usajili na upatikanaji wa huduma.

Aidha, Ofisi imejiwekea utaratibu wa kuwa na makundi sogozi na wadau wote muhimu na mahsusi, ili kufikisha kwa karibu huduma kwa wadau. Makundi haya yanasaidia kupokea kwa haraka na kufanyia kazi changamoto wanazokutana nazo kwa wakati.

4.0 Wito kwa Wakazi wa Eneo Linalosimamiwa na Mkoa

Ofisi ya Mfuko inatoa wito kwa wakazi wote wa maeneo yote yanayosimamiwa na mkoa wa Ilala kujiunga na makundi mbalimbali ya uanachama wa Mfuko ikiwemo vifurushi, Toto Afya na wanafunzi. Hii itawawezesha katika yafuatayo:

(i) Upatikanaji wa huduma bora na uhakika wa matibabu wakati wote.
(ii) Kupata huduma katika hospitali, vituo vya afya na zahanati zaidi ya 9,000 nchini kote vilivyosajiliwa na NHIF na hasa ukizingatia Ofisi ya Ilala inasimamia vituo vikubwa vya kimkakati na Hospitali za Taifa za Rufaa.
(iii) Kupata matibabu bila kulazimika kutoa pesa taslimu wakati wa dharura au ugonjwa.
(iv) Ulinzi wa kipato kwa kuzingatia ukubwa wa gharama za matibabu, na namna ambavyo ugonjwa unakuja bila kutarajia.

Vilevile, kuwahimiza wadau wote wa Mfuko kuwa mabalozi wa Mfuko kwenye maeneo yao ya kazi, jamii n.k. Aidha, tunaendelea kuwamba wadau kuzingatia miongozo katika utendaji kazi na matumizi ya huduma za Mfuko.

5.0 MALIPO KWA WATOA HUDUMA (2021–2025)

5.1 Malipo
Katika kipindi cha mwaka 2021 hadi 2025, Mkoa wa Ilala umefanikiwa kufanya malipo kwa watoa huduma kama inavyooneshwa hapa chini:

Aina ya Kituo	Malipo (TZS)
Vituo vya Serikali	381,773,192,502.94
Vituo Binafsi	168,000,268,457.49
Mashirika ya Dini (FBO)	136,746,934,778.82
Jumla	**686,520,395,739.25**

5.2 Kupunguza Kiwango cha Makato (Deduction Rate)
(i) Kutoka wastani wa asilimia 15 mwaka 2021 hadi wastani wa asilimia 6 mwaka 2025.
(ii) Mwelekeo (trend) unaonesha kushuka kwa kiwango cha makato kwa kipindi chote cha utekelezaji.

5.3 Sababu za kupungua kwa kiwangoi cha makato:
Utoaji wa elimu kwa watoa huduma.
(i) Kufanya ukaguzi shirikishi.
(ii) Uhakiki wa madai na usuluhishi wa madai.
(iii) Matumizi ya mifumo ya kidijitali katika mchakato mzima wa madai.

5.4 Kupunguza Muda wa Kukaa kwa Madai (Aging of Claims)
(i) Kutoka wastani wa siku 96 mwaka 2021 hadi wastani wa siku 29 kwa sasa (mwaka 2025).
(ii) Mwelekeo (trend) unaonesha kupungua kwa muda wa madai kukaa kwenye mfumo kabla ya kulipwa.

5.5 Sababu za kupungua Muda wa kukaa kwa madai:

(i) Vituo vikubwa kuwasilisha madai kwa njia ya mtandao.
(ii) Vituo kuwezeshwa kuwasilisha madai kila siku.
(iii) Uchakataji wa madai mara kwa mara (daily processing).
(iv) Kuongezeka kwa ufanisi wa TEHAMA.

6.0 Usimamizi wa Vituo Vikubwa vya Ki

Ofisi ya Mkoa wa Ilala inasimamia vituo vya kimkakati, ikiwemo hospitali kubwa za serikali na hospitali za Taifa.Vituo hivi vinatoa huduma za kibingwa na hufanya maamuzi ya kitaalamu kwa wagonjwa wengi wanaohamishwa kutoka vituo mbalimbali nchini.Usimamizi huu umesaidia kuboresha uratibu, kudhibiti gharama na kuongeza upatikanaji wa huduma bora za matibabu.

7.0 Utoaji wa Vibali Zaidi ya Asilimia 50 Vyatolewa na Mfuko

Ofisi imefanikiwa kusimamia utoaji wa vibali vya huduma mbalimbali kwa wakati, jambo lililoleta mafanikio makubwa.Mkoa wa Ilala unachangia zaidi ya asilimia 50 ya vibali vyote vya Mfuko nchini.Hatua hii imeongeza ufanisi, kupunguza malalamiko ya wanachama, na kuhakikisha huduma zinapatikana kwa wakati.

Kufungua Mafaili ya Huduma Mbalimbali kwa wingi:

8.0 Ofisi ya Mkoa wa Ilala imefanikiwa kufungua mafile ya huduma mbalimbali kwa wanachama kulingana na mahitaji yao ya kiafya. Huduma hizo ni pamoja na:

(i) Huduma za saratani (cancer treatment).
(ii) Huduma za usafishaji damu (dialysis).
(iii) Upatikanaji wa dawa mbalimbali muhimu kwa wagonjwa wenye magonjwa sugu.

Hatua hii imechangia kupunguza muda wa wanachama kusubiri huduma, kuongeza uwazi katika uidhinishaji wa matibabu na kuimarisha ufanisi wa mfumo.

Ofisi ya Ilala katika kuhakikisha inapenyeza ajenda ya Bima ya Afya kwa Wote, imefanikiwa kushiriki katika mikutano, maadhimisho na makongamano makubwa ambapo kumekuwa na tija kubwa katika ukuzaji wa uelewa wa dhana ya Bima ya Afya.

Kusogeza huduma karibu na wadau hususan wanachama, waajiri na watoa huduma

Kuanzisha vituo vya huduma kwenye maeneo mbalimbali kama hospitali zote za Taifa na za kimkakati na hospitali nyingine kubwa

Kuweka makambi maalum kwenye maeneo ya kimkakati, ili kuwezesha utoaji wa elimu na usajili wa wanachama

kwa kuwa na mifumo mbalimbali kama makundi sogozi, vituo vya huduma kwa wateja, kuwa na namba za simu kwa ajili ya wateja kupiga n.k

Kikao cha Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya (NHIF) na Taasisi ya Tiba ya Mifupa na Upasuaji wa Mishipa ya Fahamu (MOI) jijini Dodoma.

Dkt. Mchele S. Mchele
Meneja wa NHIF- Mkoa wa Njombe

NJOMBE

MAFANIKIO YA MIAKA MINNE

Yalipa madai kwa wakati
Yahimiza wananchi kujiunga na Mfuko

Mkoa wa Njombe unatajwa kama moja ya mikoa yenye shughuli za kiuchumi zinazochangia kwa kiasi kikubwa pato la Taifa. Shughuli kuu za kiuchumi zinazofanyika ni:

Kilimo: Parachichi, viazi, na mahindi ni mazao makuu yanayolimwa kwa wingi. Parachichi kutoka Njombe limejipatia soko la kimataifa, huku viazi na mahindi yakihudumia mahitaji ya ndani na nje ya mkoa.

Misitu: Mbao na magogo ni miongoni mwa mazao yanayotokana na misitu ya mkoa huu, ambayo imekuwa chanzo kikubwa cha kipato kwa wananchi na mapato ya serikali.

Ufugaji: Ufugaji wa ng'ombe wa maziwa umeendelea kustawi, na kufanya Njombe kuwa kinara katika uzalishaji wa maziwa nchini.

Uvuvi: Uvuvi wa samaki kwenye mabwawa na maeneo ya mito umekuwa sehemu ya kujipatia kipato na kuboresha lishe ya kaya.

Ili wananchi wa Mkoa wa Njombe waweze kutekeleza majukumu yao wakiwa na uhakika wa afya zao, Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya (NHIF), unayo Ofisi mkaoni hapo kwa lengo la kuwasogea huduma wananchi hao ikiwemo kuwapa elimu, kuwahamasisha na kuwasajili.

Katika kipindi hiki cha miaka minne ya Mhe. Rais Samia Suluhu Hassan, Ofisi ya NHIF Njombe imepata mafanikio mbalimbali ambayo ni pamoja na;-

1.0 Ongezeko la Wanachama

Katika kipindi cha miaka minne (2021–2025), Ofisi ya NHIF Mkoa wa Njombe imefanikiwa kusajili jumla ya wanachama 18,206, huku ikihudumia jumla ya wanufaika 146,560 katika halmashauri zote 6 za mkoa. Hii ni hatua muhimu katika kuhakikisha wananchi wanapata huduma bora za afya kupitia bima.

2.0 Vituo vya Kutolea Huduma za Matibabu

Mkoa wa Njombe una jumla ya vituo vya kutolea huduma za matibabu 338, ambavyo vinatoa huduma kwa wanufaika wa Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya na uwepo wa vituo hivi umechangia kuongeza ari ya wananchi kujiunga na huduma za bima ya afya.

3.0 Malipo kwa Vituo vya Kutolea Huduma za Matibabu

Ili kuhakikisha huduma zinakuwa bora, Ofisi ya Njombe imefanikiwa kulipa madai yenye jumla ya Tsh. 19,773,106,044.40 kwa vituo vya kutolea huduma kwa wakati. Fedha hizi zinazolipwa vituo zinasaidia kwa kiasi kikubwa kuboresha huduma za matibabu na kuwezesha upatikanaji wa huduma kwa urahisi zaidi.

Hii ni ishara ya dhamira ya Mfuko katika kuhakikisha watoa huduma wanalipwa kwa wakati ili kuendelea kutoa huduma bora kwa wanufaika.

4.0 Ushirikiano na Wadau

Ofisi ya NHIF Mkoa wa Njombe imeendelea kudumisha mahusiano mazuri na wadau wa sekta ya afya, wakiwemo:
(i) Ofisi ya Mkuu wa Mkoa
(ii) Halmashauri zote za Mkoa
(iii) Watoa huduma wa Serikali na Binafsi
(iv) Taasisi za umma na binafsi
(v) Waajiri, viongozi wa chama na serikali katika ngazi zote

5.0 Wito kwa Wananchi wa Njombe

Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya unaendelea kutoa huduma kwa wananchi wote ili kutekeleza azma ya Serikali ya wananchi wote kuwa ndani ya bima ya afya ili wanufaike na huduma bora za matibabu.

Utekelezaji wa Sheria ya Bima ya Afya kwa Wote, ni jukumu la kila mtu kuhakikisha kila kaya na kila familia inajiunga na huduma za NHIF kwa manufaa ya afya bora na ustawi wa jamii.

Dkt. Mkwabi Fikirini
Meneja wa Mkoa

KILIMANJARO

ELIMU DHANA BIMA YA AFYA YAONGEZEKA

- **Wigo wa wanachama waongezeka**

Mkoa wa Kilimanjaro unayo Ofisi ya Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya (NHIF), katika kuhakikisha wananchi wa mkoa huo wanapata huduma za bima ya afya hususan katika kipindi hiki cha utekelezaji wa Bima ya Afya kwa Wote.

Katika kipindi cha mwaka 2021 hadi 2025, NHIF imefanikiwa kuongeza wanachama kwa kasi kubwa. Jumla ya wanachama 133,669 wamejiunga na mfuko kupitia makundi mbalimbali, hatua ambayo inaonyesha uelewa na uhitaji mkubwa wa huduma za bima ya afya nchini.

Ili kuendana na mahitaji ya kisasa na kuongeza urahisi kwa wateja, maboresho makubwa yamefanyika kwenye mfumo ni pamoja na kuwezesha wananchi kujisajili wenyewe moja kwa moja ambapo Ofisi uya NHIF Mkoa wa Kilimanjaro umejikita katika kuelimisha wananchi ili kurahisisha upatikanaji wa huduma.

1.0 Ushirikiano na sekta binafsi

Katika kipindi cha miaka minne, NHIF imeimarisha ushirikiano na sekta binafsi ili kuhakikisha wananchi wengi zaidi wanajiunga na huduma za bima ya afya, hususan katika maeneo ya ajira zisizo rasmi na biashara binafsi.

2.0 Ukusanyaji wa michango

Kuanzia mwaka 2021 hadi 2025, NHIF Kilimanjaro, imefanikiwa kukusanya jumla ya Tsh. 23,471,665,595.01 kutoka kwa wanachama wake. Ongezeko hili linathibitisha kuwepo kwa mwamko wa wananchi kujiunga.

3.0 Mikopo ya Ukarabati Majengo na Vifaa Tiba

Katika kipindi cha Awamu ya Sita, Mfuko umetoa mikopo kwa watoa huduma wake kwa lengo la kuboresha upatikanaji wa huduma katika vituo vya kutolea huduma vilivyosajiliwa na Mfuko. Katika Mkoa wa Kilimanjaro, Baadhi ya Vituo vya matibabu vilivyonufaika na mpango huo ni pamoja na Hospitali ya Rufaa ya Kanda KCMC.

4.0 Maboresho ya Mkataba wa Huduma kwa Wateja

Kuboreshwa kwa Mkataba wa Huduma kwa Wateja, kumeongeza tija na uwazi katika utendaji kazi ambao umeongeza kuridhika kwa wanachama katika kupata huduma.

5.0 Wito kwa wananchi

Katika kipindi hiki cha utekelezaji wa Bima ya Afya kwa Wote, Ofisi ya NHIF Kilimanjaro inatoa wito kwa wananchi kujiunga na Bima ya Afya ili kuwa na uhakika wa kupata huduma za matibabu bila kikwazo chochote cha fedha.

Mkurugenzi Mkuu Dkt. Irene Isaka akiwa na watumishi wa Mfuko wa Ofisi ya NHIF Kilimanjaro.

Kiwanda cha kuzalisha oksijeni kwa ajili ya matibabu KCMC

Jengo la huduma ya dharura KCMC

MOROGORO

MOROGORO YAJIKITA UTOAJI ELIMU BIMA YA AFYA

- **Wananchi wahamasika kuwa ndani ya Mfumo wa Bima ya Afya**

Mbala Shitindi
Meneja wa Mkoa

Ofisi ya Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya Mkoa wa Morogoro inahudumia wilaya saba (07) ikiwa na Halmashauri tisa (09) za Morogoro Mjini, Morogoro Vijijini, Mvomero, Kilosa, Gairo, Ifakara Mji, Mlimba Malinyi na Ulanga. Mkoa una jumla ya wananchi 3,197,104, kwa mujibu wa Sensa ya Taifa ya mwaka 2022 ukiwa na eneo lenye mita za mraba 73,039.

1.0 Shughuli za kiuchumi

Shughuli kuu za kiuchumi za mkoa ni kilimo,ufugaji, uchimbaji madini na viwanda. Asilimia 75 ya Wananchi wa Mkoa wa Morogoro wanategemea kilimo kwa ajira, kipato na chakula. Mazao ya chakula yanayozalishwa kwa wingi ni mpunga, mahindi, ndizi, viazi vitamu, muhogo, mtama na maharage. Mazao ya biashara yanayozalishwa kwa wingi ni Miwa, Ufuta, Alizeti, Mkonge, korosho, pamba, kokoa, matunda, viungo na mboga mboga.. Mkoa pia unazo shughuli za uchimbaji wa madini, yakiwemo Ruby, Spinel, Chokaa, Dhahabu ambayo uchimbaji, uchakataji na uuzaji wake unatoa ajira kwa baadhi ya wakazi wa Mkoa.

Ofisi ya Mkoa wa Morogoro umeshiriki katika shughuli mbalimbali ili kuhakikisha wananchi wanakuwa na mwamko wa kujiunga na bima ya afya ili wawe na uhakika wa kupata huduma za matibabu wakati wote. Kutokana na shughuli hizo, kumekuwa na mafanikio mbalimbali katika kipindi cha miaka minne ya uongozi wa Mhe. Samia Suluhu Hassan.

2.0 Uhamasishaji na usajili wa wanchama

Ofisi ya Mkoa imeakuwa ikifanya uhamasishaji na usajili wa wanachama katika azma ya kuwafikia wananchi wengi kujiunga na Mfuko. Mkoa umekuwa ukifanya uhamasishaji wa waajiri, mashuleni, masokoni, mitaani, katika mikusanyiko na maonesho mbalimbali. Hadi kufikia Juni 2025 mkoa ulikuwa na jumla wanachama wachangiaji (wanaowasilisha michango Ofisi ya Mkoa) 35,329. Wanachama hao wapo katika makundi ya uanachama ya Watumishi wa Umma, Makampuni Binafsi, Wanachama wa Vifurushi na Wanafunzi.

3.0 Vituo vya matibabu

Mkoa una jumla ya vituo 492 vilivyosajiliwa na Mfuko kutoa huduma kwa wanufaika wake, kati ya hivyo vituo 405 vya Serikali, binafsi 55 na vituo vya madhehebu ya dini 32. Kati Vituo hivyo vituo 4 ni Hospitali za Rufaa za Mkoa, ikiwemo Hospitali Maalum ya Saratani.

4.0 Ulipaji wa madai ya watoa huduma

Kwa kipindi cha mwaka 2021 hadi 2025 Ofisi ya Mkoa imelipa jumla Tsh 45,214,326,326.79, ikiwa malipo kwa huduma za matibabu zilizotolewa kwa wanufaika wa Mfuko. Malipo haya yamesaidia katika uboreshaji wa huduma za matibabu kwa wanachama na wananchi kwa ujumla.

5.0 Mwenendo wa makato ya madai

Katika kipiindi cha miaka minne(04) Ofisi ya mkoa kwa wastani ililipa madai kwa uwiano wa kiasi cha malipo na madai (reimbursement rate) wa asilimia 94 ikimaanisha wastani wa kiasi cha madai yaliyokataliwa kwa sababu mbalimbali za mapungufu na ukiukwaji wa miongozo (rejection rate) kuwa asiimia 6.

6.0 Muda wa kulipa madai (aging trend) 2021-2025

Katika kipindi cha miaka miaka minne (2021-25) Ofisi ya Mkoa imefanya jitihada kubwa kuhakikisha malipo ya watoa huduma yanafanyika kwa siku chache, kuelekea lengo la siku 45; kutoka mwaka 2022 hadi 2025 wastani wa siku za kulipa madai tangu kuwasilishwa (aging) zilishuka kutoka siku 64 hadi siku 59.

7.0 Hali ya mahusiano kati ya mfuko na wadau wa mkoa

Kwa kipindi cha miaka minne ya Serikali ya awamu ya sita, Ofisi ya Mfuko Mkoa wa Morogoro imeendeleza mahusiano na ushirikiano na wadau muhimu wa Mkoa ikiwemo Ofisi ya Mkuu wa Mkoa, Ofisi ya Katibu tawala wa Mkoa pamoja na wasaidizi wake wote katika Halmashauri zote za Mkoa na wadau wengine wakiwemo Waajiri na Watoa huduma. Katika kipindi hicho Ofsi imefanya vikao na wadau, kushikiri katika mialiko ya shughuli mbalimbali za wadau ikiwemo maadhimisho, maonesho na utoaji elimu. Mahusiano hayo yamekuwa msingi wa Ofisi ya Mkoa kutekeleza majukumu yake vyema.

8.0 Wito kwa wakazi wa mkoa wa Morogoro

Ofisi ya Mkoa inatoa wito kwa wakazi wa Mkoa wa Morogoro, kuwa na uhakika wa kupata huduma za matibabu katika vituo vya matibabu vilivyosajiliwa nchini kote kwa kujiunga na Mfuko kabla kuugua. Aidha Ofisi ya Mkoa wa Morogoro imefanikiwa kuendelea kusogeza huduma zake kwa kufungu Ofisi ndogo katika mji mdogo wa Ifakara.

Kuhunga Msambichaka
Meneja wa Mkoa

MARA

MARA NA MAFANIKIO YA AWAMU YA SITA

- **Yachochea upatikanaji wa huduma za matibabu**
- **Yawaomba wananchi kujiunga bima ya afya**

Mkoa wa Mara ni moja ya Mkoa ambao Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya (NHIF), umeweka Ofisi yake kwa ajili ya kutoa huduma za bima ya afya kwa wananchi mkoani hapo. Mkoa huo unaundwa na Wilaya (6) na Halmashauri (9) ambazo ni Manispaa ya Musoma, Halmashauri ya Musoma, Halmashauri ya Rorya, Halamashauri ya tarime Mjii, Halmashauri ya Tarime, Halmashauri ya Serengeti, Halmashauri ya Bunda Mjii, Halmashauri Bunda na Halmashauri ya Butiama Vijijini, RoryaKahama, Kishapu, Msalala,Ushetu, Mara Vijiji na Manispaa.

Kwa mujibu wa takwimu za Sesa ya watu na makazi ya mwaka 2022 Mkoa wa Mara una jumla ya wakazi 2,372,015 wanaojishughulisha na shughuli za kiuchumi ambazo ni uchimbaji wa madini, utalii, uvuvi, ufugaji na kilimo.

Katika kipindi hiki cha miaka minne ya Mhe. Rais Samia Suluhu Hassan, Ofisi ya Mkoa wa Mara imepata mafanikio mbalimbali ambayo yamechochea kwa kiasi kikubwa upatikanaji wa huduma za matibabu kwa wanachama na wananchi wa Mkoa wa Mara. Mafanikio hay oni pamoja na;-

Katika kipindi cha miaka minne ya Serikali ya awamu ya sita,ofsi ya Mkoa wa Mara imepata mafanikio makubwa katika maeneo kadhaa kama ifuatavyo

1.0 Ongezeko La Usajili Wa Wanachama
Katika kipindi cha miaka minne ya serikali ya Awamu ya Sita kuanzia mwaka 2021/2022 ofisi imesajili jumla ya wanachama wapya 15,812 ambapo wanafunzi ni 60%, Vifurushi ni 15%, watumishi ni 14% na Toto Afya 11%.

2.0 Usajili wa Makampuni makubwa katika Mkoa.
Ofisi ya Mkoa wa Mara imefanikiwa kuyafikia na kusajili makampuni makubwa mawili, MMG Gold

Limited na Taifa Minning and Civils Limited amabayo yako kwenye sekta ya madini. Awali makampuni haya yalipata huduma za matibabu nje ya NHIF. Kutokana na hilo, jumla ya taasisi 57 zimeweza kusajiliwa katika ofisi ya Mfuko Mkoa wa Mara.

3.0 Wigo wa Vituo Vya Kutolea Huduma
Kwa kipindi cha miaka minne ya serikali ya awamu ya sita ofisi ya Mkoa imefanikiwa kwa kisasi kikubwa kusajili vituo mbalimbali vya kutolea huduma vya serikali, binafsi na vinavyomilikiwa na taasisi za kidini. Mpaka kufikia Mwezi June 2025, Ofisi imesajili jumla ya vituo 349 vinavyotoa huduma kwa Wanachama wa Mfuko, vituo 261 vikiwa ni vya Serikali na 88 vikiwa ni vituo vya Binafsi.
Idadi ya vituo 349 ni ongezeko la vituo 84 (29.47%) zaidi ya vituo 285 vilivyokuwa vimesajiliwa na Mfuko hadi kufikia June 2021.

4.0 Malipo ya watoa huduma.
Mafanikio mengine ni pamoja na malipo ya watoa huduma kwa wakati, katika kipindi cha mwaka wa fedha 2024/2025 Ofisi ya Mkoa imelipa jumla ya Tsh 7,233,152,172.50 kwa watoa huduma ambao wamesajiliwa na Mfuko katika Mkoa wa Mara. Malipo haya yamelipwa chini ya wakati wa mkataba.

5.0 Mikopo kwa watoa huduma
Katika jitihada za Mfuko kuhakikisha kuwa wanachama wa Mfuko na wananchi wanapata huduma bora, Mfuko umefanikiwa kuchangia uboreshaji wa huduma za matibabu kwa kukopesha jumla ya Tsh 984,900,000.00 kwa vituo kuboresha huduma zake. Uboreshaji huu unasaidia vituo na wanachama/wananchi kupata huduma bora na kwa wakati.

6.0 Kuimarika kwa mahusiano kati ya Mfuko na wadau wa Mkoa
Katika kipindi cha miaka minne ya Serikali ya awamu ya sita, Ofisi ya Mfuko Mkoa wa Mara imefanikiwa kudumisha na kuboresha mahusiano mazuri iliyonayo na wadau wote wa ndani na nje ya ofisi ya Mkoa.

Mahusiano yameboreka kwa kufanya kazi kwa ukaribu na mamlaka zingine za serikali kama Ofisi ya Mkuu wa Mkoa, Katibu Tawala wa Mkoa, Ofisi za Wakuu wa Wilaya na Wakurugenzi wa Halmashauri zote za Mkoa wa Mara.

Mahusiano yameboreshwa kwa wadau wote wanaofanya kazi na ofisi ya Mkoa wakiwemo Waajiri waliosajiliwa, watoa huduma , wanachama na wananchi kwa ujumla wake.

Mahusiano hayo mazuri yamejengwa kwenye msingi wa kushirikiana katika utekelezaji wa shughuli mbalimbali za kiserikali na kijamii na taasisi zingine za serikali, zisizo za kiserikali, watoa huduma, waajiri, wanachama na wananchi wote.

Msingi wa ushirikiano umesajidia ofisi kuhudumia vizuri wadau kwa kufanyia kazi maombi, maoni na mapendekezo yao katika kuhakikisha wanaridhika na huduma zetu na kusaidia ofisi katika kutimiza majukumu yake.

7.0 Wito kwa wakazi wa Mkoa wa Mara
Katika kipindi cha miaka minne ya Serikali ya awamu ya Sita, serikali imefanya uwekezaji mkubwa kwenye miundombinu ya kutolea huduma za afya na katika maboresho ya upatikanaji wa dawa na vitendanishi ikiwemo uwepo wa vitengo vya magonjwa ya dharura katika kila Hospitali na huduma za msingi za upasuaji kwenye kila Kituo cha Afya.

Ili kunufaika na huduma hizo, wananchi wanaombwa kujiungha na bima ya afya ili kuwa na uhakika wa kupata huduma za matibabu wakati wowote bila kikwazo cha fedha.

ARUSHA

ARUSHA YAIMARIKA UPATIKANAJI HUDUMA ZA KIBINGWA

- **Wigo wa wanachama wapaa**
- **Wajivunia uwepo wa NHIF**

Hipoliti Lello
Meneja wa Mkoa

Mkoa wa Arusha ni moja ya mikoa yenye fursa mbalimbali za kiuchumi nchini Tanzania, ukiwa na wilaya 6 za kiutawala, Halmashauri ya Jiji moja na Halmashauri za Wilaya sita. Mkoa huo kwa sasa una idadi ya watu wapatao 2,593,834, ambao wanajishughulisha na shughuli mbalimbali za kiuchumi.

Shughuli kuu za kiuchumi mkoani Arusha ni kilimo ambacho kinahusisha mazao ya biashara kama kahawa, maua na mbogamboga. Aidha, ufugaji wa ng'ombe, mbuzi, kondoo, na kuku ni sehemu muhimu ya maisha ya wakazi. Utalii na maliasili hasa kutokana na vivutio kama mbuga za wanyama na madini adimu ya Tanzanite ni chanzo kikuu cha mapato na ajira kwa asilimia 40 ya wakazi wa mkoa. Pia, viwanda vya ukubwa tofauti na ujasiriamali wa kiuchumi vimeimarisha maendeleo ya mkoa.

Pamoja na uzuri wa Mkoa wa Arusha, suala la uhakika wa huduma za matibabu limelitiliwa mkazo na Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya ambao umefanikiwa na Ofisi katika mkoa huo kwa lengo la kuwasogezea wananchi huduma ya bima ya afya.

Katika kipindi cha miaka minne ya uongozi wa awamu ya sita, Mkoa wa Arusha umefanikiwa kwa kiasi kikubwa katika kuboresha huduma za afya na ustawi wa jamii. Kupitia juhudi za Serikali, maboresho makubwa yamefanyika katika miundombinu ya afya, utoaji wa huduma bora na upatikanaji wa vifaa tiba. Yafuatayo ni mafanikio muhimu katika sekta ya afya:

1.0 Kuimarika kwa Huduma za Matibabu:
Idadi ya wanachama waliosajiliwa na Mfuko wa Bima ya Afya imeongezeka kutoka 28,071 mwaka 2021 hadi 31,653 mwaka 2025. Ongezeko la vifaa na vipimo muhimu kama CT-SCAN kutoka 1 mwaka 2021 hadi 4 mwaka 2025, pamoja na huduma za MRI na maabara za patholojia vimechangia kuwa chachu ya wananchi kujiunga na huduma za NHIF.

2.0 Huduma za Kibingwa na Bingwa Bobezi:
Hospitali ya Serikali ya Mkoa wa Arusha, Mt. Meru imeimarisha huduma za matibabu katika magonjwa ya moyo, figo, macho, mifupa, meno, afya ya akili, na huduma za dharura. Aidha kumekuwepo na mafanikio ya uwepo wa huduma za kuchuja damu (dialysis) katika vituo vinne ndani ya mkoa, vinavyoweza kuhudumia wagonjwa zaidi ya 30 kwa wakati mmoja ambapo awali hazikuweza kupatikana.

3.0 Mikopo ya Kuboresha Huduma za Afya:
Katika eneo hili, Mfuko umefanikiwa kuwa sehemu ya maboresho ya huduma za matibabu kwa kutoa jumla ya

TZS 393,520,741.00 kwa ajili ya kuboresha huduma za matibabu, huku Hospitali ya Mt. Meru ikipokea TZS 213,430,741.00 kwa ajili ya vifaa tiba na jengo la upasuaji.

4.0 Kuongezeka kwa Vituo vya Huduma za Afya
Idadi ya vituo vya kutolea huduma imeongezeka kutoka 321 mwaka 2021 hadi 364 mwaka 2025, ongezeko la asilimia 12%. Hii imepunguza gharama za usafiri na muda wa kufuata huduma za afya kwa wananchi.

5.0 Malipo kwa Watoa Huduma
Ulipaji wa madai kwa Watoa huduma umeboreka ambapo kwa sasa madai yanalipwa chini ya mud awa siku 45 ikilinganishwa na awali ambapo yalilipwa ndani ya siku 60. Kutokana na hayo, jumla ya TZS 77,275,596,015.15 zimelipwa kwa vituo 364 vilivyosajiliwa na fedha hizi zimekuwa ni sehemu ya kuendelea kuimarisha huduma za matibabu mkoani Arusha.

6.0 Elimu na Uhamasishaji
Ofisi ya NHIF, Mkoa wa Arusha imeendelea kutoa elimu kwa wananchi juu ya umuhimu wa bima ya afya, huku ikiwahimiza watoa huduma kufuata miongozo ili kuboresha huduma na kuepuka malalamiko. Huduma kwa wateja zimeimarishwa kwa kurahisisha taratibu za kujiunga na kufanya malipo ya kujiunga na Mfuko.

7.0 Ushiriki wa michezo katika kupambana na NCDs
Katika kupambana na magonjwa yasiyoambukiza, Mfuko kupitia Ofisi ya Arusha ulifanikiwa kushiriki katika michezo mbalimbali ikiwemo ya mashindano ya mbio (Marathon) ambayo pia ilitumika kuhamasisha Bima ya Afya kwa Wote.

8.0 Mikutano ya Wadau
Katika kufanikisha utekelezaji wa Bima ya Afya kwa Wote, Mfuko ulishiriki Kongamano la kujadili utekelezaji wa Bima ya Afya kwa wote na upatikanaji wa huduma kwa wananchi.Kongamano hili limesaidia katika maandalizi ya utekelezaji wa bima ya afya kwa wote.

Mafanikio haya yamewezekana kutokana na ushirikiano mzuri kati ya Serikali ya Mkoa wa Arusha, wadau wa maendeleo, na wananchi. Uboreshaji wa huduma za afya umechangia kuboresha ustawi wa jamii na kuongeza tija ya kiuchumi. Mkoa wa Arusha unaendelea kuwa mfano bora wa maendeleo endelevu.

Tully Mwakyusa
Meneja wa Mkoa

PWANI

WANANCHI WACHANGAMKIA BIMA YA AFYA

- **Yaongeza usajili wa wanachama kwa 72%**
- **Yaongeza uhakika wa Huduma za bima ya afya**

Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya (NHIF), unayo Ofisi yake katika Mkoa wa Pwani ambayo inahudumia wananchi wa Wilaya saba (7) ambazo ni Kibaha, Kisarawe, Mkuranga, Kibiti, Rufiji, Bagamoyo na Mafia. Zinazotengeneza Halmashauri (9) ambazo ni; Kibaha Mji, Kibaha, Chalinze, Bagamoyo, Kisarawe, Mkuranga, Kibiti, Rufiji na Mafia.

Kwa mujibu wa takwimu za Sesa ya watu na makazi ya mwaka 2022 Mkoa wa Pwani una jumla ya wakazi 2,024,947 wanaume 998,616 na wanawake 1,026,331. Mkoa wa Pwani una shughuli nyingi za kiuchumi kwa wananchi wake ikiwa ni pamoja na kilimo cha mazao ya Biashara na chakula (Mpunga, Korosho, Ufuta, Mbaazi, Uvuvi Ufugaji nk) Sambamba na hizi pia kuna shughuli za wajasiliamali wakubwa na wadogo bila kuhasau utalii hasa maeneo ya Bagamoyo na Mafia.

Katika eneo la Bima ya Afya, Mfuko ndani ya Mkoa wa Pwani umefanikiwa kwenye maeneo mbalimbali ambayo yamekuwa na manufaa makubwa kwa wananchi hususan katika uhakika wa kupata huduma za matibabu. Mafanikio hay oni pamoja na;-

1.0 Ongezeko usajili wa wanachama kwa 72%
Katika kipindi cha miaka minne ya serikali ya awamu ya sita na hadi kufikia june 2025 Mkoa umefanikiwa kusajili wanachama wapya 14,948 ikiwa ni ongezeko la 72% kutoka 10,730 mwaka 2024. Hii ni kutokana na na uwepo wa sheria ya bima ya afya kwa wote. Usajili wa wanachama hawa umeongezeka kutokana na kuongezeka kwa wigo wa elimu ya bima ya afya na maboresho ya huduma.

2.0 Elimu ya bima ya afya kwa wananchi
Katika eneo la elimu, Mkoa umeendelea kutoa elimu kwa makundi mbalimbali ili kuhakikisha wanajiunga na mfuko. Utoaji wa elimu huu umesaidia kuongezeka kwa wanachama wa Mfuko. Ili kuwafikia wananchi, elimu imetolewa kwa njia mbalimbali ikiwemo radio za kijamii (local radio), mikutano na wanafunzi na wazazi wa shule pamoja na makundi mengine ya wananchi kuhusu umuhimu wa bima ya afya.

3.0 Kushiriki matukio mbalimbali ya kijamii
Katika kipindi hiki ofisi ya mkoa imeongeza jitihada ya kushiriki matukio mbalimbali ya kijamii kama kutembelea vituo vya watoto yatima, kushiriki marathon na maonyesho mbalimbali lengo ikiwa ni kuutangaza Mfuko na huduma zake kwa makundi yote.

4.0 Vituo vya kitolea huduma za afya Pwani
Katika kipindi cha miaka minne ya serikali ya awamu

ya sita, Mkoa wa Pwani umeweza kuboresha huduma za tiba kwa wanachama wake kwa kusajili vituo 425 vya kutolea huduma za Afya ikijumuisha vituo vya umma, vituo vya ya sekta binafsi na vituo vya mashirika ya dini

5.0 Mikopo ya vifaa tiba, dawa na ukarabati

Ili kuhakikisha huduma zinakuwa bora zaidi, Ofisi ya Mkoa wa Pwani imeshiriki katika uboreshaji wa huduma za matibabu kwa kuendelea kutoa mikopo kwa vituo vya kutolea huduma na hivyo kupitia Mikopo hii vituo vimeboresha huduma zake na kuvutia wananchi kujiunga. Hospitali ya Mkoa wa Pwani (Tumbi) ni moja ya kituo ambacho kimefanyiwa ukarabati kwa kutumia fedha hizi za mkopo. Ukizingatia kuwa hapo awali kuna baadhi ya huduma zilikuwa hazipatikana kituoni hapo lakini sasa zinapatikana; moja wapo ya huduma hizi ni kusafisha damu (dialysis). Jumla ya Shilingi 536,018,476 zimetumika kukopesha Hspitali ya Rufaa ya Mkoa ya Tumbi, Hospitali ya Wilaya ya Mkuranga na Kliniki ya Zinga.

6.0 Ujenzi wa ofisi ya mkoa

Ofisi ya Mkoa wa Pwani imejengwa jengo lake na kuanza kutoa huduma hatua iliyosaidia wananchi kupata huduma katika mazingira mazuri. Katika kipindi hiki ambacho utekelezaji wa bima ya afya umeanza, Ofisi ya Pwani inawaomba wananchi kujiunga na kuwa na uhakika wa kupata huduma za matibabu wakati wote.

7.0 Maboresho ya mifumo

Kwa kipindi husika kumekuwa na maboresho makubwa sana ya mifumo kwa vituo hivi. Kwani kwa sasa vituo vyote vimewezeshwa kuwasilisha madai yao kwa njia ya mtandao licha ya kwamba kuna vichache ndio vimeunganishwa moja kwa moja na mfumo wa uchakataji wa madai wa Mfuko. Mifumo hii imekuwa na tija sana hasa kuwasaidia watoa huduma kupunguza makosa mbalimbali yanayotokana na kutumia karatasi wakati wa kuandika na pia inapunguza/kuondoa kabisa ucheleweshaji wa kuwasilisha madai haya.

8.0 Mahusiano na wadau na huduma kwa wateja

Ofisi ya Mkoa imefanya jitihada za kuhakikisha inaboresha mahusiano yake na wadau, kwa kipindi husika mahusiano yameboreka kwa kiasi kikubwa hatua inayosaidia kushirikiana katika shughuli mbalimbali za kuwafikia wananchi na kuwasajili.

JENGO LA OFISI YA NHIF MKOA WA PWANI

Gwamaka Mwakyoma
Meneja wa Mkoa

KIGOMA

KIGOMA NA MAFANIKIO YA AWAMU YA SITA

- **Dhana ya Bima ya Afya yaeleweka**
- **Wananchi wawa na uhakika wa huduma za matibabu**

Mkoa wa Kigoma unaundwa na Wilaya sita (6) ambazo ni Kakonko, Kibondo,Kasulu, Buhigwe, Uvinza, na Kigoma. Zinazotengeneza Halmashauri (8) za Kakonko, Kibondo,Kasulu ,Kasulu Mji, Buhigwe, Uvinza, Kigoma na Kigoma Manispaa .Kwa mujibu wa takwimu za Sesa ya watu na makazi ya mwaka 2022 Mkoa wa Kigoma una jumla ya wakazi 2,470,967.

Mkoa wa Kigoma Shughuli kuu za kiuchumi katika maeneo ya Kilimo, ufugaji, uvuvi, Biahara na utalii katika hifadhi za Gombe na Mahale.

Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya unajivunia uwepo wake katika Mkoa wa Kigoma ambapo kwa kipindi cha miaka minne, umepata mafanikio mbalimbali ambayo yameendelea kuleta uhakika wa huduma za matibabu kwa wanachama wake,

1.0 Ongezeko la wanachama
Katika kipindi cha miaka minne Mkoa umefanikiwa kusajili wanachama wapya 5,530 ikiwa ni ongezeko la 60% kutoka 3,272. Hii inatokana na kuwepo kwa mwamko mkubwa wananchi kuhusu masuala ya bima ya afya husussan katika kipindi hiki cha kuelekea utekelezaji wa bima ya afya kwa wote.

2.0 Ongezeka kwa vituo vya kutolea huduma na hali Ulipaji wa madai.
Mkoa wa Kigoma umeweza kuboresha huduma za matibabu kwa wanachama wake kwa kusajili vituo zaidi ya 325 vya kutolea huduma za Afya ikijumuisha vituo vya uma, vituo vya ya sekta binafsi na vituo vya mashirika ya dini ambavyo vimekuwa vikilipwa kwa wakati kwa kupunguza mud awa malipo kutoka siku 57 mwaka 2020 hdi siku 41 mwaka 2025.

3.0 Huduma za kibingwa na bingwa bobezi:
Katika eneo hili kumekuwa na mafanikio makubwa kutokana na wananchi kuwa na uwezo wa kupata huduma za kibingwa na kibingwa bobezi kwa urahisi zaidi ndani ya mkoa ikilinganishwa na awali ambapo huduma hizi walilazimika kuzifuata mikoa mingine na kwa gharama kubwa. Huduma hizi zinajumuisha vipimo vya uchuguzi kama CT Scan, huduma za kusafisha .damu (dialysis), huduma za kibingwa kwa maeneo ya magonjwa ya huduma za uzazi, mifupa, na upasuaji wa aina mbalimbali zinapatikana katika Hospitali ya Mkoa ya Maweni.

4.0 Mikopo ya kuboresha huduma vituoni.
Katika kuboresha huduma vituoni Mfuko ulianzisha mikopo ya riba nafuu kwa watoa huduma ikilenga kuinua na kuboresha mazingira ya huduma katika vituo vinavyohudumia wanachama wake. Mikopo ililenga katika maeneo ya ujenzi (kupanua), ukarabati, Tehama, samani , dawa na vitendanishi pamoja na vifaa tiba vya kisasa. Mfano mzuri ni vituo vimeweza kuweka mashine za kisasa za uchunguzi na kuanzisha maduka ya dawa ya ndani ambapo jumla ya TZS.349,249,400/= zimetolewa kwa kipindi hiki katika vituo saba mkoani Kigoma.

6.0 Mahusiano na wadau
Ofisi ya Mkoa imefanya jitihada za kuhakikisha inaboresha mahusiano yake na wadau, kwa kipindi husika mahusiano yameboreka kwa kiasi kikubwa. Kwasa hali tathimini ya mahusiano na hali ya kuridhika na huduma kwa wateja wetu iko katika asilimia 93%-95% . Haya ni matokeo ya jitihada zilizo fanywa na Mfuko katika maeneo yafuatao;-

Kushiriki katika shuguli za kijamii pamoja na kutoa msaada wa mshuka na vifaa vya kujifungulia kwa akina mama wajawazito, elimu na ushirikiano na wadau katika kushughulikia na kutoa majibu ya changamoto za wadau kwa wakati, maboresho ya mifumo, kuboreka kwa huduma vituoni, ushirikiano na wadau, viongozi wa ngazi zote, taasisi, madhehebu ya dini na binafsi na kushirikiana na mamlaka za Mkoa katika kutoa elimu ya umuhimu wa Bima ya Afya kwa wanachi.

Elius Odhiambo
Meneja wa Mkoa

GEITA

YASOGEZA HUDUMA KWA WANACHAMA

- **Wanachama sasa kupata huduma za kibingwa**
- **Yajipanga kuwafikia wananchi wote**

Mkoa wa Geita ni kati ya mikoa yenye kasi kubwa ya ukuaji wa idadi ya wakazi kutokana na vizazi na uhamiaji kutoka maeneo mbalimbali ya nchi ambapo kwa sasa una jumla ya wakazi wapatao 2,977,608 kwa mujibu wa sensa yam waka 2022.

Shughuli kuu za kiuchumi katika Mkoa wa Geita ni pamoja na uchimbaji madini ya dhahabu, kilimo, ufugaji, uvuvi na biashara za bidhaa na huduma. Sekta ya madini ya dhahabu ndiyo sekta kuu ya kiuchumi na itaendelea kuongoza uchumi wa mkoa kutokana na uwezeshaji wa miundombinu na teknolojia zinazotolewa na serikali pamoja na ugawaji wa vitalu vipya vya uchimbaji madini.

Ili utekelezaji wa shughuli za kiuchumi uweze kufanyika kwa ufanisi, Wananchi hao wanatakiwa kuwa na uhakika wa huduma za matibabu ili wanapapotwa na maradhi waweze kutibiwa bila kikwazo chochote.

Ofisi ya Mkoa wa Geita, imekuwa ikitekeleza majukumu yake ikiwemo kutoa elimu, kuhamasisha wananchi, kuwasajili na kusimamia upatikanaji wa huduma za matibabu kupitia vituo vilivyosajiliwa na Mfuko.

Katika kipindi hiki cha miaka minne ya uongozi wa Serikali ya Awamu ya Sita, Ofisi ya Geita imefanikiwa katika maeneo mbalimbali yanayolenga utoaji wa huduma za matibabu kwa wanachama wake ili kutimiza lengo la Serikali la Bima ya Afya kwa Wote. Mafanikio hay oni pamoja na;-

1.0 Upatikanaji wa huduma za matibabu

Uhakika wa upatikanaji wa huduma za matibabu ni moja ya kigezo kikubwa cha kuvutia wananchi kujiunga na bima ya afya, katika hili, Ofisi ya NHIF Geita, imefanikiwa kuwa na ongezeko la Vituo vya kutolea huduma 69 ambapo Mwaka 2021/22 mfuko ulikuwa na vituo 185 hadi kufikia vituo 254 mwaka 2025.

Vituo hivi vimejumuisha Hospitali ya Rufaa ya Kanda ya Chato ambayo inatoa huduma za kibigwa bobezi za tiba za moyo, mifupa na mfumo wa fahamu. Uwepow a Hospitali hii umekuwa chachu kwa wananchi kujiunga lakini pia kuondoa usumbufu walioupata awali wa kuzifuata huduma za kibingwa umbali mrefu.

Vituo vingine ni pamoja na vya binafsi na madhehebu ya dini ambavyo vimechochea upatikanaji wa huduma bora kwa wanachama mkoani Geita.

2.0 Malipo kwa watoa huduma

Ofisi ya Mkoa wa Geita imekuwa na mafanikio ya ulipaji wa madai kwa wakati kwa watoa huduma hatua iliyosaidia kuondoa malalamiko na kuboresha huduma kwa wanachama. Kwa sasa watoa huduma wanalipwa ndani ya 45 ikilinganishwa na awali ambapo walilipwa kwa zaidi ya siku 90 tangu kuwasilisha madai yao.

Ulipaji wa fedha hizi kwa wakati umewawezesha watoa huduma kuboresha huduma zao kwa kuongeza upatikanaji wad awa na vitendanishi hivyo wanachama kupata huduma kwa ubora zaidi.

3.0 Elimu kupitia Maonesho ya Madini

Ofisi ya Mkoa wa Geita imekuwa mdau mkubwa katika Maonesho ya Kitaifa ya Madini ambayo hufanyika kila mwaka Mwezi Septemba. Ofisi imekuwa ikishiriki maonesho haya kwa kutoa elimu, kusajili, kutatua changamoto mbalimbali za wanachama na kuhamasisha wananchi kujiunga na Mfuko.

4.0 Usogezaji wa huduma kwa wananchi

Ili kuwezesha malengo ya Serikali ya kuwafikia wananchi wote katika mpango wa Bima ya Afya kwa Wote, NHIF Geita imefanikiwa kusogeza zaidi huduma kwa wananchi kwa kufungua Ofisi ndogo katika Mji mdogo wa Katoro na Bukombe. Uwepo wa Ofisi hizi utawezesha wananchi kuwa na mwamko mkubwa wa kujiunga na bima ya afya.

5.0 Utekelezaji wa mpango wa Bima ya Afya kwa wote

Ofisi ya Mkoa wa Geita, imeanza utekelezaji wa Bima ya Afya kwa Wote ambapo kwa sasa inaendelea na utoaji wa elimu ya dhana ya bima ya afya ikiwemo umuhimu wake ili wananchi wajiunge na wawe na uhakika wa kupata huduma za matibabu bila kikwazo chochote.

Jarlath Mushashu
Meneja wa Mkoa

MWANZA

- **Mwanza yaboresha huduma za matibabu**
- **Wigo wa wanachama wapaa kwa 34.5%**

Mwanza ni moja ya mkoa uliopo Kanda ya Ziwa ambao una jumla ya watu 3,699,872 ikiwa na Wilaya saba na Halmashauri za wilaya nane. Mkoa huo unazo shughuli za kiuchumi ambazo ni kilimo, ufugaji, uvuvi na biashara.

Katika kuhakikisha wakazi wa Mkoa wa Mwanza wanapata huduma za bima ya afya, Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya (NHIF), ulisogeza huduma kwa kufungua Ofisi ya kuhudumia wananchi.

Ofisi ya Mwanza inayo mafanikio mengi iliyoyapata ndani ya kipindi cha miaka minne ya Serikali ya Awamu ya Sita inayoongozwa na Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan. Mafanikio hay oni pamoja na;-

1.0 Yatoa Mikopo ya Vifaa Tiba na Dawa
Moja ya lengo kubwa la Mfuko ni kuhakikisha wanachama wake wanapata huduma bora kulingana na mahitaji yao, ili kufanikisha hili, Mfuko hushirikiana na vituo kwa kuvipatia mikopo yenye riba nafuu ya uboreshaji wa miundombinu ya huduma na vifaa tiba.

Ofisi ya Mwanza katika kipindi cha miaka minne, imetoa mikopo katika maeneo ya ujenzi (kupanua), ukarabati, Tehama, samani , dawa, vitendanishi na vifaa tiba hususan katika huduma za uchunguzi. Kupitia huduma hui vituo vimenufaika na vimeweza kujenga majengo, kliniki maalumu kwa wanufaika, kuanzisha maduka ya dawa ya ndani, ukarabati wa vituo na kununua mashine za uchunguzi kubwa mfano zikiwemo CT Scan.
Uboreshaji huu umefanikisha upatikanaji wa huduma bora kwa wanachama na wananchi wote wa Mkoa wa Mwanza na mikoa Jirani ambao hupata huduma za matibabu kupitia vituo vilivyosajiliwa na Mfuko.

2.0 Yaongeza Wanachama kwa 34.5%
Kwa kipindi cha Miaka minne mwitikio wa wanachi kujiunga na huduma za Bima ya afya umekuwa ukiongezeka kwa kila mwaka kwa wastani wa asimilia 34.50 na hii inatokana na uwekezaji mkubwa katika eneo la elimu na uhamasishaji.

3.0 Upatikanaji wa huduma na maboresho
Huduma za afya zimeboreshwa na kuimalika kwa kiasi kikubwa sana. Serikali imewezesha huduma kupatikana kuanzia ngazi ya kijiji (kila kijiji kina zahanati) kwa uhakika zaidi, upatikanaji wa dawa umeongezeka kwa kiwango kikubwapamoja na watumishi vituoni. Kwa huduma zilizo kuwa zinahitaji rufaa kwa sasa zinapatikana katika vituo vya chini mfano uzazi wa njia zote kawaida na upasuaji unapatikana kuanzia ngazi ya zahanati, magari ya wagonjwa siyo changamoto tena.

USAJILI WA VITUO	
AINA YA KITUO	IDADI
Rufaa Kanda	2
Rufaa Mkoa	5
Hospitali za Wilaya	20
Vituo vya Afya	61
Zahanati	321
Maduka ya Dawa	37
Vituo vya Uchunguzi	2
Vituo vya Huduma za Kliniki	12

4.0 Yasajili Vituo 465

Mpaka sasa mfuko umesajili vituo 465 ambapo kuna Hospitali 2 za rufaa kanda ambapo wanufaika wa Mfuko wanapata huduma za kibingwa na kibingwa bobezi, Hospitali za rufaa mkoa 5,, Hospitali za Wilaya 20, Vituo vya afya 61 viko ngazi za tarafa na kata/kijiji, zahanati 321 kwa ajili huduma za msingi na dharula, Maduka ya dawa 37, vituo vya uchunguzi 2, vituo vya huduma za kliniki 12. Vituo hivi vinajumuisha zaidi ya vituo 100 (Hospitali ya rufaa mkoa 1, za Wilaya mpya 5, vituo vya afya zaidi ya 25 na Zahanati zaidi ya 70) vilivyojengwa.

5.0 Huduma za kibingwa na bingwa bobezi:

Huduma za kibingwa na kibingwa bobezi zinapatikana kwa urahisi mkoani Mwanza ikilinganishwa na awali ambapo wanachama walilazimika kusafiri kwenda Dar es Salaam au nje ya nchi kupata huduma hizo.

Hudma hizo zinajumuisha vipimo vya uchuguzi kama CT Scan, zipo katika vituo 4, MRI katika vituo 2, huduma za kusafisha damu zipo katika vituo 5 na huduma nyingi za kibingwa kwa maeneo ya magonjwa ya saratani, huduma za uzazi, mifupa, Moyo, mfumo wa fahamu na upasuaji wa aina mbalimbali kutaja kwa uchace, huduma za kusafisha damu (dialysis). Mfuko umesajili vituo vyote hivi kuhakikisha mnufaika anapata huduma karibu.

6.0 Asilimia 85 ya Madai yalipwa ndani ya siku 45:

Ili kuhakikisha huduma zinapatikana na zinaboreka vituoni Mfuko umefanya jitihada za makusudi kupunguza muda wa kulipa madai ya watoa huduma. Kwa sasa madai yanalipwa katika wastani wa siku 45 badala ya siku 60 za kimkataba. Lengo ni kuzipunguza zaidi. Mfano kwa mwaka wa fedha 2024/2025 Jumla ya TZS. 45,101,691,110.85 zimelipwa na madai 85% yamelipwa ndani ya 45.

7.0 Mahusiano na wadau

Ofisi ya Mkoa imefanya jitihada za kuhakikisha inaboresha mahusiano yake na wadau, kwa kipindi husika mahusiano yameboreka kwa kiasi kikubwa. Kwasa hali ya tathimini ya mahusiano na hali ya kuridhika na huduma kwa wateja wetu iko katika asilimia 92%-96% ikilinganishwa na awali takwimu zilionyesha 83%-90%. Haya ni matokeo ya jitihada zilizo fanywa na Mfuko katika maeneo yafuatao.

Elimu na ushirikiano na wadau (elimu kwa watoa huduma, elimu kwa wanufiaka, kushughulikia, kutoa majibu ya changamoto za wadau kwa wakati, Maboresho ya mifumo, kuboreka kwa huduma vituoni, ushirikiano na wadau, viongozi wa ngazi zote, taasisi, madhehebu ya dini, binafsi, kushiriki katika shughuli za wadau na wao kushiriki katika shughuli zetu mfn: maadhimisho, maonyesho, vikao/mikutano kutoa elimu, matamasha hii inatupa nafasi kuwasikiliza, kupokea ushauri, kutoa ufafanuzi na malipo ya watoa huduma kwa wakati.

Mfuko umekuwa na utaratibu wa kukutana na wadau ambao ni waajiri, watoa huduma, jamii nzima ambao wengine ni wanufaika watarajiwa ili kuwasikiliza kupitia mikutano, maonyesho, maadhimisho, matamasha mbalimbali, mitandao ya kijamii, kuhudhuria mialiko yao.

8.0 Wito kwa wananchi

Kutokana na uboreshaji wa huduma za matibabu uliofanyika, wananchi wanaombwa kujiunga na bima ya afya ili kunufaika au kuwa na uhakika wa kupata huduma za matibabu wakati wote.

Mfuko umeshafanya maandalizi ya kuhudumia wanachama wengi zaidi hivyo upatikanaji wa huduma ni wa kiwango cha juu.

Ofisi ya Mwanza iko tayari kuwahudumia wakati wote na kutatua changamoto, kwa ufafanuzi, maoni na elimu wasiliana nasi kupitia namba ya simu ya kupiga bure 199 au barua pepe info@mwanza@nhif.or.tz au fika katika ofisi zetu zilizoko katika Jengo la TMDA Nyakato Buzuruga, Ilemela Mwanza. Karibu sana tukuhudumie.

Isaack Katenda
Meneja wa Mkoa

SHINYANGA

- **Wigo wa wanachama waongezeka kwa 13.9%**
- **Huduma bora zavutia wananchi kujiunga bima ya afya**

Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya (NHIF), unayo Ofisi yake katika Mkoa wa Shinyanga ambao una Wilaya (3) na Halmashauri (6) ambazo ni Kahama, Kishapu, Msalala,Ushetu, Shinyanga Vijiji na Manispaa.

Kwa mujibu wa takwimu za Sesa ya watu na makazi ya mwaka 2022 Mkoa wa Shinyanga una jumla ya wakazi 2,241,299 ambao una shughuli nyingi za kiuchumi kwa wananchi wake ikiwa ni pamoja na kilimo cha mazao ya Biashara (Tumbaku na Pamba) na mazao ya chakula kama vile (Mpunga, Mahindi, Dengu,Alizeti na Karanga, Ufugaji wa Ngombe,mbuzi na Kuku,Uchimbaji wa madini (Wachimbaji wakubwa na wadogo), Viwanda vya uzalishaji,Biashara na wajasiriamali wadogo.

Katika kipindi cha miaka minne ya Serikali ya awamu ya sita, ofsi ya Mkoa wa Shinyanga imepata mafanikio makubwa katika maeneo mengi ambayo ni pamoja na;-

1.0 Yaongeza wanachama kwa 13.9%
Kutokana na mwamko mkubwa wa wananchi kujiunga na bima ya afya, katika kipindi cha miaka minne, Ofisi ya Shinyanga imefanikiwa kusajili jumla ya wanachama 23,696 wanaojumuisha makundi ya sekta ya Umma, sekta Binafsi na sekta isiyo rasmi. Ongezeko hili la usajili wa wanachama ni sawa na ongezeko la 13.90% ya wanachama waliosajiliwa kwa mwaka 2020/2021.
Aidha ndani ya kipindi hiki, ofisi imefanikiwa kusajili makampuni makubwa mawili, Williamson Diamond LTD ambayo ni kampuni kongwe katika uchimbaji wa madini ya Almasi na Kampuni ya Jambo Food Products inayojihusisha na uzalishaji wa vinywaji na bidhaa zingine za chakula.

Kupitia usajili wa makampuni haya jumla ya watumishi zaidi ya 600 na wategemezi wao wameweza kuwa na uhakikia wa huduma bora za matibabu wao na wategemezi wao.

2.0 Vituo Vya Kutolea Huduma vyaongezeka
Ili kuwahakikishia wanachama upatikanaji wa huduma za matibabu, Mfuko umefanikiwa kupanua wigo wa vituo kwa kusajili vituo 262 vinavyotoa huduma kwa Wanachama wa Mfuko, vituo 239 vikiwa ni vya Serikali na 23 vikiwa ni vituo vya Binafsi.
Idadi ya vituo 262 ni ongezeko la vituo 88 sawa na asilimia 51 ikilinganishwa na vituo 174 vilivyokuwa vimesajiliwa na Mfuko hadi kufikia June 2021. Uwepo wa vituo vingi vilivyosajiliwa katika ngazi zote kuanzia Hospitali ngazi ya Rufaa ya Mkoa hadi vituo ngazi ya Zahati katika kila Halmashauri umeendelea kurahisha upatikanaji na ubora wa huduma karibu na wananachi na kutoa wigo mpana wa uchaguzi wa vituo vya kupatia huduma kwa wanachama wanufaika wa Mfuko.

3.0 Yaongeza malipo kwa 24.85%
Katika kipindi cha miaka minne ya Serikali ya Awamu ya Sita, Ofisi ya Mkoa wa Shinyanga imerekodi ongezeko chanya la malipo yanayolipwa kwa watoa huduma, kipindi cha mwaka 2021/2022 hadi 2024/2025, Mkoa umelipa jumla ya TZS 23,584,508,734.30 kwa watoa huduma. Fedha hizi

zimekuwa ni chachu ya maboresho ya huduma katika vituo husika. Aidha ulipaji wa madai kwa sasa unafanyika ndani ya siku 45 ikilinganishwa na hapo awali ambapo madai yalilipwa ndani ya siku 60.
Hatua hii imesaidia kuondoa malalamiko ya watoa huduma hivyo kuwezesha wanachama kupata huduma bora wanapokuwa vituoni.

4.0 Kuimarika kwa mahusiano kati ya Mfuko na wadau wa Mkoa

Katika kipindi cha miaka minne ya Serikali ya awamu ya sita, Ofisi ya Mkoa wa Shinyanga imefanikiwa kudumisha na kuboresha mahusiano mazuri iliyonayo na wadau wote wa ndani na nje ya ofisi ya Mkoa.

Mahusiano yameboreka kwa kufanya kazi kwa ukaribu na mamlaka zingine za serikali kama Ofisi ya Mkuu wa Mkoa, Katibu Tawala wa Mkoa, Ofisi za Wakuu wa Wilaya na Wakurugenzi wa Halmashauri zote za Mkoa wa Shinyanga.
Mahusiano yameboreshwa kwa wadau wote wanaofanya kazi na ofisi ya Mkoa wakiwemo Waajiri waliosajiliwa, watoa huduma , wanachama na wananchi kwa ujumla wake.
Mahusiano hayo mazuri yamejengwa kwenye msingi wa kushirikiana katika utekelezaji wa shughuli mbalimbali za kiserikali na kijamii na taasisi zingine za serikali, zisizo za kiserikali, watoa huduma, waajiri, wanachama na wananchi wote.
Msingi wa ushirikiano umesajidia ofisi kuhudumia vizuri wadau kwa kufanyia kazi maombi, maoni na mapendekezo yao katika kuhakikisha wanaridhika na huduma zetu na kusaidia ofisi katika kutimiza majukumu yake.

5.0 Uwekezaji wa miundombinu na vifaa

Katika kipindi cha miaka minne ya Serikali ya awamu ya Sita, Serikali imefanya uwekezaji mkubwa kwenye miundombinu ya kutolea huduma za afya na upatikanaji wa dawa na vitendanishi ikiwemo uwepo wa vitengo vya magonjwa ya dharura katika kila Hospitali na huduma za msingi za upasuaji kwenye kila Kituo cha Afya.
Kwa kuzingatia kuongezeka kwa gharama za matibabu na umuhimu wa kila mwananchi kuwa na uhakika wa huduma za Afya, wananchi wanaombwa kujiunga na bima ya afya ili kunufaika na uwekezaji huu katika kupata huduma za matibabu.
Utaratibu wa usajili umeboreshwa sana kupitia mifumo ya TEHAMA ambapo kwa sasa sio lazima kwa mwananchi kufika ofisini kupata huduma kwani anaweza kujisajili kupitia mfumo wa kujihudumia wa mfuko unaopatikana kupitia

KAGERA

- **Wigo wa wanachama waongezeka kwa 13.9%**
- **Huduma bora zavutia wananchi kujiunga bima ya afya**

Ismail Kangeta
Meneja wa Mkoa

Mkoa wa Kagera ni miongoni mwa mikoa yenye historia ya kipekee na shughuli nyingi za kiuchumi nchini Tanzania. Ukiwa na ukubwa wa kilomita za mraba 40,838, mkoa huu unapakana na mataifa jirani ya Burundi, Rwanda na Uganda, hivyo kuufanya kuwa kitovu cha biashara na usafirishaji.
Ofisi ya NHIF Kagera inahudumia jumla ya Halmashauri nane: Bukoba Manispaa, Bukoba DC, Missenyi, Karagwe, Kyerwa, Biharamulo, Ngara na Muleba.
Katika kipindi cha miaka minne ya Mhe. Samia Suluhu Hassan, Ofisi ya Kagera imefanikiwa katika maeneo mbalimbali ikiwemo kuongeza wigo wa elimu, uhamasishaji na usajili wa wanachama ambao umechochea kuboresha huduma za matibabu mkoni humo.

Katika mwaka wa fedha 2024/2025, lengo lilikuwa wanachama wapya 35,490, ambapo 8,441 walisajiliwa (sawa na 24%). Kwa mwaka wa fedha 2025/2026, mikakati mipya imewekwa kuhusisha makundi maalum kama Wanafunzi, Vyama vya Ushirika, Taasisi za Dini, Taasisi Binafsi na Jumuiya za Watumiaji Maji na Wafanya Biashara.

1.0 Usajili wa Vituo vya huduma
Mkoa umefanikiwa kuongeza wigo wa Vituo vya kutolea huduma ambapo mpaka sasa jumla ya vituo 360 vimesajiliwa na vinatoa huduma za matibabu kwa wanachama wa Mfuko.
Kusajiliwa kwa vituo hivi kumeleta mapinduzi makubwa ya upatikanaji wa huduma za matibabu lakini pia uboreshaji wa huduma kutokana na kuwepo kwa chanzo cha uhakika cha mapato kutoka NHIF.

2.0 Yalipa Madai Bilioni 7.7 kwa Watoa Huduma
isi ya Mkoa wa Kagera kwa mwaka 2024/2025 jumla ya Shilingi Bilioni 7.75 kwa vituo vyote vilivyosajiliwa mkoani huo. Malipo haya yamefanyika chini ya muda uliopo kwenye mkataba wa huduma. Kulipwa madai kwa wakati kumesaidia kupunguza malalamiko ya watoa huduma ambayo awali yalikuwepo.

3.0 Kusogeza huduma kwa wananchi
Ili kurahisisha utekelezaji wa bima ya afya kwa wote, Ofisi ya Mkoa wa Kagera imefanikiwa kushusha huduma kwa wananchi zaidi kwa kufungua Ofisi ndogo katika Wilaya ya Karagwe ambayo itasaidia wananchi katika kupata elimu kwa haraka na kujisajili kwa urahisi zaidi.

4.0 Hali ya mahusiano kati ya mfuko na wadau wa mkoa
Kwa kipindi cha Serikali ya awamu ya sita, Ofisi ya Mfuko Mkoa wa Kagera imeendeleza mahusiano na ushirikiano na wadau muhimu wa Mkoa ikiwemo Ofisi ya Mkuu wa Mkoa, Ofisi ya Katibu tawala wa Mkoa pamoja na wasaidizi wake wote katika Halmashauri zote za Mkoa na wadau wengine wakiwemo Waajiri na Watoa huduma.

5.0 Mikakati iliyopo
Mfuko kupitia Ofisi ya Kagera inayo mikakati mbalimbali ikiwemo kupanua wigo wa wanachama kwenye makundi mapya, kulipa madai kwa wakati na kupunguza makato kwa watoa huduma, kudhibiti udanganyifu kwa watoa huduma na wanachama, kuboresha huduma kwa wateja kwa kushughulikia changamoto kwa haraka na kutoa elimu zaidi kwa waajiri katika matumizi ya Mfumo wa usajili ili waweze kujihudumia wenyewe.

Bi. Irene Kataraihya
Meneja wa Mkoa

LINDI

LINDI YALETA CHACHU USAJILI WA WANACHAMA

Yasajili zaidi ya wanachama Elfu nne

Mkoa wa Lindi ni moja ya Mkoa ulioko Kusini mwa Tanzania wenye jumla ya wananchi 1,912,502 kw mujibu wa Sensa yam waka 2022. Shughuli zake kuu za kiuchumi ni kilimo, ufugaji na uvuvi. Mkoa huu ni moja ya mkoa unaozalisha zao la korosho na ufuta.

Katika kipindi cha Uongozi wa Awamu ya Sita, Mkoa wa Lindi umekuwa na mafanikio katika nyanja mbalimbali ambazo ni Pamoja na;-

1.0 Usajili wa Wanachama

Na	Kipimo	2021/2022	2022/2023	2023/2024	2024/2025
	Wanachama waliosajiliwa	2,439	2,223	2,923	4,137

2.0 Usajili wa Vituo

Ili kuwahakikishia wanachama upatikanaji wa huduma bora, Mkoa ulifanikiwa kusajili vituo 305 vyenye umiliki wa Serikali, Binafsi na Madhehebu ya dini.

Vituo na umiliki wake	Serikali	Dini	Binafsi
	299	5	1
	98.03%	1.63%	0.33%

3.0 Malipo kwa Watoa huduma

Ofisi ya Mkoa wa Lindi imelipa jumla ya Shilingi 9,393,520,347.37 kwa huduma zilizotolewa kwa wanachama ambapo madai haya yamelipwa ndani ya siku 45 ikilinganishwa na siku 60 za awali.

4.0 Uboreshaji wa huduma kupitia mikopo ya vifaa tiba

Ili kuimarisha ubora wa huduma zitolewazo kwa wanachama, Mfuko umeendelea kutoa mikopo nafuu wa vifaa tiba ambapo kwa kipindi tajwa kiasi cha shilingi 19,353,818.53 zimetumika katika Hospitali ya Kipatimu, shilingi 19,800,000.00 na Shilingi 10,000,000 hospitali ya wilaya Ruangwa na shilingi 10,000,000.

5.0 Ushiriki wa NHIF Mbio za Mwenge wa Uhuru

Ofisi ya mkoa imekua ikishiriki kikamilifu mbio za Mwenge wa Uhuru kila mwaka kwa kuchangia na kushiriki mbio hizi. Kipekee, mwaka 2025 mbio za mwenge wa Uhuru ziliweka jiwe la Msingi la Jengo la NHIF ambalo ni ofisi mpya zitakazohudumia wana Lindi.

6.0 Mahusiano ya Mfuko na Wadau

Ofisi ya Mkoa imefanikiwa kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi ikiwa na ushirikiano mkubwa kutoka kwenye uongozi wa Mkoa Wakuu wa Wilaya zote za Mkoa wa Lindi, Ruangwa, Liwale, Nachingwea, Kilwa na Lindi Manispaa inayojumuisha Halmashauri ya Mtama na Jimbo la Mchinga.

RUVUMA

RUVUMA YAFANIKIWA KUSAJILI VITUO 418

Bw. Hance Mwankenja
Meneja wa Mkoa

Mkoa wa Ruvuma ni moja ya Mkoa unaojishughulisha na shughuli za kiuchumi ambazo ni Kilimo na uchimbaji Madini yakiwemo Makaay a Mawe.

Katika kipindi cha Uongozi wa Awamu ya Sita, Mkoa wa Ruvuma umekuwa na mafanikio katika nyanja mbalimbali ambazo ni Pamoja na;-

1. Usajili wa Wanachama

Katika eneo hili, Mkoa umefanikiwa kuwafikia wananchi wa makundi yote ambapo jumla ya Wanachama 4,033 wamesajiliwa kutoka makundi ya Waajiriwa, Wanafunzi, Waajiri Binafsi na Vifurushi.

2. **Usajili wa Vituo**

Ili kuwahakikishia wanachama wanachama wanapata huduma bora, Mkoa ulifanikiwa kusajili vituo vituo 418 vyenye umiliki wa Serikali, Binafsi na Madhehebu ya dini. Vituo hivyo vina mchanganuo ufuatao;-

Serikali	338	418
Binafsi	26	
Madhehebu ya dini	54	

3. **Yalipa zaidi ya Bilioni 26.9**

Ofisi ya Mkoa wa Ruvuma katika kipindi cha Miaka minne, imefanikiwa kulipa jumla ya Shilingi 26,974,688,793.63 kwa huduma zilizotolewa kwa wanachama ambapo madai haya yamelipwa ndani ya siku 45 ikilinganishwa na siku 60 za awali.

4. **Mahusiano ya Mfuko na Wadau**

Mahusiano kati ya Mfuko na wadau wa Mkoa ni mazuri ambayo yamerahisisha utendaji kazi hususan katika kuwafikia wananchi na kuwahamasisha kujiunga na Mfuko

5. **Wito kwa wananchi**

Wakazi wa Mkoa wa Ruvuma wanaombwa kuendelea kutumia huduma za Bima ya afya na kujiunga na kuwa na uhakika wa kupata huduma za matibabu wakati wote.

Bw. Benjamin Mwalugaja
Meneja wa Mkoa

SINGIDA

HUDUMA ZA MATIBABU ZABORESHWA

Wigo wa vituo wafikia 299

Mkoa wa Singida kwa mujibu wa Sensa ya mwaka 2022 ina jumla ya wananchi 2,008,058 ambapo asilimia 84 ya wananchi hao wanaishi vijijini na 16% wanaishi mjini.
Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya mkoani Singida unayo Ofisi ya Mkoa ambayo majukumu yake ni pamoja na kusajili wanachama na bima ya afya, kusajili watoa huduma na kulipa madai yao, kutoa elimu na kushiriki maendeleo ya Mkoa wa Singida ikiwemo uboreshaji wa huduma za matibabu.

Katika kipindi cha miaka minne (2021-2021) ya Serikali ya Awamu ya Sita, Ofisi ya Mkoa imeshiriki shughuli mbalimbali ambazo zimekuwa na mafanikio makubwa.

1.0 Usajili wa Wanachama

Ofisi imefanikiwa kuwafikia wananchi wa Mkoa wa Singida kwa kuwapa elimu, kuwahamasisha kujiunga na bima ya afya ili wawe na uhakika wa kupata huduma za matibabu wakati wote na bila kikwazo cha fedha. Kutokana na hilo, jumla ya wanachama wapya 17,130 wamesajiliwa.

Wanachama hao wametokana na makundi ya wanafunzi 14,540, Watumishi wa umma 185, Watumishi sekta Binafsi 812, wanachama wa vifurushi 1,483, Madaktari tarajali 39 na madiwani 71.

2.0 Usajili wa Vituo

Ofisi ya Mkoa imefanikiwa kusajili jumla ya vituo 299 vya kutolea huduma ambapo vya Serikali ni 252, Vituo Binafsi 27 na madhehebu ya Dini 20.

3.0 Mahusiano na Wadau

Ofisi ya Mfuko ina mahusiano ya kuridhisha na uongozi wa mkoa kwa kushiriki kikamilifu katika shughuli zinazoandaliwa na mkoa pamoja na mkoa kushiriki katika shughuli zinazoratibiwa na mfuko ambapo shughuli hizo ni pamoja na Mapokezi ya mwenge wa uhuru, Mei mosi, Maadhimisho ya siku ya wanawake duniani na Shuhghuli za Mfuko za uandikishaji na uhamasishaji wa makundi mbalimbali ya wanachama.

Bw. Franklin Chekani
Meneja wa Mkoa

SIMIYU

WANANCHI SIMIYU WAIKUBALI BIMA YA AFYA

Huduma za Matibabu zaboreshwa Yalipa Bilioni 9.5/=

Mkoa wa Simiyu una jumla ya Wilaya tano (5) zenye jumla ya Halmashauri 6 ambazo ni Bariadi mjini, Bariadi Vijijini, Busega, Itilima, Maswa na Meatu. Mkoa wa Simiyu zikiwa na idadi ya wananchi 2,140,497 wanaojishughulisha na Kilimo, Ufugaji, Uvuvi, Ujasiriamali, Biashara na Uchimbaji wa madini.

Katika kipindi cha miaka minne ya Serikali ya Awamu ya Sita, Ofisi ya NHIF Simiyu imekuwa na mafanikio makubwa hususan kuwafikia wananchi na kuwaelimisha kuhusu bima ya afya kwa lengo la kubadili mtazamo wa kiimani uliokuwa kwa wananchi wa Mkoa huo.

Kutokana na uwepo wa Ofisi ya NHIF, imesaidia kueleweka kwa dhana ya bima ya afya lakini pia uwekezaji uliofanywa na Serikali katika eneo la huduma za matibabu umechochea wananchi kuwa na mwamko wa kujiunga na bima ya afya.

Mafanikio ambayo Mfuko kupitia Ofisi ya Mkoa imeyapata ni pamoja na;-

1.0 Usajili wa Wanachama

Katika eneo hili jumla ya wanachama 35,925 wamesajili ambapo Watumishi wa Umma ni 27,338, Watumishi wa makampuni Binafsi 1,721 na Sekta isiyo rasmi kupitia vifurushi ni wanachama 6,866.

2.0 Usajiliwa Watoa Huduma

Ili kurahisisha upatikanaji wa Huduma za Matibabu kwa wanachama wake, Mfuko kupitia Ofisi ya Mkoa wa Simiyu imefanikiwa kusajili jumla ya Vituo 251 kuanzia ngazi ya Zahanati hadi Hospitali ya Mkoa.

2.1 Usajili wa Vituo kwa ngazi

Na	Ngazi ya kituo	Serikali	Binafsi	Taasisi za dini	Jumla ya Vituo
1	Zahanati	205	9	7	221
2	Kituo cha Afya	19	1	1	21
3	Hospitali za Wilaya/Halmashauri	6	0	2	8
4	Hospitali Rufaa Mkoa	1	0	0	1
	Jumla	**231**	**10**	**10**	**251**

3.0 Malipo kwa Watoa Huduma

Ofisi ya Mkoa wa Simiyu pia inalo jukumu la kuhakikisha inalipa madai kwa watoa huduma, gharama ambazo wanachama wamezitumia wakati wa kupata huduma za matibabu. Mchanganuo wa malipo hayo ni kama ifuatavyo;-

Na	Mwaka	Jumla ya Malipo yaliyofanyika
1	2021	1,031,142,240.00
2	2022	1,803,704,772.00
3	2023	2,398,417,699.00
4	2024	2,524,845,131.00
5	2025	1,803,806,093.40

4.0 Hali ya mahusiano kati ya Mfuko na wadau wa mkoa;

Ofisi ya Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya Mkoa wa Simiyu umekua na mahusiano mazuri na wadau wote katika mkoa hususan Ofisi ya Mkuu wa Wilaya, Wakuu wa Wilaya zote, Watoa Huduma, Waajiri na wadau wengine. Mahusiano haya yamesaidia utekelezaji wa shughuli za Mfuko hususan katika kuwafikia wananchi.

5.0 Wito kwa wananchi

Ili kuhakikisha wananchi wote wanakuwa na uhakika wa kupata huduma za matibabu bila kikwazo cha fedha, Mfuko unawaomba kujiunga na bima ya afya ili kunufaika na uwekezaji mkubwa uliofanywa na Serikali kwenye sekta ya afya.

Bw. Fidelis Shauritanga
Meneja wa Mkoa

DODOMA

DODOMA YAANZA UTEKELEZAJI BIMA YA AFYA KWA WOTE

Yaboresha Huduma za Matibabu

Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya una dhamana ya kuhakikisha huduma za afya zinawafikia Wananchi wote ili kuwa na Jamii yenye afya bora na Ustawi, ambayo itachangia kikamilifu katika maendeleo ya mtu binafsi na Maendeleo ya nchi kwa ujumla.

Ili kuhakikisha hilo linatekelezeka, Mfuko unazo Ofisi zake katika mikoa yote ikiwemo Dodoma ambayo ndio Mji Mkuu wa nchi ya Tanzania. Mkoa una shughuli nyingi za kiserikali na Binafsi kuanzia ngazi ya mkoa hadi kitaifa zinazofanyikia mkoani hapa.

Kwa kiasi kikubwa uchumi wa Mkoa wa Dodoma unategemea kilimo hasa kilimo cha mazao ya chakula na biashara. Mazao yanayozalishwa kwa wingi katika ukanda huu ni pamoja na mahindi, mtama, mtama, mchele, alizeti na zabibu. Lakini pia huduma za Viwanda, Ujenzi na biashara.

Mfuko kupitia ofisi yake ya mkoa wa Dodoma umeshiriki katika matukio na hafla za kitaifa za serikali lengo ni kuhakikisha huduma za bima zinawafikia Wananchi kwa; kutoa huduma za bima, elimu na ushiriki katika matukio yote yanayofanyika mkoani hapa.
Ushiriki wa Mfuko katika shughuli hizi za serikali ya awamu ya sita (6) zimechochea mahusiano chanya kati ya Ofisi za Serikali zikiwemo za watoa huduma za matibabu kwa wananchi, Taasisi binafsi, Watumishi,Wafanyabiashara na Wakulima, hivyo kupelekea ukuaji wa uelewa kuhusu Mfuko katika mkoa wa Dodoma

Katika kipindi cha Serikali ya Awamu ya Sita, Mkoa wa Dodoma umekuwa na mafanikio katika Nyanja mbalimbali ambazo ni pamoja na;-

- **Maboresho ya huduma za Matibabu**

Mfuko kupitia mpango mkakati wa serikali ya awamu ya sita kuhakikisha kuwa kila mwananchi anapata huduma za Bima ya Afya,sheria Namba 13 ya mwaka 2023 inayohusu Bima ya Afya kwa wote ilipitishwa.

Katika kufanikisha mpango huu, kabla sheria rasmi kuanza kutumika Mfuko uliboresha vifurushi vyake na kuja na vifurushi vilivyokidhi mahitaji ya wananchi na kwa makundi yote ambavyo ni Tarangire,Ngorongoro,Mikumi,Serengeti,Tanzanite.na Mpango wa Toto afya pia uliboreshwa ili kuwafikiwa wanufaika wengi zaidi.

- **Wigo wa Wanachama Waongezeka**

Maboresho haya ya vifurushi yamewezesha ongezeko kubwa la wanachama ambapo ofisi ya Mkoa wa Dodoma kusajili Wanachama 265,930 hadi kufikia kipindi cha mwaka 2025.

- **Usajili wa vituo vya kutolea huduma**

Juhudi hii ya serikali ya awamu ya sita imewezesha kuwa na ongezeko la usajili wa vituo vya kutolea huduma za matibabu.Hadi kufikia mwaka 2025 Mkoa umeweza kusajili jumla ya vituo 543 kutoka vituo 450 ambavyo vilikuwa vimesajiliwa awali ili kutoa huduma za matibabu katika mkoa wa Dodoma.Hili ni ongezeko la vituo 93

• Malipo kwa vituo vya kutolea huduma

Mfuko umehakikisha kuwa madai ya vituo vya huduma yamelipwa kwa wakati kwa watoa huduma ambapo kwa kipindi cha miaka minne jumla ya Shilingi 34,787,166,578 zimelipwa kwa vituo vyote vilivyosajiliwa mkoani Dodoma.

• Bilioni 4 zatolewa Mikopo ya vifaa Tiba

Katika kuhakikisha kuwa vituo vya kutolea huduma vinafanikisha lengo la msingi la kutoa huduma, Serikali ya awamu ya sita (6) kupitia Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya,kupitia Mkoa wa Dodoma umeweza kutoa mkopo wa vifaa tiba katika vituo 10 vya kutolea huduma ambapo jumla ya Shilingi 4,029,270,768. Uboreshaji huu wa huduma umekuwa kivutio kwa wananchi kujiunga na bima ya afya na kuwa na uhakika wa kupata huduma za matibabu.

• Elimu wa Umma

Mfuko umeweza kushiriki katika utoaji wa elimu ya umuhimu kwa Wananchi kuwa na Bima ya Afya katika hafla na matukio mbalimbali ikiwemo maonyesho ya kiserikali ambayo yamekuwa yakifanyika mkoani Dodoma kama vile Nane Nane. Mfuko pia umekuwa ukitoa elimu kupitia vituo mbalimbali vya redio mkoani Dodoma .Kupitia hafla hizi Wananchi wameweza kufikiwa na elimu ya dhana ya bima ya afya.

Mafanikio haya yaliyopatikana katika kipindi cha Serikali ya Awamu ya Sita mkoani Dodoma chini ya uongozi mahiri wa Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano waTanzania,yamewezesha wananchi wengi wa mkoa wa Dodoma kuwa na uelewa kuhusu Bima ya Afya kwa wote ambayo itamsaidia kila atakayejisajili kuwa na uhakika wa matibabu ambalo ni jukumu kubwa la Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya

Ofisi ya Dodoma inatoa wito kwa wananchi kutumia fursa ya Bima ya Afya kwa Wote ili kuwa na uhakika wa kupata huduma za matibabu wakati wote bila kikwazo cha fedha.

Dkt. Gwamaka Edward
Kaimu Mwenyekiti wa TUGHE

TUGHE TAWI INAVYOSHIRIKIANA NA MENEJIMENTI

Ni kuhakikisha Watanzania wanakuwa na bima ya afya

Chama cha Wafanyakazi wa Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya (NHIF), ni kati ya vyama vya wafanyakazi ambavyo vinaendeshwa kwa kuzingatia sheria, taratibu na miongozo huku kipaumbele chake kikiwa ni utulivu mahala pa kazi.

Katika kipindi cha miaka minne ya Serikali ya Awamu ya Sita, Tughe Tawi imeendelea kushirikiana na Menejimenti kuandaa mpango wa motisha kwa Watumishi ikiwa ni pamoja na kuhamasisha watumishi kuendelea kufanya kwa bidii ili kufikia malengo yaliyowekwa na Serikali kwa Mfuko.

Ili kuhakikisha haki za Watumishi zinapatikana kwa wakati, Chama kimeshirikiana na Uongozi wa Mfuko katika kushughulikia mashauri mbalimbali ya Watumishi hali inayoleta utulivu na usalama mahalai pa kazi.

Hivi karibuni Mkurugenzi Mkuu Dkt. Irene Isaka alipohudhuria Mkutano Mkuu wa TUGHE, alipongeza watumishi wa Mfuko kupitia TUGHE kwa mafanikio ya kiutendaji lakini pia akahimiza kuendelea kujituma na kuwa wabunifu ili kuongeza idadi na michango ya wanachama.

Dkt. Isaka alisisitiza dhamira ya NHIF ya kuinua hali za wafanyakazi na kuhimiza mazungumzo endelevu kati ya uongozi na chama cha wafanyakazi ili kuhakikisha mazingira mazuri ya kazi.

Kukamilika kwa Mkutano huo, kulikuwa na mafanikio yanayoashiria kuimarisha hali wa wafanyakazi wa NHIF, sambamba na kukuza ubora wa taaluma katika taasisi. Wanachama wa chama pamoja na uongozi walionyesha matumaini kuhusu ushirikiano endelevu unaolenga kuboresha ustawi wa wafanyakazi na kuendeleza utoaji huduma bora kwa Watanzania.

Je ni sahihi kumuazima mtu kitambulisho changu cha NHIF ili apate matibabu?

Hapana sio sahihi na ni kosa kisheria. Usiazime wala kutumia kitambulisho kisicho chako na hatua kali zitachukuliwa kwa wanaobainika.

NATIONAL HEALTH INSURANCE FUND
NHIF
Dedicated to providing quality health Care
ISO 9001:2015 CERTIFIED
Jiunge na NHIF wewe na familia yako kwa Uhakika wa Matibabu

JARIDA HILI HUANDALIWA NA KUCHAPISHWA
NA MFUKO WA TAIFA WA BIMA YA AFYA
S.L.P 1437 DODOMA
TANZANIA

WAANDAJI WA JARIDA

James Mlowe
Mhariri

Catherine Kameka
Mhariri

Grace Kisinga
Mwandaaji wa habari

Theresia Mallya
Mwandaaji wa habari

Elisha Mwanjoka
Msanifu wa kurasa

Charles Madangi
Msanifu wa kurasa

BIMA YA AFYA KWA WOTE,
JIUNGE SASA

MAKAO MAKUU
Jengo la NHIF,
2 Barabara ya Ukaguzi,
S.L.P 1437,
41104 Tambukareli,
DODOMA.
Simu: +255 26 2963887/8
Barua pepe: info@nhif.or.tz

Anuani za Ofisi za NHIF

MAKAO MAKUU
Jengo la NHIF,
2 Barabara ya Ukaguzi,
S.L.P 1437,
41104 Tambukareli,
DODOMA.
Simu: +255 26 2963887/8
Barua pepe: info@nhif.or.tz

ILALA
Ofisi ya Mkoa wa Ilala,
Jengo la NSSF Mafao House,
Ilala Boma,
S.L.P 7195,
DAR ES SALAAM.
Simu: +255 22 2183797
Barua pepe: infoilala@nhif.or.tz

GONGO LA MBOTO
Ofisi ya Gongo la Mboto,
Ukonga, Jengo la Magereza Mkoa,
S.L.P 7195,
DAR ES SALAAM.
Simu: +255 737 221935
Barua pepe: infoilala@nhif.or.tz

TEMEKE
Ofisi ya Mkoa wa Temeke,
Kurasini Bendera Tatu,
S.L.P 45777,
DAR ES SALAAM.
Simu: +255 734 203163
Barua pepe: infotemeke@nhif.or.tz

KIGAMBONI
Ofisi ya Kigamboni,
Jengo la Kibada Gardens,
Barabara ya Mjimwema Kongowe,
Mtaa wa Kifurukwe,
S.L.P 45777,
DAR ES SALAAM
Simu: +255 734 203164
Barua pepe: infotemeke@nhif.or.tz

KINONDONI
Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya (NHIF),
Ofisi ya Mkoa wa Kinondoni,
Jengo la PSSSF Commercial Complex,
Barabara ya Sam Nujoma,
S.L.P 32668,
DAR ES SALAAM.
Simu: +255 733 242199
Barua pepe: infokinondoni@nhif.or.tz

UBUNGO
Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya (NHIF),
Ofisi ya Ubungo,
Jengo la Utawala, Ghorofa ya Pili
Stendi ya Magufuli - Mbezi,
Barabara ya Morogoro,
S.L.P 34562,
DAR ES SALAAM.
Simu: +255 733 242199
Barua pepe: infokinondoni@nhif.or.tz

MOROGORO
Ofisi ya Mkoa wa Morogoro,
Jengo la Kenya Commercial Bank (KCB), Ghorofa ya Pili,
Barabara ya Boma,
S.L.P 955,
MOROGORO.
Simu: +255 734 116860
Barua pepe: infomorogoro@nhif.or.tz

DODOMA
Ofisi ya Mkoa wa Dodoma,
Jengo la NHIF, Tambukareli,
Barabara ya Jakaya Kikwete,
Ghorofa ya Chini,
S.L.P 2221,
DODOMA.
Simu: +255 26 2963887/8, +255 737 708749
Barua pepe: infododoma@nhif.or.tz

KIBAHA
Ofisi ya Mkoa wa Pwani,
Jengo la Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya,
Barabara ya Stendi Mpya
S.L.P 30438,
KIBAHA – PWANI.
Simu: +255 735 445509, +255 734 130295, +255 734 130296
Barua pepe: infokibaha@nhif.or.tz

TANGA
Ofisi ya Mkoa wa Tanga,
Jengo la Old Revenue, Ghorofa ya Chini,
Mtaa wa Swahili,
S.L.P 5486,
TANGA.
Simu: +255 27 2645415
Barua pepe: infotanga@nhif.or.tz

RUKWA
Ofisi ya Mkoa wa Rukwa,
Jengo la NHIF,
Mtaa wa National Housing – Jangwani,
S.L.P 225,
SUMBAWANGA.
Simu: +255 25 2800358
Barua pepe: inforukwa@nhif.or.tz

TABORA
Ofisi ya Mkoa wa Tabora,
Jengo la Chuo cha Afya na Sayansi Shirikishi, Ghorofa ya Chini,
Barabara ya Kazehili,
S.L.P 1654,
TABORA.
Simu: +255 734 198580, +255 734 198582, +255 734 198583
Barua pepe: infotabora@nhif.or.tz

KILIMANJARO
Ofisi ya Mkoa wa Kilimanjaro,
Jengo la NSSF,
Makutano ya Barabara ya Old Moshi na Bath/Upinde,
S.L.P 8998,
MOSHI – KILIMANJARO.
Simu: +255 27 2755143, +255 27 2754264
Barua pepe: infomoshi@nhif.or.tz

ARUSHA
Ofisi ya Mkoa wa Arusha,
Jengo la NSSF Kaloleni Plaza,
Ghorofa ya Pili,
S.L.P 16110,
ARUSHA.
Simu: +255 27 2520026, +255 27 2520027
Barua pepe: infoarusha@nhif.or.tz

RUVUMA
Ofisi ya Mkoa wa Ruvuma,
Jengo la CWT, Ghorofa ya Pili,
Mtaa wa Zanzibar,
S.L.P 160,
SONGEA.
Simu: +255 25 2602908, +255 737 917889
Barua pepe: inforuvuma@nhif.or.tz

KAGERA
Ofisi ya Mkoa wa Kagera,
Jengo la NSSF Mafao House
Barabara ya Jamhuri,
S.L.P 1950,
BUKOBA.
Simu: +255 28 2221193, +255 736 120740
Barua pepe: infokagera@nhif.or.tz

SINGIDA
Ofisi ya Mkoa wa Singida,
Jengo la NHC Singidani Complex,
Barabara ya Arusha,
S.L.P 762,
SINGIDA.
Simu: +255 26 2502236
Barua pepe: infosingida@nhif.or.tz

KIGOMA
Ofisi ya Mkoa Kigoma,
Jengo la NHC Biashara House, Ghorofa ya Pili,
Barabara ya Lumumba,
S.L.P 1165,
KIGOMA.
Simu: +255 28 2802650
Barua pepe: infokigoma@nhif.or.tz

MARA
Ofisi ya Mkoa wa Mara,
Jengo la NHC, Ghorofa ya Kwanza,
Makutano ya Mtaa wa Ghandhi na Kusaga,
S.L.P 1348,
MUSOMA.
Simu: +255 28 2620554
Barua pepe: infomara@nhif.or.tz

IRINGA
Ofisi ya Mkoa wa Iringa,
Jengo la NHIF,
Barabara ya Mapinduzi - Gangilonga,
Jengo la NHIF,
S.L.P 2486,
IRINGA.
Simu: +255 26 2701276
Barua pepe: infoiringa@nhif.or.tz

MBEYA
Ofisi ya Mkoa wa Mbeya,
Jengo la NHIF Tower,
Barabara ya Karume,
Ghorofa ya Kwanza,
S.L.P 6137,
MBEYA.
Simu: +255 25 2500656
Barua pepe: infombeya@nhif.or.tz

ZANZIBAR
Ofisi ya Zanzibar,
Michenzani Mall
Ghorofa ya Nne,
S.L.P 4888,
ZANZIBAR.
Simu: +255 24 22372247,
Fax: +255 24 22372242,
Barua pepe: infozanzibar@nhif.or.tz

MANYARA
Ofisi ya Mkoa wa Manyara,
Jengo la BAWASA, Mkabala na TRA,
Ghorofa ya Kwanza,
S.L.P 430,
BABATI - MANYARA.
Simu: +255 27 2510022
Barua pepe: infomanyara@nhif.or.tz

LINDI
Ofisi ya Mkoa wa Lindi,
Jengo la CWT, Ghorofa ya Kwanza,
Mtaa wa Msonobalini,
S.L.P. 51,
LINDI.
Simu: +255 23 2202901
Barua pepe: infolindi@nhif.or.tz

SIMIYU
Ofisi ya Mkoa wa Simiyu,
Jengo la Nsagali,
Mtaa wa Salunda,
S.L.P 471,
BARIADI – SIMIYU.
Simu: +255 738 160182
Barua pepe: infosimiyu@nhif.or.tz

KATAVI
Ofisi ya Mkoa wa Katavi,
Jengo la NHC,
S.L.P 223,
MPANDA - KATAVI.
Simu: +255 25 2820147
Barua pepe: infokatavi@nhif.or.tz

NJOMBE
Ofisi ya Mkoa wa Njombe,
Jengo la NSSF - Mafao House,
Mtaa wa Nazareth, Barabara ya Songea,
S.L.P 1085,
NJOMBE.
Simu: +255 26 2782199
Barua pepe: infonjombe@nhif.or.tz

GEITA
Ofisi ya Mkoa wa Geita,
Majengo ya Halmashauri (W) Geita,
Mtaa wa Bomani,
S.L.P 482,
GEITA.
Simu: +255 28 2520170
Barua pepe: infogeita@nhif.or.tz

MWANZA
Ofisi ya Mkoa wa Mwanza,
Jengo la TMDA, Ghorofa ya Pili,
Nyakato Buzuruga,
S.L.P 1187,
MWANZA.
Simu: +255 28 2981299
Barua pepe: infomwanza@nhif.or.tz

SHINYANGA
Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya (NHIF),
Ofisi ya Mkoa wa Shinyanga,
Jengo la NSSF,
Barabara ya Mwanza,
S.L.P 230,
SHINYANGA.
Simu: +255 28 2763708
Barua pepe: infoshinyanga@nhif.or.tz

MTWARA
Ofisi ya Mkoa wa Mtwara,
Jengo la Raha Leo Complex, Ghorofa ya Tatu,
Barabara ya Chikongola,
S.L.P 484,
MTWARA.
Simu: +255 657 249342, +255 752 524255, +255 685 272878
Barua pepe: infomtwara@nhif.or.tz

SONGWE
Ofisi ya Mkoa wa Songwe,
Jengo la CWT,
Old Vwawa,
S.L.P 186,
SONGWE.
Simu: +255 25 2580157
Barua pepe: infosongwe@nhif.or.tz